# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SITA

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Januari, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

### KIAPO CHA UAMINIFU

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliapa:

Mhe. Abdallah Majula Bulembo;
Mhe. Anne Kilango Malecela;
Mhe. Juma Ali Juma;
Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tusikilizane tuweze kuendelea baada ya magoli hayo manne. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Tano wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa mwaka 2016 *(The Media Services Bill, 2016)* na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *(Na. 3)* wa mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2016)*; Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo miwili imekwisha pata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi ambazo zinaitwa; Sheria ya Huduma za Habari (Na.12) ya 2016 *(The Media Services Act (No.12) of 2016)* na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, (Na. 3 na Na.13) ya mwaka *2016 (The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.3 and No. 13) Act, 2016),* hiyo ndiyo taarifa ambayo ningependa niwape.

Waheshimiwa Wabunge, pia ninapenda kutumia nafasi hii kuwapa maelezo kuhusiana na ushiriki wa timu yetu ya *Bunge Sports Club* kwenye michezo ya Mabunge ya nchi za Afrika Mashariki iliyofanyika Mjini Mombasa, Kenya kati ya terehe 4 na 10 Disemba 2016.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba baada ya Mkutano wa Tano wa Bunge kumalizika, timu yetu ya *Bunge Sports Club* ilipata nafasi ya kushiriki katika michezo ya Mabunge ya Nchi za Afrika Mashariki iliyofanyika Jijini Mombasa nchini Kenya iliyofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 10 Disemba, 2016. Katika michezo hiyo, kwa kweli timu yetu iliweza kutuwakilisha vizuri sana na imeweza kudhihirisha kuwa ilienda kushindana na siyo kwenda kushiriki tu. Hivyo ninayo furaha kuwataarifu kuwa katika mashindano hayo ambayo yalijumuisha michezo mbalimbali, timu yetu ya Bunge imeweza kushika nafasi za juu pamoja na kushinda medali mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kwanza, mchezo wa mpira wa pete imeshika nafasi ya pili, mpira wa miguu timu yetu ya *Bunge Sports Club* imeshika nafasi ya tatu, mpira wa wavu wanawake, imeshika nafasi ya tatu, mchezo wa kuvuta kamba timu yetu imeshika nafasi ya tatu. *(Makofi)*

Aidha, baadhi ya wachezaji wa timu yetu ya Bunge waliweza kushinda medali za ubora katika michezo mbalimbali kutokana na vipaji na ubora waliouonesha katika michezo hiyo na wachezaji hao ni hawa wafuatao:-

Kwanza Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu na Mheshimiwa Venance Methuselah Mwamoto. Pamoja na Wabunge hao, pia aliyekuwa Mbunge wa Dimani, Marehemu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliweza kutunukiwa medali ya Mbunge aliyeshiriki mashindano hayo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza timu yetu ya Bunge kwa ushindi wa nafasi hizo walizoshika pamoja na washindi wote wa medali mbalimbali. Hii imedhihirisha kwamba umahiri wetu haupo kwenye kujenga hoja za kisiasa ndani ya Bunge peke yake bali hata kwenye masuala ya michezo. Kipekee kabisa nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kwa ushindi wa medali nyingi katika michezo mbalimbali pamoja na kutuletea sifa nyingi sana kama Bunge na kama nchi na hatimaye kuacha gumzo kubwa miongoni mwa washiriki wa mashindano hayo. Mheshimiwa Esther Matiko alionesha uzalendo wa hali ya juu katika michezo yote kwani licha ya kipaji alichokionesha pia aliweza kushiriki michezo mingi aliyojishindia medali mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwisho napende kuchukua nafasi hii kuendelea kuwahamasisha Waheshimwa Wabunge wote kuwa na utamaduni wa kutenga muda wa kufanya mazoezi kwa ajili ya afya zetu wenyewe pia kwa ajili ya kujiandaa na michezo mbalimbali ya kirafiki. Ikumbukwe kwamba kwa mwaka huu 2017 mashindano haya mwishoni mwa mwaka huu yatafanyika hapa Dodoma, kwa hiyo tunatarajia ushiriki wa Wabunge kuwa mkubwa zaidi na katika michezo mingi zaidi. *(Makofi)*

Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali na swali la kwanza kama ilivyo ada tunaanza leo na Ofisi ya Mheshimiwa Rais - TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Handeni, Omari Abdallah Kigoda.

Na. 1

**Hospitali ya Wilaya ya Handeni Kupatiwa Vifaa Tiba na Wauguzi**

**MHE. OMARI A. KIGODA** Aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Handeni inahudumia wagonjwa kutoka Kilindi, Mziha, Wegero na Handeni yenyewe.

Je, ni lini Serikali itaipatia vifaa tiba na wauguzi wa kutosha hospitali hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Said Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mahitaji ya vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni, Serikali imetenga shilingi milioni 181.9 katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Fedha zote zimeshapokelewa na zimetumika kununulia vifaa tiba vinavyohitajika kusaidia utoaji wa huduma vikiwemo *BP machine,* vifaa vya kupimia kiwango cha damu, vifaa vya kujifungulia na kupima upumuaji wa watoto, pamoja na kulipia gharama za manunuzi ya jokofu katika chumba cha kuhifadhia maiti.

Halmashauri imeomba mkopo kutoka Bima ya Afya ya Taifa *(NHIF)* ili kununua *ultra-sound* yenye thamani ya shilingi milioni 75. Halmashauri imeahidi kurejesha fedha zote kupitia makusanyo ya Tele kwa Tele ya Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)*.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi katika Hospitali hiyo ni 359, watumishi waliopo ni 170 na upungufu ni watumishi 189. Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri watumishi 118 katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo baadhi ya watumishi hao watapelekwa katika Hospitali ya Wilaya. Kati ya watumishi hao walioombwa, watumishi 49 ni wauguzi, watumishi 25 ni madaktari na kada nyingine ni watumishi 44.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigoda swali la nyongeza.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa Serikali imeshatoa kibali cha kupeleka wauguzi kule na ukizingatia kwamba hospitali ina upungufu wa wauguzi zaidi ya asilimia 60. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kupeleka hao wahudumu ukizingatia kwamba hali ya kule siyo nzuri kwa sasa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wenzetu wa Handeni waliomba kibali. Naomba niseme kwamba ni vibali katika kada mbalimbali zimeombwa, lakini naomba niwahakikishie wazi kwamba, kwa sababu mchakato wa utoaji wa vibali ulishaanza katika sekta ya elimu hasa katika suala zima la walimu wa sayansi, kwa kadri Serikali itakavyoona inafaa tutajitahidi kuhakikisha tunapeleka nguvu na hasa vile vibali ambavyo vimebainishwa.

Ofisi ya Utumishi ikishatoa *go ahead* katika maeneo mbalimbali, tutashiriki kuona ni jinsi gani tutafanya kuongeza watumishi, tukijua kwamba siyo sekta ya afya peke yake isipokuwa kada mbalimbali zina matatizo makubwa sana na hivyo ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba tunafanya kila iwezekanavyo ili wananchi waweze kupata huduma inayostahiki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Omari naomba ondoa hofu katika hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, changamoto katika sekta ya afya ukiacha vifaa tiba, sasa hivi pameibuka changamoto kubwa mpya, ambao wananchi wanakuwa wakilipa bima zao za afya, wanakwenda katika hospitali, wanaandikiwa tu dawa lakini wanashindwa kupatiwa pale. Kwa hiyo, nilitaka nijue ipi ni kauli ya Serikali kwa wananchi ambao wamelipia bima zao lakini hawapati matibabu katika hospitali husika?

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Silinde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwananchi yeyote ambaye ana kadi ya Bima ya Afya anatakiwa kupata huduma zote za afya bure ikiwemo vipimo. Nikiri kwamba katika baadhi ya vituo vya afya vya umma, hasa nadhani unazungumzia *CHF* tuna changamoto ya upatikanaji wa dawa zote katika vituo vyetu, ndiyo maana Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya una maduka ya dawa ambapo kama umeiokosa ile dawa katika hospitali husika unatakiwa kwenda katika duka la dawa ambalo limetambuliwa na *NHIF*.

Mheshimiwa Spika, kwa *CHF* kidogo hapo niseme kuna changamoto. Kwenye mikoa ambapo tumeenda kwenye Bima ya Afya iliyoboreshwa wao wanaweza wakapata dawa katika maduka ya dawa, kwa hiyo tunaifanyia kazi changamoto hii.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata, swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza.

Na. 2

**Kuboresha Miundombinu ya Elimu Vijijini**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** Aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya elimu vijijini kama nyumba za walimu pamoja na kulipa malimbikizo ya madeni ya walimu wanayoidai Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaboresha miundombinu ya shule nchini kupitia mipango na bajeti ya Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi na wadau wa maendeleo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 13.9 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 1,157 kwa shule za msingi na shilingi bilioni 11.14 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 661 kwa shule za sekondari. Aidha, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES II),* Serikali imekamilisha ujenzi wa nyumba 146 kati ya nyumba 183 ambazo kila nyumba wataishi watumishi sita (walimu). Ujenzi wa nyumba hizo umegharimu shilingi bilioni 21.9. Nyumba 37 zinaendelea kujengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 5.5 na zitakamilika tarehe 30 Aprili, 2017.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulipa madeni ya walimu kadri yanavyojitokeza na kuhakikiwa. Katika mwezi Oktoba, 2015 Serikali ililipa madeni ya shilingi bilioni 20.12 kwa walimu 44,700 na shilingi bilioni 1.107 zililipwa mwezi Februari, 2016 kwa walimu 3,221. Hivi sasa walimu wanadai Serikali madeni yanayofikia shilingi bilioni 26.04 kwa ajili ya walimu waliopo kazini 33,620 na walimu wastaafu 2,134. Deni hilo limewasilishwa Hazina kwa ajili ya taratibu za mwisho za kulipwa kwa walimu wanaodai.

**SPIKA:** Lah! Hili swali mbona limekuwa taabu tena, Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri, lakini ni wazi kwamba kwa miaka mingi sana Serikali haijatoa kipaumbele kwa suala la nyumba za walimu. Kwa mfano, kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imepanga kujenga nyumba 1,818, ukiangalia nikitumia Mbozi kama *case study* ya Mkoa wa Songwe, kuna uhaba wa nyumba za walimu 1,432. Je, ni lini sasa Serikali italeta mpango kabambe wa kumaliza tatizo la nyumba za walimu hasa wa vijijini ili iwe kama motisha?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri ambacho nilitaka kufahamu kwamba je, ni lini madeni hayo ya walimu yataanza kulipwa kwa sababu ukisema kwamba yamepelekwa tu Hazina bado haileti tija kwa walimu wa Tanzania. Ninataka kujua kwamba ni lini rasmi madeni hayo yataanza kulipwa?

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, najua Mbunge anaguswa sana na sekta ya elimu na nikupongeze sana kwa sababu ukiwa kijana lazima uguswe na elimu.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi na mkakati wa Serikali nimezungumza pale awali. Kwa vile tumebaini changamoto ya nyumba za walimu ndiyo maana Serikali katika bajeti ya mwaka huu tunaoenda nao imetenga takribani shilingi bilioni 13, hii ni kwa ajili ya nyumba za walimu wa shule za msingi peke yake, lakini shilingi bilioni 11 kwa ajili ya shule za sekondari. Hata hivyo, *commitment* katika mpango mwingine wa *MMES II,* nimezungumza hapa karibuni nyumba zipatazo140 tumeshazikamilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge katika ziara zangu katika Mikoa mbalimbali, miongoni mwa mambo ninayoyatilia kipaumbele sana ni kukagua ujenzi wa nyumba za walimu. Naomba niwapongeze Wabunge wote kwa ujumla wetu katika maeneo yetu nilipopita nimekuta ujenzi wa nyumba za walimu kwa kweli unaenda kwa kasi sana. Kwa vile katika *commitment* ya Serikali imeshatenga hizi fedha, naomba niwaambie fedha tunaendelea kuzipeleka katika Halmashauri zetu, lengo kubwa walimu waweze kupata mazingira salama ya kuweza kuishi.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la madai ya walimu, nimesema kwamba sasa hivi tumeshahakiki deni la shilingi bilioni 26.04 na haya ni madeni yasiyo ya mshahara. Maana yake Serikali haiwezi kulipa madeni lazima kwanza kuweza kuhakiki, ndiyo maana nimesema zoezi la uhakiki limeisha Oktoba, 2016. Sasa hivi ni mchakato ambao upo katika Wizara ya Fedha kwa utaratibu wa mwisho wa kuweza kulipa. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira tu kwa sababu kigezo kikubwa ni kwamba ni lazima deni lihakikiwe na madeni haya yameshahakikiwa na naomba niwaambie walimu wa Tanzania kwamba wawe na subira kipindi siyo kirefu, Hazina kwa kadri inavyojipanga, madeni haya yanaweza kulipwa walimu mbalimbali ili mradi wapate haki zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Nagu nilikuona.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Serikali ningependa ijue kwamba kuna wananchi waliojitolea kwa kujua umuhimu wa walimu kujenga maboma kwa ajili ya nyumba za walimu, pamoja na madarasa.

Je, Serikali itatoa kipaumbele kwa wale wananchi ambao wameonesha umuhimu wa walimu na umuhimu wa elimu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, jibu ni ndiyo Serikali itatoa. Ndiyo maana hivi sasa tumeshaleta fedha karibu awamu mbili za *Capital Development Grand,* ambapo katika baadhi ya Halmashauri imeshaanza kuweka kipaumbele kumalizia nyumba za walimu. Maeneo niliyofika zile fedha zilizofika, utakuja kuona yale maboma ambayo mwanzo yalibakia sasa hivi utakuta yanakamilishwa. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali, naomba nikupongeze na hili ni jukumu la kwetu sote Wabunge zile fedha zinavyopita ni lazima tuzisimamie vizuri, tuende tukamalize haya maboma yaliyopo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholas Matiko swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naitwa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba ukosefu wa nyumba za walimu na kukaa mbali na shule unasababisha kutokuwa na kiwango kizuri cha ufundishaji kwenye shule zetu. Hivi karibuni tulisikia kauli ya Waziri Mkuu akitoa msisitizo kwamba walimu waishi kwenye shule ambazo wanafundisha. Kwa majibu ya Naibu Waziri ni dhahiri bado Serikali haijawa na mpango madhubuti wa kuhakikisha walimu wanakaa kwenye maeneo ambayo wanafundisha.

Ni nini mpango mkakati wa Serikali hasa kwa pale ambapo wananchi wamejenga maboma wanashindwa kuyamalizia ili watoto wetu waweze kupata elimu mbadala kwa Walimu kukaa maeneo ya shule. Napenda kupata mkakati ambao unatekelezeka siyo wa kuandikwa tu kwenye makaratasi, ahsante.

**SPIKA:** Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa George Simbachawene majibu tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza na kuongezea kwenye swali la msingi pia ambalo limejibiwa na Naibu Waziri vizuri kabisa, Mheshimiwa Jafo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna mahitaji makubwa ya madarasa, tuna mahitaji makubwa ya nyumba za walimu. Kwa mfano, tuna upungufu wa madarasa katika shule ya msingi kwa sasa 127,745. Tuna upungufu wa madarasa kwa shule za sekondari 10,204. Hali kadhalika tuna upungufu wa

nyumba za walimu. Mipango yote, mpango uwe mpango mkakati, uwe mpango wa haraka, uwe mpango wa dharura, inafanyika kwenye Halmashauri zetu. Tusitegemee kwamba tutakuja na mpango fulani nje ya mipango ile ya Halmashauri, kwa sababu Serikali kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa sheria, tunatekeleza dhana ya ugatuaji wa madaraka.

Mheshimiwa Spika, kugatua madaraka maana yake ni kwamba tupange vipaumbele sisi tulioko huko kwa wananchi. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza sana wananchi wote wa Tanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kwa namna tulivyoshirikiana vizuri sana katika suala la kupunguza upungufu wa madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo sasa, tuangalie namna ya kwenda kwenye mchakato wa kupunguza tatizo la nyumba za walimu na madarasa. Tukifikiri kuna njia nyingine nadhani tutakuwa tunajidanganya, ukweli ni kwamba lazima tujipange wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu tunayoiandaa, msisitizo mkubwa ambao tumeelekeza Halmashauri sisi TAMISEMI ni kwamba wajipange sana kuweka fedha nyingi na mipango mikubwa kwenye madarasa na nyumba za walimu. Hii itatusaidia ili hata Serikali kama ikitoa fedha yoyote ile, itakwenda kwa njia hiyo ili kutekeleza upungufu uliopo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumzia zile nyumba za sita kwa moja nadhani zinazojengwa hivi sasa, sijui Waheshimiwa Wabunge wenzangu huko kwenye Majimbo yenu lakini kwa kweli zile nyumba ni maoni yetu kule Kongwa kwamba hazifai kabisa. *(Makofi)*

Unawaweka walimu sita mahali pamoja, mlango, mlango, chumba kimoja sijui na sebule, yaani hata yule manamba wa kule Tanga ana afadhali kidogo kuliko mwalimu wa sekondari. Ile ramani TAMISEMI muingalie, ile hapana kabisa. Unasafiri unaacha mke wako jirani yuko hapo hapo, sasa usalama utakuwa uko wapi? Mheshimiwa Jafo kaliangalie hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Swali la tatu Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe.

Na. 3

**Upandishaji Hadhi Vituo vya Afya**

**MHE. ESTER A. MAHAWE** aliuliza:-

Wilaya ya Simanjiro haina Hospitali ya Wilaya na hivyo kusababisha mateso kwa wakazi wa maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo hususan wanawake ambao wanakosa huduma za kujifungua lakini pia kutokana na uchache wa vituo vya afya na zahanati.

(a) Je, ni lini Serikali itavipa hadhi vituo vya afya vya Mererani na Orkesment ili kupunguza tatizo?

(b) Wilaya ya Simanjiro ina gari moja tu la wagonjwa; je, ni lini Serikali itapeleka gari lingine kwenye Kituo cha Afya Mererani ili kuokoa maisha ya akina mama wajawazito?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maombi ya kupandisha hadhi Kituo cha Afya Orkesment kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kuwa Hospitali Teule ya Wilaya tayari yamewasilishwa katika Wiazara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto mwezi Oktoba, 2016 kwa uamuzi, baada ya kujadiliwa na kukubalika katika vikao ngazi ya Halmashauri na Mkoa. Kibali kikipatikana Serikali itaingia mkataba rasmi wa utoaji huduma na mmiliki wa kituo hicho ili kuainisha majukumu ya kila mdau. Aidha, Halmashauri imepokea shilingi milioni 80.0 zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi katika kituo cha afya cha *Urban Orkesment* kinachomilikiwa na Serikali. Taratibu za kumpa Mkandarasi zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri imetenga gari moja ambalo linatumika kutoa huduma za dharura kwa wagonjwa wenye rufaa. Gari hilo hutoa huduma kwa wagonjwa katika vituo vyote kikiwemo Mererani pale inapotokea dharura.

Hata hivyo, gari hilo ni chakavu kiasi cha kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara. Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro imeshauriwa kuweka kipaumbele na kutenga bajeti katika mwaka 2017/2018 kwa ajili ya ununuzi wa gari la kuhudumia wagonjwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mahawe swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza linasema kwamba kuna uhaba mkubwa wa watumishi wa kada ya afya, hasa katika Mkoa wa Manyara kwenye zahanati na vituo vya afya. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha hilo nalo linatatuliwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili tuna upungufu wa dawa hususan Mkoa wa Manyara kwenye hospitali zake zote Je, Serikali ina mpango gani na hili maana afya za wananchi ziko hatiani? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika suala zima la watumishi kama tunavyojua ni kwamba maeneo mbalimbali yanakabiliwa na uhaba wa watumishi, hii tumesema ni *commitment* ya Serikali. Kama nilivyosema katika jibu wakati namjibu Mbunge wa Handeni kwamba Serikali sasa hivi mchakato wa vibali ukikamilika vizuri katika Ofisi ya Utumishi, basi nadhani tutapeleka watumishi kwa kadri maeneo yote yanayowezekana, *especially* katika Mkoa wako wa Manyara Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, suala zima la upungufu wa dawa ni kweli na naomba kila Mbunge hapa a-*pay attention* ya kutosha. Nimepita katika Halmashauri mbalimbali Serikali tumeamua kutoa fedha za *basket fund* awamu mbili zimekamilika, hivi sasa tumeshapeleka fedha za *basket fund* katika awamu ya tatu, lakini kwa bahati mbaya sana miaka yote uki-*track record* fedha za *basket fund* ambayo inakuonesha *one third* lazima itumike katika kununua madawa na vifaa tiba katika Halmashauri zetu fedha hizo hazitumiki sawasawa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine utakuta fedha tumezipeleka lakini wakati natembelea juzi, fedha za awamu ya kwanza na fedha za awamu ya pili

utafika katika Halmashauri bado fedha za *basket fund* kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa tiba hazijanunuliwa. Ndiyo maana tumetoa maelekezo kwa *DMO* wote wahakikishe kwamba fedha zilizopelekwa katika maeneo yao zinaenda kutatua matatizo ya wananchi kama tulivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, hili nimhakikishie Mheshimiwa Ester, juzi nilikuwa naongea na Mkurugenzi wako kule wa eneo lile na kumwelekeza kwamba zile fedha aweze kununua na ameniambia ameshanunua dawa nyingine, lakini kuna dawa zingine bado anaziomba kutoka *MSD,* kuna dawa zingine ameambiwa hazipatikani na nimewaelekeza kwamba, wafanye utaratibu kuzipata dawa hizo lengo kubwa ni wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma. Kwa hiyo, ni *commitment* ya Serikali na tunajitahidi kufanya kila liwezekanalo ili kuondoa hili tatizo la dawa nchini kote.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mohamed Amour Mohamed

Na. 4

**Unyanyasaji Unaofanywa na Vikosi vya SMZ Zanzibar**

**MHE. ALLY SALEH ALLY (K.n.y. MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED)** Aliuliza:-

Suala la usalama wa raia na mali zao ni moja ya dhamana ya Jeshi la Polisi nchini; ni muda sasa Zanzibar wananchi wamekuwa wakipigwa, kunyanyaswa na kunyang'anywa mali zao kunakofanywa na vikosi vya SMZ.

Je, nini kauli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusiana na matukio hayo huko Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa usalama wa raia na mali zao ndiyo dhamana kuu au kazi ya msingi ya Jeshi la Polisi nchini. Taarifa hizo hadi sasa hazijapata uthibitisho sahihi kutoka kwa wale ambao wanadai kutendewa vitendo hivyo, kwani hakuna taarifa yoyote iliyoripotiwa kwenye vituo vya polisi

Visiwani Zanzibar kuhusiana na uhalifu huo. Kwa mujibu wa taratibu zilizopo ni kwamba mtu yeyote ambaye anafanyiwa kitendo chochote cha uhalifu anapaswa kutoa taarifa kwenye kituo cha polisi, ili hatua za kiuchunguzi na kiupelelezi zifanyike ili kubaini wahalifu ambao wamehusika na hatua stahiki za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi bado inasisitiza kuwa haitambui uwepo wa vitendo hivyo na inatoa wito kwa wananchi wote ambao watafanyiwa au wamefanyiwa vitendo kama hivyo, watoe taarifa kwenye vituo vya polisi au kwa viongozi wa polisi waliopo Makao Makuu Zanzibar na Dar es Salaam ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa dhidi ya vitendo hivyo kwa watuhumiwa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kweli hii ni *standard answer,* hata tungefumba macho tu tungejua kwamba jawabu lingekuwa hili. Ni kawaida swali hili limeulizwa hii mara ya tano tangu mimi kuingia Bungeni na Serikali yenye macho, masikio, yenye pumzi, inasema haijui chochote kinachotokea kule Zanzibar. Hili ni jambo la aibu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa je, kwa sababu hapa mimi mwenyewe nimeleta ripoti za haki za binadamu na nikawapa baadhi ya Mawaziri hapa kuonesha matendo yanayoonekana Zanzibar. Je, Bunge hili kwanza halioni wakati sasa umefika wa kuunda Tume ya Kibunge kuchunguza mambo yanayotokea Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu wananchi wa Zanzibar sasa hawana imani na vituo vya polisi ambako wamekuwa wakiripoti. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kutoa *commitment* humu ndani Bungeni leo kwamba tukutane Uwanja wa Amani tarehe ambayo yeye anataka, tumletee wananchi ambao wameonewa, wamenyanyaswa, wamepigwa, wamedhalilishwa, tumuoneshe kwamba watu wapo na ushahidi wa hili Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani akiri, mara ngapi nimemwandikia na hata siku moja hajaja Unguja wala Pemba tukafanya naye kazi kuhusu suala hili? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge ameshatoa hoja hizo na ameandika, lakini sehemu moja tu anasema Waziri wa Mambo ya Ndani hajaja Unguja ama Pemba. Mimi nimeshafika Unguja na Pemba na… *(Makofi)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Hujafika kwa walioathirika, tutafute sisi tukuoneshe!

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh, tafadhali! Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taratibu za utendaji wa kazi zinafanyika kwa kutumia vikao na baadhi ya Wabunge nilikutana nao, tena Wabunge wa Majimbo mpaka Pemba na Mheshimiwa Khatib ni Mbunge mmojawapo na nilionana naye.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba utaratibu wa upokeaji wa malalamiko upo kwa njia zilizo rasmi na hakuna utaratibu wa kuweka *parade* uwanjani kupokea malalamiko. Kwa sababu vitendo vya aina hiyo ikiwa vimetokea tunapokea malalamiko na kuna taasisi nyingine ambazo zinatakiwa ku-*verify* kwamba vile vilifanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ndiyo tunaanza tu Bunge leo, waelekeze watu wako na mimi nitawaelekeza watu wangu wafike na wafikishe hayo malalamiko, halafu *verification* zifanyike kujua ukweli wa hicho kinachofanyika.

Na. 5

**Kujenga Ofisi ya Polisi ya Wilaya ya Kigamboni**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Pamoja na Jimbo la Kigamboni ni Wilaya ya Kipolisi, majengo ya Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Wilaya *(OCD)* na kituo chake ni chakavu sana:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha Wilaya hii inakuwa na ofisi nzuri za polisi?

(b) Je, hatua hizi zitaanza kutekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kigamboni ni moja kati ya Wilaya tano za Mkoa wa Dar es Salaam ambayo imeanzishwa mwaka 2006 chini ya mpango wa maboresho ya Jeshi la Polisi kwa lengo la kuboresha na kusogeza

huduma za ulinzi na usalama karibu na wananchi. Kutokana na uhaba wa rasilimali fedha na majengo, huduma za kipolisi zilianza kutolewa katika jengo dogo la Kituo cha Polisi Kigamboni chenye hadhi ya Daraja la C.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inakusudia kujenga vituo vyote vya polisi kwenye Wilaya ambazo hazina majengo yenye hadhi stahiki ikiwemo Wilaya ya Kigamboni. Ujenzi wa kituo hicho utafanyika eneo la Kibada mara fedha zitakapopatikana.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Wilaya ya Kigamboni ina askari takribani 100, magari yanayofanya kazi matatu na nyumba chache sana za askari. Je, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ina mkakati gani wa kuongeza askari katika Wilaya mpya ya Kigamboni ili kukidhi mahitaji, hususan tukizingatia kwamba, Wilaya mpya ya Kigamboni ina changamoto kubwa sana ya uvuvi haramu, uhamiaji haramu pamoja na ongezeko la uhalifu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilitaka kujua; katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba ujenzi wa kituo kipya cha Wilaya utajengwa katika Kata ya Kibada mara fedha zitakapopatikana. Je, Wizara inaweza ika-*make commitment* kwamba itaingiza ujenzi wa kituo kipya cha Polisi cha Wilaya katika bajeti hii inayokuja ya mwaka wa fedha 2017/2018?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engineer* Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na pendekezo la Mheshimiwa Mbunge kuhusu haja ya kuongeza idadi ya Askari Kigamboni, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeliona hilo na tunategemea pengine katika askari ambao wanaweza wakaajiriwa katika mwaka ujao wa fedha tuweze kuangalia uwezekano wa kuongeza idadi ya askari katika maeneo yote ambayo kuna upungufu wa askari ikiwemo Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ametaka kujua kwamba katika bajeti ya mwaka huu wa fedha kwamba fedha hizo za ujenzi wa Kituo cha Kigamboni zitaingizwa. Naomba kwanza nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka sasa hivi hatua ambazo zimefikiwa ni hatua za kuridhisha kwani mbali na

kupatikana eneo la ujenzi wa kituo, lakini tayari hatua za awali ikiwemo utayarishaji wa ramani kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho umeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wazo lake tutazingatia ingawa inawezekana ikawa kwa bajeti ya mwaka huu ikawa tumechelewa, lakini tutaangalia utaratibu mwingine wa kuweza kuangalia jinsi gani ya kupiga hatua zaidi na pale ambapo tutaweza kuingiza katika bajeti ya mwaka mwingine wa fedha, tutaziingiza kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 6

**Ubakaji na Ulawiti kwa Watoto**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Tatizo la kesi za ubakaji na ulawiti kwa watoto wadogo limekuwa likiongezeka siku hadi siku katika Mkoa wa Iringa.

(a) Je, nini mkakati wa Serikali kunusuru hawa watoto wasiendelee kufanyiwa matendo haya ya kikatili?

(b) Je, ni utaratibu gani unatumika kushughulikia watuhumiwa wa kesi hizi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti vitendo hivi haramu dhidi ya watoto tumetunga sheria zenye adhabu kali kwa watuhumiwa wanaopatikana na hatia ya makosa ya ubakaji na ulawiti. Kifungu cha 136(1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, kimeweka adhabu ya kifungo cha maisha jela kwa mtu yeyote anayekutwa na hatia ya kubaka na kifungu cha 132(2) kinatoa adhabu ya kifungo cha miaka 14 jela kwa yeyote anayekutwa na hatia ya kujaribu kubaka. Aidha, kifungu cha 154 kimeweka adhabu ya kifungo cha miaka 14

jela kwa kosa la kulawiti. Lengo la kutoa adhabu hizo kali lilikuwa kutoa fundisho na onyo kwa yeyote mwenye dhamira ya kutenda makosa hayo ya jinai.

Mheshimiwa Spika, matukio mengi ya aina hiyo Mkoani Iringa yanahusisha ndugu au jamaa wa familia moja au sehemu moja. Ushahidi wa msingi hufichwa unapohitajika na wahusika wa pande zote mbili huyamaliza masuala husika kwa maelewano kifamilia na hivyo kuchochea matendo hayo ya jinai kushamiri.

Napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi kuvisaidia vyombo vya dola wakati wa upelelezi na uendeshwaji wa mashauri haya mahakamani ili kukomesha kabisa matukio hayo. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge na wenzako Mkoani Iringa kuwa mstari wa mbele katika kampeni hii ya kuomba ushirikiano na wananchi.

Mhesimiwa Spika, aidha, ili kuweka mazingira rafiki kwa waathirika na wananchi wenye taarifa au ushahidi wa aina hiyo, Serikali imeanzisha madawati ya jinsia katika vituo mbalimbali vya polisi yanayopokea taarifa mbalimbali kutoka kwa wananchi na kuliwezesha Jeshi la Polisi kuendesha upelelezi kwa ufanisi. Pindi, tukio la kubaka au kulawiti linaporipotiwa upelelezi hufanyika na mtuhumiwa hufunguliwa mashitaka mara moja.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika kushughulikia watuhumiwa wa kesi za kubaka na kulawiti umefafanuliwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16. Sheria hizi zimeainisha namna ya kushughulikia makosa hayo kuanzia wakati wa kupokea taarifa ya kutokea kitendo cha ubakaji na ulawiti mpaka hatua ya kutoa adhabu kwa wahusika wa vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taratibu za kisheria zilizoainishwa katika sheria hizo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa kesi za kubaka na kulawiti zinamalizika mapema na kuwa sheria zinasimamiwa ipasavyo.

Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kwa lengo la kujenga kesi na kuwa na ushahidi usiotia shaka ili kuiwezesha Mahakama kufikia maamuzi ya kuwatia hatiani watuhumiwa wa vitendo hivyo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika Mkoa wetu wa Iringa tatizo hili limekuwa kubwa sana. Kwa mwaka 2016 tu zimeripotiwa karibu kesi 221 na kesi zilizopo Mahakamani zilizofikishwa ni 37 tu. Kwa kuwa kumekuwa na ukiritimba mkubwa sana wa kushughulikia hizi kesi, sasa kutokana na ukubwa wa tatizo hilo ni kwa nini Serikali isianzishe Mahakama Maalum ya kushughulikia kesi hizi yaani *Sexual Offence Court* kama wenzetu *South Africa*?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu kama ilivyo Mahakama ya Mafisadi, Mahakama ya Ardhi. Kama jambo hili ni gumu ni kwa nini kesi hizi zisipewe kipaumbele kama kesi za watu wenye ualbino? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa, hili tatizo kwa kweli limekuwa likiwaathiri sana watoto wanaobakwa, wazazi, hata sisi viongozi. Na kesi hizi zimekuwa zikichukua muda mrefu sana na kuathiri ushahidi mzima na mbaya zaidi hawa wenzetu wabakaji wamekuwa wakitumia wanasheria wanapopelekwa mahakamani, lakini hawa wenzetu ambao wamekuwa wakipata hizi kesi wamekuwa hawana uwezo, wengi hawana uwezo wa kuwatumia wanasheria.

Ni kwa nini, Serikali isiweke utaratibu wa kuwapatia msaada wa kisheria waathirika wa tatizo hili, badala ya kutegemea *NGO* ambazo nyingi haziko huko vijijini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kabisa kwamba kuna tatizo kubwa siyo tu Iringa, lakini na sehemu zingine za Tanzania. Jana na juzi nilikuwa Mkoani Iringa kujiridhisha mimi mwenyewe kuhusu hali hiyo, nimefika mpaka magerezani.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa takwimu Kitaifa kwa miaka miwili mitatu iliyopita ni kwamba, kila siku ya Mungu kuna matukio 19 ya kubaka na kulawiti hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la matendo haya kwa upande wa Iringa ni kwamba yanatokea katika familia na ndugu, lakini familia hizo tunapopeleka kesi mahakamani ama tunapochunguza wanalindana, hawatoi ushirikiano kwa vyombo vyetu vya upelelezi ndiyo maana kesi nyingi zinachelewa. Hata

tukianzisha mahakama hiyo ya *Sexual Offences Court or whatever,* bado hiyo mahakama itakwama kwa sababu wananchi hawajapata uelewa kwamba, wanavyolindana ndivyo wanazidi kuchochea hayo makosa.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kutoka Mkoa wa Iringa akiwemo Mheshimiwa Msigwa na wengine, naomba tuendeshe kampeni kwa pamoja kuwaomba wananchi wetu, wapiga kura wetu, waachane na mchezo huu wa kulindana katika makosa haya. *Otherwise* Iringa baada ya muda si mrefu tutakuwa na idadi kubwa ya vijana waliokwishaharibika.

Mheshimiwa Spika, suala la kutoa msaada kwa waathirika hilo liko wazi na leo hii akisoma Mheshimiwa Mbunge *Order Paper,* nawasilisha hapa Muswada wa Msaada wa Kisheria. Sheria hiyo, nawahakikishia wananchi utawasaidia sana Watanzania, siyo tu waathirika wa vitendo hivi, lakini vilevile wajane, wanawake wanaonyanyaswa wakati wa mirathi, katika ndoa, katika talaka na kadhalika ili tuweze kukidhi matakwa ya Ibara ya 13 ya Katiba ya usawa kwa kila mtu mbele ya sheria. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote leo tuwepo mpaka jioni ili sheria hiyo tuitendee haki, tuipitishe iwasaidie watu wetu wanaohangaika bila msaada wa kisheria.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utaalii, swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. Ni kwa sababu ya muda Waheshimiwa.

Na. 7

### Mgogoro wa Ardhi Kati ya Wananchi na *WMA* – Mpanda Vijijini

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** Aliuliza:-

Vijiji vya Kabage, Kungwi, Sibwesa, Kasekese na Kaseganyama viko kwenye mgogoro mkubwa wa ardhi na *WMA*.

Je, ni lini Serikali itaingilia kati na kutatua mgogoro huo unaoleta usumbufu mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori za mwaka 2012 zinaelekeza wananchi kuanzisha maeneo hayo katika ardhi ya kijiji kwa ridhaa yao wenyewe, kwa faida yao kiuchumi na kijamii, lakini pia kwa faida za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, eneo linalopendekezwa kuwa *WMA* ya Ubende ilianza na vijiji kumi ambavyo vimeongezeka kufikia vijiji 18. Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda lilitoa baraka za kuanzishwa kwa *WMA* hiyo katika kikao chake cha tarehe 25 Machi, 2005.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanzishwa kwa *WMA* ya Ubende haukuweza kuendelea katika hatua za mbele baada ya kusajiliwa kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya (*CBO)* mwaka 2006 kwa sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa fedha, uvamizi wa maeneo yaliyotengwa, mabadiliko ya maeneo ya kiutawala na kutoelewana kwa baadhi ya makundi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa eneo hili husika kiikolojia na kiuhifadhi kwa ujumla, Wizara yangu itaharakisha kutoa ushauri, msaada wa kitaalam na kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ya Mpanda, Manispaa ya Mpanda na Wilaya ya Nsimbo ili kufikia malengo mapana ya kuanzishwa kwa *WMA* ya Ubende. Aidha, Wizara yangu inaamini kwamba kuanzishwa na kuendeshwa kwa tija kwa Jumuiya ya Uhifadhi ya Ubende kutaleta mafanikio siyo tu ya kiuhifadhi lakini pia ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa vijiji husika na Taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, wakati Jumuiya inaanzishwa maeneo haya yalikuwa na kijiji kimoja tu cha Sibwesa, lakini leo hii kuna vijiji zaidi ya sita na kata mbili zimeanzishwa kwenye maeneo hayo na Serikali inatambua maeneo hayo ya kiutawala. Je, ni lini Serikali kupitia Wizara wataenda ku-*review* mipaka hiyo ambayo ipo inayoleta migogoro ya mara kwa mara kwenye

maeneo hayo ili kuondoa shida inayosababisha wananchi kupigwa mara kwa mara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati Jumuiya inaanzishwa ilikuwa na malengo mazuri ya kiuchumi ambayo kwa sasa hayapo na wananchi hawajanufaika na mradi wowote ule ulioanzisha Jumuiya hiyo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaachia hayo maeneo ili yaendelezwe na vijiji vyenyewe husika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza kimsingi anakubaliana na hoja ya jibu la msingi kwamba tangu wazo la kuanzishwa kwa *WMA* lilipotolewa hadi leo mabadiliko mengi yametokea ikiwemo kuongezeka na kubadilika kwa maeneo ya utawala. Ameuliza swali ni lini Serikali itaenda kushughulikia mabadiliko hayo na kuweza kupima umuhimu wa kuendelea na wazo la *WMA*?

Mheshimiwa Spika, jibu langu ni kwamba mara tu baada ya kukamilika kwa kikao hiki kinachoendelea cha wiki mbili mimi na Mheshimiwa Mbunge tutapanga ratiba vizuri kwa sababu nadhani tukienda pamoja mimi na yeye tutafanya jambo ambalo ni la tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge anasema hapo zamani eneo hili ni kweli lilikuwa linaonekana lina faida za kiuchumi na kijamii lakini kwa maoni yake anasema kwamba hali hiyo imebadilika kwa hivyo hivi sasa anadhani kwamba kuna haja ya Serikali kupitia upya mawazo au maamuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, jibu ni kama lilivyo kwenye majibu ya msingi aya ya mwisho kabisa kwamba sasa Serikali tutakwenda kwanza kutoa ushauri lakini pia kushirikisha wataalam wa eneo hili ili tuweze kwa pamoja sasa kupima hicho ambacho tunasema kwamba zamani kilikuwepo lakini sasa hakipo. Mimi naamini tukienda wote tukakaa pamoja na kukagua maeneo yanayohusika tunaweza tukafikia muafaka. Ahsante sana.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda tuendelee na swali la Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 8

**Mpango wa Serikali Kupunguza Bei ya Maji**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA** aliuliza:-

Serikali kupitia Mawakala wake wa Maji katika Mkoa wa Shinyanga imepandisha bei ya maji kwa takribani asilimia 100 kwa *unit* na *service charge*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ya huduma ya maji ili wananchi waweze kumudu gharama za huduma hiyo na pia kuwavutia zaidi wawekezaji viwandani ili waendelee na uzalishaji?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Injinia Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Shinyanga (*SHUWASA)* imepandisha bei ya maji mwezi Septemba, 2015 kwa matumizi mbalimbali kwenye Manispaa hiyo.

Mamlaka hiyo ilipandisha bei hizo baada ya kupata kibali cha kufanya hivyo toka Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati *(EWURA)*. Bei hizo zimepandishwa kutoka shilingi 790 hadi shilingi 1,000 kwa ujazo wa lita 1,000 kwa matumizi ya majumbani ambayo ni sawa na asilimia 26 na shilingi 1,370 hadi shilingi 2,000 kwa ujazo wa lita 1,000 kwa matumizi ya viwandani ambayo ni sawa na asilimia 46.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuongeza bei za maji ni wa kawaida na ni wa kisheria. Kabla ya kupandisha bei za maji mamlaka husika hulazimika kuomba kibali cha kufanya hivyo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati *(EWURA)* wakionesha sababu za kusudio la kupandisha bei hizo ambazo hujumuisha gharama za uendeshaji pamoja na sehemu ya uwekezaji wa miundombinu. *EWURA* kwa kuzingatia sheria, kanuni na ushirikishaji wa wataalam mbalimbali katika eneo au mji unaohudumiwa na mamlaka hiyo

huendesha uchunguzi na mchakato wa kujiridhisha na uhalisia wa kupandisha bei hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kupunguza bei za maji pale inapogundua gharama za umeme kwa ajili ya uzalishaji wa umeme utatumia gesi ya asili ambayo ina gharama nafuu kuliko ukizalisha kwa kutumia dizeli. Kwa maeneo ya vijijini gharama za uzalishaji zitapungua maeneo mengi kwani Serikali ina mpango wa kubadilisha mifumo ya mitambo ya maji kwa kutumia nishati ya jua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba nimekuona.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaridhishi. Anaongea habari ya gesi asili Shinyanga yaani mpaka gesi asili ije kufika hizi ni ndoto na kwa kweli tutaendelea kuumia na bei ya maji. *EWURA* hawajaenda kufanya *consultation*, hawajaenda kuongea na wananchi, wamepandisha bei ofisini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maji ya Shinyanga na Kahama wametengeneza muungano wakaweka kitu kinaitwa *SHUWASA* na kazi ya *SHUWASA* ilikuwa ni kuboresha usambazaji wa huduma ya maji katika Wilaya hizi mbili. Badala yake *SHUWASA* sasa hivi wanauzia maji Mamlaka ya Kahama na ya Shinyanga ambapo watumiaji wa mwisho wanaumizwa na bei kubwa kwa sababu ya kuwepo na mtu wa katikati. Waziri ana mpango gani wa kujaribu ku-*standardize* suala la bei ya maji katika wilaya hizi mbili kwa sababu hali hii inawaumiza wadau na wawekezaji wanakimbia kwa sababu hakuna huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nikimnukuu Mheshimiwa Rais Magufuli kwenye kampeni zake alisema atahakikisha akiingia madarakani nchi nzima tutapata maji na kama tukikosa maji atawageuza ninyi Mawaziri kuwa maji, lakini mpaka leo hamjawa maji. Shinyanga ni Kata nane tu za Wilaya ya Kahama Mjini ndiyo zina maji wakati Kata 12 zote mpaka leo hazijapata maji, watu wanahangaika wanatumia maji taka na inatishia kuleta milipuko ya magonjwa. Ni lini watatimiza mpango wa kutandaza mtandao wa maji katika Wilaya hizi mbili ili watu waepukane na magonjwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sikujua kama Mheshimiwa Salome Makamba ni mkali hivi. Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Lwenge majibu tafadhali. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge pamoja na jazba aliyokuwa nayo wakati akiongea, kama ifuatavyo:-

**MBUNGE FULANI:** Hatuna maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimfahamishe kwamba masuala ya kupandisha bei yapo kisheria. Huyu mdhibiti ambaye anaitwa *EWURA* ipo *procedure* ambayo lazima aifuate. Kwa hiyo, *procedure* ya kupandisha bei ilifuatwa, hilo ni la kwanza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, pia naomba afahamu kwamba *jurisdiction* ya *SHUWASA* ni katika Mji wa Shinyanga kule Kahama wana mamlaka nyingine ambayo inashughulikia Kahama. Kwa hiyo, tunayo mamlaka ambayo inaleta maji *SHUWASA* kwa *bulk* halafu *SHUWASA* sasa ndo inafanya *distribution.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja kubwa hapa ungesema tu kwamba unaona bei iliyowekwa ni kubwa, hilo ni jambo ambalo tunaweza tukazungumza. Ndiyo maana kwenye majibu tumesema kwamba nusu ya gharama za uendeshaji wa *SHUWASA* ni kulipa bili za umeme. Kwa hiyo, bili za umeme zikishushwa *definitely* na bili ya maji itashuka. Tukasema kwamba uzalishaji wa umeme kwa mfano kama tunatumia nishati ambayo inalazimisha bei ya umeme ishuke basi hata bei ya maji itashuka, ndiyo hoja ambayo ulikuwa umeuliza kwenye swali la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukielezea suala la kwamba mpaka sasa upatikanaji wa maji maeneo mengi hakuna, lakini ni lazima Mheshimiwa Mbunge afahamu tulipitisha bajeti mwaka huu na tumepanga fedha za kutekeleza miradi na kila Wilaya inaendelea kutekeleza. Sasa akilizungumza kwa ujumla inakuwa vigumu kuelewa swali lake tulijibu vipi. Nataka awe *specific* na swali kwamba ni Wilaya ipi na ni mradi upi ambao haujakamilika. Serikali inaendelea kukamilisha miradi kulingana na mpango ambao Wabunge mlipitisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul swali la nyongeza.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitambue Mheshimiwa Masele ndiye aliyeuliza swali kwa Mheshimiwa Rais kuhusu bei za maji. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul swali fupi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TANESCO* wameondoa *service charge* na hawa ndiyo wanatusaidia kusukuma maji katika vyanzo vyetu lakini wenzetu wa Wizara ya Maji kwenye bili zetu za maji bado kuna *service charge*. Je, ni lini hii *service charge* itaondolewa kwa wananchi wetu kwa sababu kwa kweli ni gharama kubwa pamoja na bili hizi ambazo zimepanda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Gekul kuhusu ni lini tutaondoa *service charge* kwenye bili za maji. Mpango huo tumeuanza na kwa sasa Mkoa wa Iringa *meter reading* haisomwi tena na watendaji, *meter reading* hakuna kwa sababu tumeweka mita za LUKU. Ukitaka maji unakwenda kulipia kwa kutumia mfumo uliopo, unapata maji kama jinsi ambavyo unanunua umeme. Kwa kufanya hivyo, sasa hivi Mkoa wa Iringa bado muda kidogo hakutakuwa na *service charge*. Kwa hiyo, tukifanya hivyo nchi nzima *service charges* zitaondolewa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na swali ni la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, kwa niaba yake Mheshimiwa Mama Nagu. Yupo?

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, swali ni la Mary Nagu sio la Mary Machuche.

**SPIKA:** Samahani sana Mheshimiwa Mama Nagu tafadhali.

Na. 9

**Hitaji la Visima Virefu na Mabwawa – Wilaya na Hanang**

**MHE. DKT. MARY M. NAGU** aliuliza:-

Wilaya ya Hanang ni moja ya Wilaya ambazo ziko katika Bonde la Ufa na hivyo upatikanaji wa maji ni wa shida sana. Suluhisho la kudumu ni kuchimba visima virefu na kujenga mabwawa.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga bwawa la maji katika Kijiji cha Gidahababiegh ambalo lilibomoka kutokana na mvua?

(b) Je, ni lini Serikali itarudia kuchimba visima katika Vijiji vya Hirbadamu, Dajameda, Mwanga, Gidika, Lalaji na Wandela ambavyo awali vilipata ufadhili kupitia Mradi wa Benki ya Dunia lakini maji hayakupatikana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Jimbo la Hanang, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bwawa la Gidahababieg ni bwawa kwa ajili ya umwagiliaji na lilibomoka kutokana na athari za mvua za mwaka 2006. Makisio ya gharama ya ujenzi wa bwawa hilo ilikuwa ni shilingi bilioni 1.09 na yaliwasilishwa kwenye Ofisi ya Katibu Mkuu – TAMISEMI tarehe 18/02/2013 kwa ajili ya kuomba fedha za ujenzi wa bwawa hilo. Ukarabati wa bwawa hilo haukuweza kufanyika kwa wakati huo kwa sababu ya kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji itatuma wataalam kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa bwawa hilo katika robo ya tatu ya mwaka 2016/2017. Aidha, katika bajeti ya 2017/2018, Serikali itatenga fedha ili kuanza ujenzi wa Bwawa la Gidahababeigh ili liweze kutoa huduma kwa wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mradi wa Maji Vijijini kupitia Mpango wa Vijiji Kumi kwa kila Halmashauri, Halmashauri ya Hanang ilikamilisha miradi saba na miradi mitatu ya Wandela, Dajameda na Hirbadawa ilikosa

vyanzo vya maji. Vilevile miradi ya Mwanga, Gidika na Lalaji iliyofadhiliwa na wadau wengine ilikosa vyanzo vya maji. Vijiji vyote vilivyokosa vyanzo vya maji vimepewa kipaumbele katika Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili viweze kutafutiwa vyanzo vingine vya maji na hatimaye wananchi waweze kupata huduma ya maji kama ilivyokusudiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Nagu swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali langu.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Bwawa la Gidahababieg siyo la umwagiliaji tu, maeneo yote yale hayana maji ya uhakika kwa hivyo litakuwa ni kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo pamoja na umwagiliaji ikiwezekana. Baada ya bwawa lile kuvunjika kutokana na athari za mvua mwaka 2006, nilifikisha suala hilo kwenye Serikali mwaka 2007 na mpaka leo hakuna lililofanyika. Nataka kujua kama ni kweli mchakato utaanza na bwawa hili lirudi kwa sababu ndiyo linakusanya maji ya mlima Hanang yanayomwagika na kupotea bure?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Vijiji vya Hirbadaw, Dajameda, Mwanga, Gidika, Lalaji na Wandela vyote vilikuwa kwenye Mradi wa Benki ya Dunia na maji hayakuweza kupatikana. Naomba nijue ni lini vijiji hivyo vitaanza kutafutiwa vyanzo vingine ili watu wale waweze kupata maji kwani Bonde la Ufa halina maji? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme kwa bahati nzuri nimetembelea Wilaya ya Hanang na wakati nikiwa kule tulishirikiana na Mheshimiwa Mbunge tukazunguka maeneo yote ambayo yanahitaji huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza ameonesha kwamba Bwawa la Gidahababiegh sio kwa ajili ya umwagiliaji tu na kweli nilikwenda kwenye lile bwawa likishakamilika litatumika kwa umwagiliaji, mifugo na maji yale yakichakatwa yatatumika pia kwa matumizi ya majumbani. Sasa anauliza ni kweli bwawa hili litatengenezwa? Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumetenga fedha katika robo ya pili ya mwaka wa fedha huu

tulionao. Fedha tunazo tayari na wakati wowote wataalam watatumwa kwenda kule kwa ajili ya kufanya *survey. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kwenye hivi vijiji ambavyo havikupata vyanzo vya maji, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulitembea naye na kweli wakati tupo kwenye ziara tuliwaahidi wananchi kwamba haya maeneo ambayo hayakupata vyanzo vya maji kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 ambayo sasa hivi inaandaliwa tutahakikisha tunaweka fedha ili twende kukakamilisha miradi hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado tuko Wizara hiyo hiyo, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 10

**Mto Ruaha Mkuu Kutiririsha Maji Bwawa la Mtera na Kidatu Mwaka Mzima**

**MHE. RISALA S. KABONGO** aliuliza:-

Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mto Ruaha Mkuu unatiririsha maji yake katika Bwawa la Mtera na Kidatu kwa mwaka mzima kama ilivyokuwa miaka iliyopita?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Risala Saidi Kabongo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Ruaha Mkuu ni kati ya mito mikuu minne inayounda Bonde la Rufiji ambayo ni Mto Kilombero, Mto Luwegu, Mto Ruaha Mkuu na Mto Rufiji wenyewe. Maji ya Mto Ruaha Mkuu hutokana na mito inayotiririka kutoka safu za Milima ya Livingstone kule Mbeya. Mito hiyo huingiza maji yake kwenye eneo oevu la Usangu (Ihefu) ambalo likishajaa maji hutoka hapo kama Mto Ruaha Mkuu.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa maji kwenye mto huu kwa kiasi kikubwa unachangiwa na shughuli za kijamii na kiuchumi ambazo zinasababishwa na ongezeko la watu. Shughuli hizo ni pamoja na kupanuka kwa kilimo cha

umwagiliaji ambapo miundombinu yake haijasanifiwa na kuboreshwa. Vilevile uharibifu wa mazingira ikiwemo ukataji miti, kilimo kisichokuwa bora, ongezeko la mifugo na mabadiliko ya tabia nchi vinachangia upungufu huo wa maji.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hii, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Bonde la Rufiji imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa lengo la kuongeza mtiririko wa maji kwenye mto huo. Jitihada hizo ni pamoja na mpango wa ujenzi wa Bwawa la Lugoda katika Mto Ndembela ambapo lengo kuu la mradi ni kuongeza mtiririko wa maji wakati wa kiangazi katika Mto Ruaha Mkuu unaopita katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yakiwemo Mabwawa ya Mtera na Kidatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Risala nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza, kwa kuwa vyanzo vya maji ya Mto Ruaha Mkuu vinatoka nje ya Bonde la Usangu katika Milima ya Chunya, Mbeya, Mufindi, Mpanga na Kitulo, je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kushirikisha wananchi katika kutunza vyanzo vya maji visiendelee kuharibika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Lugola ili kunusuru uhai wa Hifadhi ya Ruaha na Bwawa la Mtera na Kidatu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Risala amesema Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inashirikisha wananchi kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji. Katika muundo wa Wizara ya Maji tunayo Idara maalum ambayo inashughulikia utunzaji wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo tunashirikisha maeneo ya vijiji, tunaunda kamati ndogo ndogo kwenye maeneo husika ili ziweze kulinda vyanzo vile ambavyo vina manufaa na wao wenyewe. Kwa hiyo, tunafanya ushiriki kupitia kwenye Wilaya, Halmashauri, Mikoa pamoja na vijiji ili kushirikisha hao wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sasa ni lini tutajenga hili Bwawa la Lugoda, sasa hivi tumeshakamilisha usanifu. Sasa hivi Serikali inafanya juhudi ya kuwasiliana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupata fedha ili tuweze kujenga hili Bwawa la Ndembera ambalo litatunza maji na kipindi cha kiangazi maji yatafunguliwa kuhakikisha kwamba Ruaha Mkuu inatiririsha maji wakati wote.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa kwa sababu ya muda, mkiangalia muda wetu mtaona umebaki mdogo na maswali ni mengi. Sasa tunakwenda kwenye swali la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Na. 11

**Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki**

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Tulipoanza kutekeleza Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki, kuna bidhaa kutoka Kenya ziliwekwa kwenye kundi 'B' ambazo zilikuwa zinatozwa kodi iliyokuwa ikipungua taratibu hadi ilifikia kiwango cha asilimia sifuri mwaka 2010.

(a) Je, bidhaa hizo ziliongezeka kwa kiasi gani kuingia Tanzania kuanzia mwaka 2005 – 2015?

(b) Je, viwanda vya Tanzania vinavyozalisha bidhaa za kundi 'B' vilikabiliwa na changamoto zipi kutokana na kuondolewa kwa kodi iliyokuwa ikipungua taratibu hadi kufikia asilimia sifuri mwaka 2010?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye vipengele (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Umoja wa Forodha ni kukuza biashara ya bidhaa baina ya nchi wanachama na kuongeza uwekezaji na uzalishaji ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha, nchi wanachama zilikubaliana kuwa na kipindi cha mpito cha miaka mitano kuanzia Januari, 2005 hadi Disemba, 2009 ambapo baadhi ya bidhaa kutoka Kenya kuingia nchi za Uganda na Tanzania ziliendelea kutozwa Ushuru wa Forodha uliokuwa unapungua taratibu na kufikia kiwango cha sifuri Disemba 2009. Bidhaa za Kenya ambazo hazikuondolewa ushuru moja kwa moja wakati wa kuanza kutekeleza Umoja wa Forodha ziliwekwa katika kundi 'B' ambazo ni zile zilizosindikwa kwa kiwango cha kati *(semi finished goods)* na zile zilizokamilika *(finished goods)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye vipengele (a) na (b).

(a) Mheshimiwa Spika, thamani ya bidhaa zilizonunuliwa kutoka Kenya mwaka 2005 ilikuwa ni shilingi bilioni 64.837 ikilinganishwa na hela za Kitanzania shilingi bilioni 174.396 mwaka 2010. Aidha, mwaka 2015, thamani ya bidhaa hizo ilifikia hela za Kitanzania shilingi bilioni 267.881 ambapo manunuzi yaliongezeka kwa wastani wa asilimia 14.9 katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015. Bidhaa ambazo Tanzania imekuwa ikinunua kwa wingi kutoka Kenya ni pamoja na dawa baridi, mafuta ya kula, saruji, sabuni, vipuli vya kuendeshea mitambo, dawa za mifugo, madaftari, bidhaa za plastiki na vifungashio vya bidhaa ambavyo vingi vinatumiwa na wajasiriamali wadogo wadogo na viwanda vidogo vidogo.

(b) Mheshimiwa Spika, viwanda vya Tanzania vilikabiliwa na changamoto ya ongezeko la bidhaa za kundi 'B' kutoka Kenya hali ambayo iliongeza ushindani ukizingatia sekta ya viwanda nchini Kenya ni shindani, kuongezeka kwa vikwazo visivyo vya kiforodha kwa bidhaa kundi tajwa zinapoingia nchini Kenya kama vile vinywaji vikali vinavyozalishwa na viwanda vya Tanzania na utamaduni wa Watanzania kupenda bidhaa za kutoka nje zaidi.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali iliunda Kamati ya Kitaifa ya kudhibiti na kusimamia uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha, kuboresha mazingira ya uendeshaji wa biashara kwa kuwa na miundombinu iliyo mizuri kama ya barabara, bandari, viwanja vya ndege pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika na bei rahisi na kuhamasisha wafanyabiashara kuzalisha bidhaa zenye ubora na viwango vya Kimataifa ili kuleta ushindani katika Soko la Afrika Mashariki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kamala ameridhika, eeh swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu lakini ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kipindi cha mpito kilimalizika mwaka 2010 na kwa kuwa tathmini ya uhakika ilitakiwa ifanyike ili kuweza kujua changamoto zilizotokana na kutekeleza utaratibu wa kodi kupungua taratibu, je, ni lini Tanzania ilifanya tathmini ya uhakika kujua changamoto hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Kanda ya Ziwa, Mwanza, Tanga na Arusha kuna viwanda vingi ambavyo vimelazimika kufungwa kwa sababu ya ushindani wa bidhaa kutoka Kenya; viwanda kama vya mafuta ya kula, maziwa, sabuni na vinginevyo, siwezi kutaja vyote. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inasaidia viwanda hivyo kufufuliwa kwa sababu kufa kwake kumetokana na utekelezaji wa sera ambazo hazikufanyiwa tathmini na kuzirekebisha ili viwanda vyetu visiweze kufungwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ambalo anataka kujua kwamba ni lini tathmini hiyo ilifanywa baada ya kipindi kile cha mpito cha kuanzia 2005 mpaka 2009, niseme tu maelezo niliyotoa yanatokana na tathmini ambayo ilitolewa katika tathmini ya mwaka 2015. Ndiyo maana unakuta katika maelezo yangu nimesema mbinu mbalimbali zimefanyika ili kuweza kuboresha viwanda vyetu na kuhamasisha wafanyabiashara wafanye kazi yao vizuri, kwa hiyo tathmini ilifanyika.

Mheshimiwa Spika, vilevile amezungumzia suala la kuhusu viwanda ambavyo baada ya kuruhusu Ushuru wa Forodha kufutwa katika bidhaa hizo zilizokuwa katika kundi 'B', biashara nyingi au viwanda vingi vya Mikoa kama ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Tanga, Mwanza, Rukwa na hata Arusha viliathirika na najua kabisa na yeye pia anajua kwa sababu katika *thesis* yake aliyoiandikia *Ph.D* ilikuwa juu ya hiyo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Serikali inaendelea kufanya mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba inaboresha mazingira ya ufanyaji wa kazi katika viwanda na kuwajengea *capacity*. Kuna mikutano, semina na

hata kuangalia vigezo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinafufuka.

Mheshimiwa Spika, mara zote hapa Waziri wa Viwanda na Biashara amekuwa akitoa mikakati mbalimbali ambayo Wizara yake inafanya ili kuhakikisha wafanyabiashara hao wenye viwanda waweze kufufua viwanda vyao. Moja ya mikakati ni kuweza kutambua viwanda gani ambavyo vimekufa na nani anavyo au kuna viwanda gani ambavyo vimeathirika na tatizo hilo la mambo ya ushuru ili viweze kuwezeshwa na kuanza kufunguliwa upya.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba katika kipindi hicho cha 2009 mpaka 2010, viwanda vinavyozalisha bidhaa kama za saruji vilikuwa vimekufa, lakini kwa sasa hivi tunaona kwamba sehemu kubwa ya viwanda vinavyofanya vizuri ni pamoja viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa za saruji pamoja na mafuta ya kupikia. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 12

**Mahitaji ya Umeme kwa Wananchi**

**MHE. DANIEL E. MTUKA** aliuliza:-

Watanzania wengi wanahitaji umeme mjini na vijijini lakini wanashindwa kuvuta umeme kutokana na gharama kubwa ambapo *service line* ni shilingi 177,000 na zaidi na gharama ya nguzo ni shilingi 337,740 na zaidi:-

(a) Kwa kuwa nguzo ni mali ya *TANESCO,* je, kwa nini nguzo hizi zisilipiwe na Serikali?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kupunguza *service line costs* kuwa shilingi 27,000 kama ilivyo kwa mradi wa *REA?*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* hugharamia miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo na vifaa vingine ili kupeleka umeme kwa wateja. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti si rahisi kupeleka miundombinu ya umeme maeneo yote kwa wakati mmoja. Kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme wananchi kwa hiari ya kuchangia gharama husogeza miundombinu hiyo katika maeneo ili kuharakisha huduma hiyo. Aidha, kulingana na Kanuni za Sheria ya Umeme ya mwaka 2011, wateja wanaruhusiwa kugharamia miundombinu hiyo kisha kukubaliana na *TANESCO* namna ya kurejeshewa malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo tayari yamefikiwa na huduma ya umeme, wananchi huchangia kwa kulipia vifaa muhimu ikiwemo nguzo, mita pamoja na gharama nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali inagharamia Miradi ya Umeme Vijijini *(REA)* kwa asilimia 100 na kiasi cha shilingi 27,000 wanacholipa wananchi ili kuunganishiwa umeme katika miradi hii ni kwa ajili ya gharama ya *VAT* tu. Lengo ni kuhamasisha na kuwawezesha wananchi wa vijijini ili wapate huduma hiyo kwa gharama nafuu. Baada ya miradi ya *REA* kukamilika, wateja huunganishiwa umeme kwa kufuata taratibu za *TANESCO* ambapo gharama yake ni shilingi 177,000 kwa umbali usiohitaji nguzo.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme kwa wateja wa majumbani maeneo ya mijini ni shilingi 320,960 kwa umbali usiohitaji nguzo ambapo wateja hufungiwa waya na mita. Gharama za maombi ya *services charge* ziliondolewa tangu tarehe 01 Aprili, 2016 lengo likiwa ni kupunguza gharama kwa wateja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtuka swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni ombi, baadhi ya vitongoji ndani ya Mji wangu wa Manyoni havijapata umeme mpaka sasa hivi ninavyozungumza, ukitembea usiku utakuta pale umeme unawaka, pale umeme hauwaki, karibu nusu ya Mji wa Manyoni upo gizani na tatizo kubwa ni gharama za nguzo kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kwa bajeti ya kuanzia mwaka huu imtengee fedha Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya ya Manyoni angalau aweze kununua nguzo na sisi tutaweza kuchangia gharama nyingine ndogo ndogo, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mkandarasi anayetekeleza Mradi wa *REA II* katika Tarafa ya Nkonko yenye vijiji 25 hajakamilisha mradi huu mpaka sasa hivi ambapo ilitakiwa aukamilishe Septemba, 2015. Pamoja na juhudi za Mbunge, Naibu na Waziri kufuatilia zimegonga mwamba, mkandarasi huyu anaonekana ni mzembe na mvivu. Wananchi wa Manyoni wamenituma, wanasema hawataki kumuona hata kwa sura yule mkandarasi, Kampuni ya Spencon.

Je, ni lini Serikali itatuletea mkandarasi mwingine kwa sababu yule hatumtaki tena, hatufai kabisa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mtuka kwa jinsi anavyofuatilia maslahi ya wananchi kwa upande wa umeme. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Mashariki kwamba ni kweli kabisa vile vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme, kulikuwa na shida ya nguzo kwa mkandarasi lakini nimhakikishie kwamba tumeanza kutekeleza Mradi wa *REA III* kuanzia tarehe 6 Januari, 2017. Nitumie nafasi hii kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi kwamba utekelezaji wa *REA III* umeanza tangu tarehe 6 Januari, 2017 na utaendelea kutekelezwa ndani ya miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kutekeleza Mradi wa *REA* katika mikoa sita ikiwemo Mikoa ya Pwani, Tanga, Mara, Iringa, Arusha pamoja na Mbeya. Kadhalika tumeanza kutekeleza mradi huo katika mikoa mingine ambayo ilikuwa kwenye mikoa mama hapo awali ikiwemo Mkoa ya Songwe pamoja na Njombe.

Mheshimiwa Spika, sasa ili nijielekeze kwa swali la Mheshimiwa Mtuka, nimhakikishie vile vijiji 75 ambavyo havijapata umeme kikiwemo Kijiji chake cha Simbangulu, Makutupora, Mwembela na London vitapata umeme. Kwa hiyo, namhakikishie Mheshimiwa Mtuka kwamba vijiji vyake 75 vilivyobaki vitapata umeme bila mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na mkandarasi Spencon, nichukue nafasi hii kusema rasmi kwamba yule mkandarasi amesimama kazi tangu mwezi Novemba. Ni kweli kati ya wakandarasi tuliokuwa nao hakufanya kazi kwa ufanisi na kama Serikali tumeshachukua hatua. Hatua ya kwanza tuliyochukua tumeshikilia mshahara wake wa mwezi Novemba. Hatua ya pili, tumepeleka shtaka rasmi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili tumshtaki mahakamani na hatua ya tatu hatumpi kazi tena kwenye kandarasi zinazofuata. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine tuliyochukua ni kuanza majadiliano na kumpeleka mkandarasi Octopus katika Mkoa wa Singida ili ianze kutekeleza mradi huu mara moja. Kwa hiyo, wananchi wa Singida watapata umeme haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na.13

**Ujenzi wa Viwanda Mahali Zinapopatikana Malighafi**

**MHE. MUSA R. NTIMIZI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga viwanda mahali zinapopatikana malighafi.

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha Tumbaku Mkoani Tabora?

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha Kusindika Asali Mkoani Tabora?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora huzalisha tumbaku nyingi hapa nchini. Kwa mwaka 2015, Mkoa wa Tabora ulizalisha tumbaku tani 39,502. Pamoja na uzalishaji wa tumbaku hiyo, Mkoa wa Tabora hupokea tumbaku inayozalishwa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kigoma. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inalipa kipaumbele suala la ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani tumbaku mkoani Tabora. Serikali imefanya mawasiliano ya awali na wawekezaji nchini Vietnam na China ili kuvutia nchi hizi kuwekeza hapa nchini. Kituo cha Uwekezaji Nchini *(TIC)* kimepewa maelekezo maalum kunadi fursa hii kwa wawekezaji katika sekta ya tumbaku na sigara hapa nchini.

(b)Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora unazalisha asali takribani lita 11,461,500 sawa na tani 11,500 kwa mwaka. Asali hiyo husindikwa na wajasiriamali wadogo kwa njia ya asili bila kutumia mitambo yenye teknolojia ya kisasa. Wajasiriamali hao wanasindika lita 4,126,140 sawa na tani 4,126 ikiwa ni wastani wa asilimia 36 kwa mwaka. Kiasi cha lita 7,335,360 kinabaki bila kusindikwa.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo hayo, Mkoa wa Tabora una fursa kubwa ya uwekezaji wa malighafi hiyo muhimu ambayo pia ina soko la kutosha ndani na nje ya nchi. Kinachotakiwa ni wananchi kutumia fursa hii kuanzisha viwanda vidogo na vya kati hapa nchini. Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zitenge maeneo ya viwanda vidogo na vya kati na kuyajengea miundombinu wezeshi kisha kuchangamkia fursa kwa kufungua viwanda Tabora na maeneo yote inakopatikana asali kwa wingi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani kwa majibu hayo. Mheshimiwa Ntimizi una swali la nyongeza?

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia pamoja na Serikali kutoa maelekezo kwa *TIC* kuhusu kunadi fursa hiyo kwa wawekezaji kuja kujenga kiwanda hiki Mkoani Tabora lakini wawekezaji wa Philip Morris wanaozalisha sigara duniani wanatarajia kuja kujenga kiwanda hiki mkoani Morogoro. Pamoja

na kwamba Serikali kupitia Halmashauri yetu ya Nzega, Tabora Manispaa na Wilaya ya Uyui tulishatoa maeneo kwa ajili ya kiwanda hiki kuja kujengwa Tabora, lakini bado tunasikia Philip Morris wanakuja kujenga kiwanda hiki Mkoani Morogoro.

Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wana Tabora ambao ndiyo watoka jasho wakubwa katika zao hili la tumbaku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali dogo la pili, Serikali imekiri asali bora na nyingi inazalishwa katika Mkoa wa Tabora hususani katika Jimbo la Igalula. Kwa nini Serikali kwa makusudi makubwa kabisa isingesaidia uongezaji wa thamani wa zao hili la asali kwa maana ya kupata utaalamu na *packaging* ili kusaidia kipato cha wana Igalula na nchi kwa ujumla? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ntimizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kampuni ya Philip Morris wamekwishaanza ujenzi wa kiwanda cha kuongeza thamani ya tumbaku pale Morogoro. Wawekezaji wanazo sababu na vigezo wanavyovitumia katika kuchagua maeneo ya mahali gani wawekeze. Kazi ya Serikali mara zote imekuwa ni kuwashawishi na kuwashauri lakini hatufiki mahali tukawalazimisha kama wao wanaamini kwamba sehemu fulani ndipo patakapowapa tija katika uwekezaji wao. Kwa hivyo, Philip Morris pamoja na kushauriwa kwamba wakajenge kiwanda hicho Tabora wao waliamua kuendelea kuwekeza hapo Morogoro. Tukiwalazimisha wanaweza wakaamua kwenda kujenga kiwanda hicho nchi nyingine ambayo pia inazalisha tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuona hilo, Chama Kikuu cha Ushirika cha Tumbaku Mkoa wa Tabora *(WETCU)* katika mkutano wao mkuu waliamua kwamba na wao wawekeze kwenye kiwanda cha kuongeza thamani tumbaku. Mpaka leo wamekwishapata eneo kule Urambo na limepimwa. Sasa hivi wanafanya tathmini ili walipe fidia kwa wananchi walioko pale. Wakishawaondoa wale wananchi walio kwenye eneo hilo, ujenzi wa kiwanda cha kuongeza thamani katika mkoa wa Tabora Wilaya ya Urambo utaanza kufanyika mara moja kupitia Chama hiki cha Msingi cha Ushirika cha *WETCU.*

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Ntimizi lilihusu wananchi kueleweshwa namna bora ya kusindika na kufungasha asali. Hili jambo linaendelea, viko vikundi na kupitia Halmashauri vikundi hivi vimekuwa vinaendelea kupatiwa mafunzo ya namna hii na *SIDO* Mkoa wa Tabora na wao wamekuwa wakijihusisha na hili jambo la kuwafundisha wananchi namna bora ya usindikaji wa asali ili iweze kuwa na ushindani katika soko la ndani na soko la Kimataifa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, maswali haya mawili yaliyobaki yatapangiwa muda wa kujibiwa wakati mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko katika Ukumbi wetu ni pamoja na mgeni aliyeko kwenye *gallery* ya Spika ambaye ni Mheshimiwa John Samwel Malecela, Waziri Mkuu na Makamu wa Rais Mstaafu. Tunakukaribisha sana Mzee Malecela, tunajua leo umekuja kwa sababu mahsusi za kumshuhudia Nyila Mtemi akiapishwa hapa. Hilo jina la Nyila Mtemi wengine hamuwezi kulijua ni la heshima kubwa sana kwa Wagogo. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao wamekuja kutembelea Bunge na kujifunza. Tunaomba tuchukue fursa hii kuwakaribisheni wageni wote mliokuja siku ya leo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria anawaomba Wajumbe wake kukutana leo saa 7.00 mchana katika kikao cha Kamati katika Jengo la *Utawala Annex* kule *dispensary*.

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada ya *CCT* anawaomba wahusika mkutane saa 7.00 mchana Wanamaombi wote kwa ajili ya Ibada maalum katika Jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili. Mheshimiwa Anna Lupembe anaomba wale waumini wa *CCT* mkutane ghorofa ya pili.

Baada ya maelezo hayo kwa vile muda wetu ni mdogo, naomba tuendelee na shughuli. Naomba sasa nichukue fursa hii kumkaribisha Mheshimiwa Naibu Spika aweze kuendelea na shughuli zilizopo. *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mwongozo.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama Mheshimiwa Spika alivyosema tutaendelea na shughuli zilizopo mbele yetu, Mheshimiwa Julius.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kuhusu Kanuni ya 47 ambapo inasema:-

*"Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma."*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana na juzi kwenye vyombo vya habari, tulipata taarifa ya uamuzi wa Waziri wa Maliasili kuagiza wananchi wa Loliondo zaidi ya 54,000 katika vijiji 14 kuacha kuendesha shughuli zote wanazoziendesha katika maeneo yao hasa ufugaji na kuondoka. Wiki hii hii ametangaza kwamba kuanzia sasa mifugo yote itakayokamatwa katika maeneo ya Hifadhi itaifishwe bila *fine* wakati Waziri hana mamlaka hiyo kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi yetu lakini alitamka. *(Makofi/Kicheko)*

Katika jambo hili ambalo linaleta taharuki kubwa sana katika Taifa letu na kuendeleza migogoro kati ya wakulima na wafugaji na wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza kwamba katika mgogoro wa Loliondo iundwe Kamati ya kulishughulikia jambo hilo na Kamati hiyo imeundwa. Mwezi Mei, 2016, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliagiza kutokuwasumbua wafugaji mpaka pale Serikali itakapotenga maeneo mahsusi kwa ajili ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa nini jambo hili Bunge lisiielekeze Serikali namna ambavyo itali-*handle* suala la wafugaji kuliko kuhatarisha maisha ya wananchi zaidi ya 54,000 wanaotakiwa kusitisha shughuli zao kuanzia sasa kwa agizo tu la Waziri ambaye ana chuki na wafugaji na asiyejali maslahi ya wafugaji katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja hiyo ili jambo hili liweze kujadiliwa na Bunge liweze kutoa maelekezo kwa Serikali. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama kuunga mkono hoja ya Mhe. Julius K. Laizer)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo wako. Utakumbuka tarehe 12 Oktoba, 2016 nilisimama kuomba Bunge liahirishwe kwa Kanuni ya 47 ili tujadili jambo halisi na la dharura wakati huo ambapo ndugu zetu kule Kagera walikuwa wamepata matatizo ya tetemeko na nyumba zao zikabomoka, hali ikawa mbaya, wote tunajua. Lile jambo likajadiliwa hapa na jana nimepokea simu nyingi sana kutoka Kagera kwamba mvua imenyesha kubwa sana na watu wanalala nje, kuna mlipuko wa magonjwa utatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakumbuka Wabunge wote 390 tulichanga fedha ili ziende kwa wahanga na zikatatue matatizo ya wahanga, lakini Rais alipokuwa kule Kagera amesema hizo pesa haziendi kwa wahanga, zinakwenda kufanya shughuli za Serikali. Kwa hiyo, naomba utoe mwongozo hizo pesa zirejee Bungeni tupelekee wahanga moja kwa moja kuliko kwenda kufanya shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Julius Kalanga mwanzo wakati amesimama alisema anaomba mwongozo, lakini baadaye badala ya kutumia Kanuni hiyo inayohusu mwongozo akaenda kwenye Kanuni ya 47. Kama alivyotusomea nadhani hakuna haja ya kurudia kusoma lakini Kanuni ya 47 inahusu kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo ya Mheshimiwa Julius Kalanga, amelieleza Bunge hili kwamba jana kwenye vyombo vya habari amepata taarifa kama alivyoeleza kwa kirefu kwamba kuna vijiji kadhaa ambavyo vitaathiriwa na maelekezo ama maagizo aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Pia ameeleza kwamba katika hiyo taarifa kuna habari za kutaifisha mali za wanavijiji huko Loliondo na ameturejesha kwenye maagizo ambayo Mheshimiwa Julius Kalanga anasema yamewahi kutolewa na Mheshimiwa Makamu wa Rais kwamba wafugaji wasibughudhiwe mpaka Serikali itakapokuwa imeweka utaratibu mzuri wa kuweza kuhakikisha hawapati taabu na mali zao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matumizi ya Kanuni ya 47 yako pamoja na Kanuni ya 48. Kwa hiyo, Kanuni ya 47 inabidi isomwe na Kanuni ya 48 kwa sababu Kanuni ya 48 ndiyo inayotoa masharti kuhusu jambo lipi litakuwa ni la dharura na lipi si jambo la dharura.

Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 48 namshauri Mheshimiwa Julius Kalanga atumie Kanuni nyingine ili tupate muda Bunge hili kuliongelea jambo hili.

Namshauri atumie Kanuni ambayo itamfanya yeye alete hoja hapa kwa ajili ya mjadala, lakini si kwa ajili ya kusitisha shughuli tulizonazo leo. Kwa sababu hilo jambo kama alivyotupa taarifa ndefu yeye mwenyewe si jambo la dharura isipokuwa Bunge lina uwezo wa kulijadili kwa kutumia kanuni nyingine atakapoleta hoja mahsusi.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mwongozo alioomba Mheshimiwa Heche, ametupeleka mwaka jana katika Bunge la mwezi Oktoba kwamba alisimama hapa baada ya nchi yetu kupata tatizo la tetemeko katika Mkoa wa Kagera. Kasema aliomba jambo lile lijadiliwe kama dharura kwa sababu wananchi walikuwa wanapata taabu na anasema amepata pia taarifa jana kwamba mvua zimenyesha nyingi na wananchi wanalala nje na kuna uwezekano wa kutokea mlipuko wa magonjwa, lakini hata kama si mlipuko wa magonjwa watu tu kulala nje hilo ni tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa taarifa hii Mheshimiwa Heche ndiye ambaye ametupa sasa hivi, sisi wote hatuna namna ya kulijua jambo hilo kwa undani kwa sasa.

Kwa hivyo, kwa kuwa yeye ameomba mwongozo hasa ukizingatia kwamba Bunge kwa maana ya Wabunge walichanga fedha zao kwenda kusaidia kwenye lile tetemeko Bukoba, kwa mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 68 nitatoa mwongozo kuhusu jambo hili hapo baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Ni wewe ndiyo uliyesema utaratibu?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtolea unajua ukisema utaratibu wakati niliyetoka kuongea ni mimi nadhani unaijua Kanuni inayohusu utaratibu maana yake ni kwamba nimefanya kinyume na Kanuni. Ukitumia Kanuni ya Kuhusu Utaratibu maana yake nimefanya kinyume na Kanuni ndiyo zinavyosema hizi Kanuni zetu. Kwa hiyo, naomba uzisome vizuri utumie Kanuni nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu atoe hoja ya kutengua Kanuni za Bunge.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe mbele ya Kiti chako maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Sita wa Bunge unaoanza leo tarehe 31 Januari, 2017 ambao umepangwa kumalizika tarehe 10 Februari, 2017. Katika Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, Bunge linatarajia kujadili na kupitisha Miswada mitatu ya Sheria ya Serikali pamoja na kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za mwaka za Kamati 14 za Kudumu za Bunge.

KWA KUWA Kamati ya Uongozi katika kikao chake kilichofanyika siku ya Jumatatu tarehe 30 Januari, 2017, iliona kwamba siku zilizopo ni chache na taratibu zikiendelea kama kawaida upo uwezekano wa shughuli zilizopangwa kutofanyika kwa ufanisi na hivyo iliazimia kuliomba Bunge likubali kutengua baadhi ya Kanuni zake ili upatikane muda zaidi wa shughuli zilizopangwa.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 21(2) na (4), vikao vya Bunge huanza saa 3.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana na kurejea saa 11.00 jioni hadi saa 1.45 usiku; na kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15), Bunge haliwezi kukutana siku za Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko; na kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) kifungu cha (a), Mbunge anayechangia hoja atachangia kwa muda wa dakika zisizozidi 15.

HIVYO BASI, Bunge linaazima kwamba katika Mkutano huu wa Sita, Kanuni za 28 na 62 zitenguliwe kwa mujibu wa Kauni ya 28(3) na 153(1) ili kubadili muda wa vikao vya Bunge, muda wa Mbunge kuchangia hoja Bungeni na siku za vikao vya Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, namba moja, Kanuni ya 28(4) na (5) zitenguliwe ili Bunge likisitishwa saa 7.00 mchana lirejee tena saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 jioni. Vile vile Kanuni ya 28(15) itenguliwe ili Bunge likutane siku ya Jumamosi tarehe 4 Februari, 2017 kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana, isipokuwa kwamba katika kikao cha siku hiyo ya Jumamosi hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kanuni ya 62(1)(a) itenguliwe ili kila Mbunge achangie hoja kwa muda wa dakika zisizozidi 10 badala ya dakika 15. Utaratibu huu mpya uanze kutumika Ijumaa tarehe 3 Februari, 2017, Bunge litakapoanza shughuli za kupokea na kujadili taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge na uendelee hadi kukamilika kwa Mkutano wa Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:** Kauli za Mawaziri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunazo Kauli za Mawaziri, tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Hali ya Chakula Nchini

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 Kanuni 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu hali ya Chakula na Lishe kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka katika Bunge lako la Kumi, Serikali ilitoa kauli kuhusu upatikanaji wa mahitaji ya chakula baada ya kukamilisha tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2015/2016 na upatikanaji wa chakula mwaka 2016/2017. Katika Kauli hiyo ya Serikali, Bunge

lako lilielezwa kuwa tathmini ilionesha kuwa Kitaifa, uzalishaji wa chakula utafikia tani 16,172,841 za chakula na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2016/2017 ni wastani wa tani milioni 13,159,326 na hivyo nchi itakuwa na ziada ya chakula tani milioni 4,013,515.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya ziada hiyo, tani milioni 1,101,341 ni za mazao ya nafaka na tani 1,912,174 ni za mazao yasiyo ya nafaka. Nchi ilikuwa na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 123. Aidha, pamoja na hali nzuri ya chakula kitaifa, kulikuwa na Halmashauri 43 ambazo zilikuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Januari mwaka huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya usalama wa chakula na lishe, imekamilisha tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe nchini zikiwemo Halmashauri 43 zilizoainishwa mwanzo kuwa na upungufu wa chakula. Tathmini hii ilishirikisha Shirika la Umoja na Mataifa la Kilimo na Chakula *(FAO)* na Mpango wa Chakula Duniani *(World Food Program – WFP).*

Aidha, wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)* na Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* na Wizara ya Afya, kupitia taasisi yake ya chakula na lishe, *TFNC* walishiriki. Tathmini hii imebainisha kuwa kuna Halmashauri 55 zenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la tathmini lilikuwa ni kuainisha mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula na masuala yanayohusiana na lishe katika msimu wa 2015/2016 na athari zake katika mfumo ya maisha ya wananchi katika maeneo husika kwa kipindi cha Januari, 2017 na matarajio katika kipindi cha Mei, 2017 kabla ya mavuno ya msimu wa 2016/2017. Matokeo ya tathmini ya kina yameiwezesha Serikali kuchukua maamuzi stahii katika utekelezaji wa jukumu la hali endelevu ya usalama wa chakula na lishe nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hii ilizingatia Mihimili Minne ya usalama wa chakula ambayo ni upatikanaji wa chakula *(food availability),* ufikiwaji wa chakula *(food accessibility)* utumiaji wa chakula *(food utilization)* na uthabiti wa chakula *(food stability).*

Aidha, ilitumia mfumo wa uainishaji wa madaraja mbalimbali ya usalama wa chakula na lishe, *Integrated Food Security Phase Classification (IPC)* unaotumika Kimataifa katika kuainisha watu na hali mbalimbali za makundi, *phases* kiusalama wa chakula na lishe na aina ya hatua stahiki za kukabiliana nazo. Mfumo huu umewezesha kuchanganua vigezo mbalimbali na kutoa

taswira ya hali halisi ilivyo kuanzia Julai, 2016 hadi Julai, 2017 na hali inayotarajiwa katika kipindi kijacho kuanzia mwezi Februari hadi mwezi Mei mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya hali ya upatikanaji wa mvua kutoka mikoa inayopata mvua za vuli, zinaonesha kwa ujumla mvua zimechelewa kuanza na zimenyesha katika kiwango cha wastani na chini ya wastani, zikiwa na mtawanyiko usioridhisha. Mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita, Mara, Pwani, Tanga, Morogoro pamoja na sehemu ya Mkoa wa Shinyanga na Simiyu, mvua zilipoanza kunyesha zilikuwa chini ya wastani. Ukosefu wa mvua za vuli uliipata pia Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Mazao yanayopandwa katika baadhi ya maeneo hayo yameathirika kutokana na ukame uliojitokeza ukiwamo Mkoa wa Kagera katika Wilaya za Kyerwa, Misenyi na Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha mvua za msimu kilichoanza mwezi Novemba mwaka 2016 kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua *(unimodal);* Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Lindi na Mtwara, zinatarajiwa kuendelea hadi mwezi Aprili, Mwaka huu 2017. Kwa ujumla mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi, isipokuwa maeneo ya Kaskazini mwa Mkoa wa Lindi yanatarajiwa kupata mvua chini ya wastani katika kipindi cha mwezi Januari hadi Februari, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na inaendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mazao ya chakula hususan mahindi, mchele na maharage ili kujiridhisha uwepo na upatikanaji wake sokoni. Bei ya wastani ya mahindi katika msimu wa chakula na soko kwa mwaka 2016/2017 imekuwa na mwelekeo wa kupanda kuanzia mwanzo wa mwezi Julai, 2016. Bei hii iko juu ukilinganisha na bei katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Hadi tarehe 23 Januari 2017 bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 imepanda na kufikia wastani wa Kitaifa; naomba hapa nirudie, "wastani wa Kitaifa" wa shilingi 92,057 ukilinganishwa na mwezi Januari, 2016 ambapo gunia la kilo 100 liliuzwa kwa wastani wa shilingi 67,048. Kwa upande wa mchele, bei zina mwelekeo mzuri bado kwa ulinganisho wa mwaka jana na bado hazijabadilika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanda na kushuka kwa bei katika kipindi kama hiki ni jambo lililotegemewa, kwani mwanzo mwa msimu hakuna mazao yanayoingia sokoni na hivyo hupelekea bei kupanda. Aidha, mwanzo wa mavuno, bei hushuka kutokana na mazao mengi kuingia sokoni. Hali ya mwenendo usioridhisha wa unyeshaji wa mvua za vuli na za msimu kwa kipindi cha 2016/2017 kwa ajili ya upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2017/2018 katika

maeneo mengi ya nchi, imechangia wafanyabiashara wa nafaka nchini na hasa zao la mahindi kuingiza zao hili kidogo kidogo sokoni, hivyo kuongeza kasi ya uhitaji kutoka kwa wananchi na kusababisha bei kuzidi kupanda.

Aidha, uwepo wa mahitaji makubwa na bei nzuri ya mahindi katika nchi jirani zinazotuzunguka ambazo zilikuwa na upungufu wa chakula, umesababisha bei ya mahindi kuzidi kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe imekamilishwa. Matokeo ya tathmini hii yamebainisha kuwa hali ya upatikanaji wa chakula bado ni ya kuridhisha pamoja na kuwa maeneo yenye upungufu wa chakula hapa nchini yapo.

Mheshimiaw Naibu Spika, tathmini imebainisha kuwa jumla ya tani 35,491 za chakula zinahitajika ili kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula na lishe kati ya mwezi Februari na mwezi Aprili mwaka huu kwa watu 1,186,028 walioainishwa kuwa wana upungufu wa chakula katika Halmashauri 55 tulizozitaja.

Aidha, jumla ya watu 1,018,603 wasio na uwezo wa kupata chakula *(destitute population)* watahitaji tani 3,549 za chakula cha bei nafuu haraka. Serikali imekwishaanza kuchukua hatua kukabiliana na hali hiyo ikiwemo ya kuuza chakula kwa bei nafuu katika maeneo yaliyobainishwa kuwa na upungufu mkubwa ili kushusha bei iliyopo na hatimaye kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuchelewa kwa mvua na mtawanyiko usioridhisha katika maeneo mengi hapa nchini, athari zifuatazo zinatarajiwa kutokea.

(1) Matarajio ya malengo ya uzalishaji wa mazao ya chakula huenda yasifikiwe.

(2) Uzalishaji wa mbegu za mazao ya kilimo utapungua.

(3) Uwezekano wa kuongezeka kwa bei za baadhi ya chakula, upo.

(4) Kupungua kwa mapato yatokanayo na ushuru wa mazao kwa baadhi ya Halmashauri.

(5) Uwezekano wa kuwa na maeneo mengi yenye upungufu wa chakula na hivyo kuongezeka kwa kiwango cha utapiamlo.

(6) Kuongezeka kwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kutokana na uhaba wa malisho na maji.

(7) Uwezekano wa kupungua kwa mapato yatokanayo na mazao ya kilimo yanayouzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na athari za ukame kama nilivyozieleza hapo juu, tathmini imebainisha kuwa Halmashauri za Wilaya hizi 55 zinahitaji jumla ya tani 1,969 za mbegu bora za mahindi, mtama na mizizi inayokamaa kwa muda mfupi na kustahimili ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu hizo zinahitajika ziwafikie mwezi Februari mwaka huu ili ziweze kupandwa katika msimu wa 2016/2017 katika maeneo yanayoendelea kupata mvua wakati huu wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa inachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa hali ya chakula na lishe ni imara na hatua hizi ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(1) Kusimamia usambazi wa mbegu za mazao ya kilimo zinazostahimili ukame na zinazozaa kwa muda mfupi ambazo ni pamoja na mtama, uwele na mbegu za mazao aina ya mizizi na mihogo na viazi vitamu ili kuzitumia vizuri mvua zinazonyesha kwa sasa. Wizara ilikutana na wazalishaji wa mbegu za mazao ya kilimo Jijini Arusha mwaka 2016 mwezi Oktoba ili kubaini mahitaji ya mbegu ikiwa ni pamoja na usambazaji wa mbegu hizio ili ziweze kuwafikia wakulima kwa wakati.

(2) Kuhamasisha wakulima kupanda mazao aina ya mizizi, mtama na uwele kwa maeneo yanayopata mvua za masika ambazo zinaendelea kunyesha na mawakala wa pembejeo pamoja na vituo vya utafiti vilivyopo katika kanda mbalimbali hapa nchini.

(3) Serikali kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula *(NRFA)*, itaendelea kuhifadhi kwa uangalifu chakula kilichopo ili kitumike pale kitakapohitajika.

(4) Kuhamasisha sekta binafsi kununua mazao ya chakula katika maeneo yaliyo na ziada na kuyauza katika maeneo yenye uhaba wa chakula. Aidha, wafanyabiashara waliohifadhi mahindi; narudia. “Aidha

wafanyabiashara waliohifadhi mahindi" wanaomba kusambaza chakula hicho katika masoko ya ndani ya nchi, jambo ambalo litasaidia kupunguza mfumuko wa bei.

(5) Kuhimiza usindikaji wa mazao ya chakula kwa kuyaongezea thamani na kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kula vyakula vya aina zote.

(6) Kutokana na hali ya mwenendo wa unyeshaji wa mvua za vuli na msimu kutoridhisha katika meneo mengi ya nchi, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanaelekezwa kuendelea kuhamasisha na kusimamia wakulima kutumia mbegu zinazokomaa mapema na kupanda mazao yanayostahimili ukame.

(7) Kuwashauri wananchi kutumia kwa uangalifu, kutunza na kuhifadhi akiba ya chakula kwa matumizi ya kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusisitiza kuwa Serikali itaendelea kufuatilia hali ya chakula na lishe nchini kwa kushirikiana na wadau wetu ili kuhakikisha kuwa hali ya chakula na lishe ni imara wakati wote. Aidha, wakulima waendelee kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha kwa kupanda mazao yanayostahimili ukame na kukomaa kwa muda mfupi na pia waendelee kutunza na kutumia chakula walichonacho kwa uangalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango.

**HALI YA UCHUMI WA TAIFA**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge namba 49(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Kauli ya Serikali kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa, hususan mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi, ikiwemo ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, mwenendo wa sekta ya nje na akiba ya fedha za kigeni,

mwenendo wa Sekta ya Fedha ikiwa ni pamoja na hali ya ukwasi, lakini pia deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa kauli hii ili kukitaarifu chombo hiki muhimu cha wawakilishi wa wananchi kuhusu afya ya uchumi wa Taifa letu ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwafikishia wananchi ujumbe na maelezo sahihi badala ya uvumi wa mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ukuaji wa pato la Taifa. Ukuaji wa uchumi ni mojawapo ya viashiria vinavyotazamwa katika kutathmini afya uchumi wa Taifa. Takwimu za ukuaji wa pato la Taifa, zinaonesha kuwa uchumi wa Taifa umeendelea kukua na Tanzania ni miongoni mwa nchi za Bara la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo uchumi wake unakuwa kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mifano tu, Kenya ukuaji wa uchumi mwaka 2015 ilikuwa asilimia 5.6 na inatarajiwa kwa mwaka 2016 uchumi wa Kenya utakua kwa 6%. Kwa upande wa Rwanda mwaka 2015 uchumi wao ulikua kwa 6.9% na mwaka 2016 utakua kwa 6%. Kadhalika Uganda, 2015 uchumi wao ulikua kwa 4.8% na mwaka 2016 4.9%. Kwa upande wa Zambia, 2015 uchumi wao ulikua kwa 3% na mwaka 2016 inakadiriwa utakua kwa hiyo hiyo 3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara mwaka 2015 ilikuwa 3.4% na mwaka 2016 ni asilimia 1.4%. Kwa Upnde wa nchi yetu, mwaka 2015 uchumi wa Taifa letu ulikua kwa 7% na inakadiriwa kwamba mwaka 2016 uchumi wetu utakua kwa wastani wa 7.2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Januari hadi Setemba, 2016, ukuaji wa pato la Taifa uliongezeka kufikia 6.5% ikilinganishwa na 6.3% katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Sekta ambazo zimekua kwa viwango vikubwa ni pamoja na shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe, 15.8%; usafirishaji na uhifadhi wa mizigo 15.5%; habari na mawasiliano, 13.4%; na huduma za fedha, 11.5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ya sasa ni kufikia ukuaji wa wastani wa 7%. Hii inatokana na kuwa, sekta ambazo zinaajiri watu wengi na ambazo zina mchango mkubwa katika uchumi hazikukua kwa kasi ambayo ilitarajiwa ikiwemo Sekta ya Kilimo, ambapo katika hiyo miezi, ilikua kwa wastani wa 2.1% tu wakati matarajio yalikuwa ni 22.6%; na biashara ilikuwa kwa wastani wa 5.6% ikilinganishwa na matarajio ya 7.6%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mfumuko wa bei, ambacho ni kiashiria kingine cha afya ya uchumi wa Taifa letu, mfumuko wa bei ulipungua kutoka 6.5% Januari, 2016 hadi 5.5% Juni, 2016 na kupungua zaidi hadi 4.5% Septemba, 2016 na baadaye umepanda kidogo mwezi Desemba kufikia 5%. Kwa ujumla Mwenendo huu wa kushuka kwa mfumuko wa bei ulichangiwa na kasi ndogo ya kuongezeka kwa bei ya chakula nchini, kushuka kwa wastani wa bei ya mafuta ya petroli katika Soko la Dunia lakini pia utekelezaji wa sera za bajeti na fedha lakini pia utulivu wa shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mfumuko wa bei, pana uwezekano wa kuongezeka kutokana na hali ya ukame inayojitokeza hapa Tanzania, lakini pia katika baadhi ya nchi za ukanda wa nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiashiria kingine cha afya ya uchumi ni uimara wa thamani ya shilingi. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani ilipungua kwa kasi ndogo kutoka wastani wa shilingi 2,144.7 kwa dola moja mwezi Desemba, 2015 hadi shilingi 2,170 kwa dola moja mwezi Desemba, 2016. Hata hivyo thamani ya shilingi kwa dola ya Kimarekani ilishuka kufuatia kuimarika kwa dola ya Kimarekani na hii pia iliathiri sarafu nyingine siyo ya Tanzania peke yake, ikiwemo hata *Yuan* ya China ambayo ilishuka thamani kwa 3.55% kwa kipindi cha miezi 12 kufikia tarehe 19 Januari, 2017.

Kadhalika faranga ya Rwanda nayo iliteremka kwa 8.55% lakini hata pauni ya Kiingereza nayo iliteremka kwa 13.04.%. Dola ya Kimarekani iliimarika kutokana na kupanda kwa kitu kinaitwa *Federal Reserve Fund Rate* mwezi Desemba, 2016 ambayo iliwafanya wawekezaji kuongeza mahitaji yao ya dola ya Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa upande wa sekta ya nje na akiba ya fedha za kigeni, mwaka 2016 nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa huduma na uhamishaji mali nchi za nje *(current account deficit)* ilipungua kufikia dola za Kimarekani milioni 2,054.8 kutoka nakisi ya dola za Kimarekani milioni 4,011.6 mwaka 2015 na kupungua huko kulitokana zaidi na kuongezeka kwa thamani ya madini, bidhaa asili, mapato yatokanayo na utalii na kupungua kwa thamani ya bidhaa ambazo tunaagiza nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Desemba, 2016 akiba ya fedha za kigeni imefikia dola za Kimarekani 4325.6 ambazo zinatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi 4.2, na hivyo akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze mwenendo wa sekta ya kibenki. Tathmini ya hali ya mabenki yetu na taasisi ya fedha inaonesha kuwa mabenki yetu yako imara na salama, yana mitaji na ukwasi wa kutosha. Kiwango cha mitaji ikilinganishwa na mali iliyowekezwa kwa Kiingereza tunasema; *total capital to total risk weighted assets and of balance sheet exposures* kilikuwa 17.8% kikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria ambacho ni 10%. Ukwasi ni kiasi cha fedha kilichopo katika uchumi na kwa kawaida inajumlisha fedha taslim na amana katika mabenki, zilizopo Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoshelevu wa ukwasi katika uchumi unapimwa kwa kuangalia viashiria mbalimbali, ikiwemo ujazi wa fedha, mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi, kiwango cha mitaji ya mabenki, uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kwa fedha taslim na amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi na upatikanaji wa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo imedhihirika kwamba kuna upungufu wa ukwasi katika uchumi, Serikali kupitia Benki Kuu huwa inachukua hatua mbalimbali za kisera ili kuchochea shughuli za kiuchumi; na hatua hizi ni pamoja na kuongeza ujazi wa fedha na kuboresha mazingira kwa sekta binafsi kukopa. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaweza kupunguza kodi na kuongeza matumizi ya Serikali baada ya kupata ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo sasa, ukiangalia kigezo cha uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslim na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi, kwa Kiingereza, *liquid assets to demand liabilities,* uwiano huu ulikuwa 42.4% ikilinganishwa na 37.2% katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Kiwango kinachohitajika cha chini kisheria ni 20%. Pia amana za wateja katika mabenki zilipungua kidogo kutoka shilingi trilioni 20.73 mwezi Desemba, 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 20.57 mwezi Septemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, amana za Serikali kwenye mabenki ya biashara ni 3% tu ya amana zote za mabenki. Aidha, jumla ya rasilimali za mabenki zimeendelea kuongezeka kutoka shilingi bilioni 26,917.2 mwezi Desemba, 2015 hadi kufikia shilingi bilioni 27,978.2 mwezi Desemba, 2016, sawa na ongezeko la asilimia 2.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mikopo kwa sekta binafsi, mikopo iliongezeka kwa 7.2% katika kipindi cha mwaka ulioishia Desemba, 2016 ikilinganishwa na ongezeko la 24.8% katika kipindi hicho mwaka 2015. Kupungua kwa kiwango cha ukuaji kilitokana na tahadhari zilizochukuliwa na mabenki

kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu kutoka 6.4% Desemba, 2015 hadi 9.5% Desemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa kasi ya kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi, katika miezi ya hivi karibuni siyo kwa Tanzania peke yake, tumeangalia nchi nyingine kama Kenya, nako tunaona ilipungua kutoka 19.7% kati ya Julai na Oktoba, 2015 hadi 4.1% katika kipindi hicho mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini Uganda mikopo kwa sekta binafsi nayo ilipungua kwa 25.2% mwezi Septemba, 2015 hadi -1% Septemba, 2016. Pia mwenendo usioridhisha unajitokeza katika mikopo chechefu *(nonperformaning loans),* katika nchi hizo za jirani na kusababisha baadhi ya mabenki kuwekwa chini ya uangalizi kama vile *Crane Bank* ya kule Uganda. Hali hii tunaona ni mbaya zaidi katika nchi ambazo zinauza mafuta kama Naigeria na Ghana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wasiofikiwa na mabenki umeendelea kuongezeka kutokana na ubunifu na mipango ya utoaji huduma za malipo ya rejareja kupitia simu za kiganjani na huduma za uwakala wa mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo benki zilizopata msukosuko katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha, *CRDB* na *TIB Development Bank* zilipata hasara na hasara ilisababishwa na tengo kwa ajili ya mikopo chechefu, yaani *provision for nonperforming loans.* Twiga Bancorp iliwekwa chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania, lakini licha ya hali hiyo, benki nyingi zikiwemo *CRDB* yenyewe na *TIB Development Bank* zimebaki kuwa na mitaji na ukwasi wa kutosha kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vizuri kukumbuka kwamba jumla ya benki ina taasisi za fedha nchini ziko 66 na zina matawi 783 na hivyo kwa benki tatu kupata msukosuko katika robo moja tu ya mwaka siyo sababu ya kuzua taharuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo juu ya utoaji wa fedha kwa mamlaka za Serikali za Mitaa, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2016. Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka fedha katika Halmashauri zetu maana huko ndiko utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi unapofanyika. Katika robo ya kwanza ya 2016/2017 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 114.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo.

Aidha, katika robo ya pili ya mwaka Serikali iliongeza mgao wa fedha ziliozoenda kwenye Halmashauri ambapo kiasi cha shilingi bilioni 203.4 zilipelekwa. Serikali itaendelea kupeleka fedha katika Halmashauri kwa kipindi kilichobaki kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri ili kuwahudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ulipaji wa madai mbalimbali, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 kiasi cha shilingi bilioni 3,113.7 ziliwasilishwa ikiwa ni madai ya wakandarasi, watumishi, wazabuni na watoa huduma. Baada ya Serikali kufanya uhakiki kupitia kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali, ilibainika kuwa madeni halali yalikuwa ni shilingi bilioni 2,934.2 na madai yaliyokosa vielelezo na hivyo kukosa uhalali yalikuwa shilingi bilioni 179.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha nusu mwaka 2016/2017 Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 600.2 na kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 42.35 zilikuwa ni kwa ajili ya madai ya watumishi, shilingi bilioni 49.46 kwa ajili ya wazabuni, shilingi bilioni 11.2 kwa ajili ya watoa huduma, shilingi bilioni 30 kwa ajili ya madai ya vyombo vya ulinzi na usalama na shilingi bilioni 467.2 ni kwa ajili ya wakandarasi mbalimbali ikijumuisha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya makandarasi wa maghala na skimu za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni ya pembejeo, Serikali bado inaendelea na uhakiki wa madeni hayo ili kubaini madeni halali na yasiyo halali. Hata hivyo, katika kipindi cha Julai mpaka Desemba, 2016 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo. Aidha, katika kuhakikisha madai ya wakandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma wa ndani yanapewa kipaumbele, Serikali imeweka mkakati wa kutenga fedha kila mwezi ambapo mwezi Januari, 2017 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 70 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa deni la Taifa; deni la Taifa linajumuisha mikopo ambayo hukopwa na Serikali kutoka nje na ndani ya nchi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na kujaza nakisi ya bajeti. Deni la nje hukopa kutoka kwenye taasisi za kifedha kama Benki ya Dunia, nchi wahisani na pia kutoka kwenye benki za biashara, wakati deni la ndani linapatikana kwa kuuza dhamana za Serikali *(treasury bills)* na hati fungani *(treasury bonds)*. Mikopo kutoka Benki Kuu ya Tanzania na benki za biashara za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Desemba, 2016 deni la Taifa ikijumuisha deni la ndani na la nje, lilifikia dola za Kimarekani milioni 19,021.9. Hiyo ndiyo *dead stock* ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 18,459.3 mwezi Juni, 2016 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.05, na ongezeko la deni hilo limetokana na mikopo iliyopo na mikopo mipya iliyopokelewa na Serikali na ambayo bado haijaiva, kutoka mikopo ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ambayo iligharamiwa na mikopo hiyo imeelezewa kwa kina katika kitabu cha uchambuzi wa deni la Taifa pamoja na miradi iliyofadhiliwa na deni hilo toka uhuru.Tumeandaa kitabu ambacho Waheshimiwa Wabunge watagawiwa ambacho kinatoa taarifa ya uchambuzi wa deni la Taifa na miradi yote iliyofadhiliwa na deni hilo tangu uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa deni la Taifa hauangalii ukubwa wa deni lililopo *(debt stock)* bali kadri deni linavyoiva *(debt maturity)*. Hali hiyo sasa, sehemu kubwa ya deni la Taifa inaiva kwa kipindi cha muda mrefu *(long term maturity)* na kutokana na hali hiyo wastani *(average time to maturity)* kwa deni lililopo sasa litaiva kwa kipindi cha miaka takribani 12. Hali hii inaashiria kwamba athari zake kwenye bajeti ziko chini *(low re-finance risk)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikilipa madeni ya nje na ndani kwa mujibu wa mikataba. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Desemba, 2016 Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 2,570.1 kulipa madeni ya ndani na nje yaliyoiva; na kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi bilioni 1,822.3 na deni la nje ni shilingi bilioni 747.8. Malipo ya deni la ndani yanajumuisha malipo ya mtaji *(roll over)* ya shilingi bilioni 1,367.1 na malipo ya riba shilingi milioni 455.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuendelea kulipa kwa wakati mikopo yote ya nje inayoiva kwa mujibu wa sheria, maana tusipolipa kuna athari kubwa za kutolipa. Baadhi ya athari hizo ni kwamba, nchi itahatarisha mahusiano yaliyopo kati yake na nchi wahisani; taasisi za fedha za Kimataifa na mabenki ya nje; nchi inaweza kushitakiwa kwenye Mahakama za Kimataifa na kuisababishia hasara na kutopata mikopo; kukamatwa kwa mali zake zilizopo nje na ndani ili kulipia madeni ambayo hayajalipwa; na kulipa gharama za ziada kama adhabu *(Penalty)* kulingana na makubaliano na hivyo kuongeza mzigo wa deni kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ifahamike kwamba malipo yote ya mikopo ya ndani na nje yanakasimiwa kwenye Fungu Na. 22 na kwa kuzingatia utaratibu wa kibajeti, matumizi yote yaliyokasimiwa katika fungu hili ni matumizi

yasiyoepukika *(first charge)*. Kutokana na utaratibu huo wa kibajeti na athari nilizozieleza hapo awali, kutolipa mikopo kulingana na mikataba, malipo yote ya mikopo ya ndani na nje hulipwa kwa wakati pindi yanapoiva.

Aidha, kwa upande wa madai ya ndani ya wakandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma, malipo yake hukasimiwa kwenye mafungu mengine ya Wizara, Mikoa na Halmashauri ambayo hayapo katika kundi la matumizi yasiyoepukika na hivyo, madai haya hulipwa baada ya uhakiki kukamilika. Sambamba na ulipaji wa Deni la Taifa, Serikali imeendelea kugharamia utoaji wa huduma nyingine mbalimbali kwa jamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme juu ya tathmini ya uhimilivu wa Deni la Taifa. Kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134, Serikali ina wajibu wa kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni *(Debt Sustainability Analysis)* kila mwaka ili kupima hali ya deni na uhimilivu wake. Kwa kuzingatia matakwa ya sheria, nilivyosema, Wataalamu wamekamilisha tathmini ya uhimilivu wa Deni la Taifa kwa mwaka 2016/2017 na matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa deni ni himilivu kwa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Matokeo haya yanafanana na yale yaliyotolewa katika Taarifa ya *IMF* ya Uhimilivu wa Deni la Taifa iliyotolewa Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hiyo tathmini ya Novemba, 2016 viashiria vinaonesha kuwa, thamani ya sasa ya jumla ya Deni la Taifa *(Present Value of Total Public Debt)* kwa pato la Taifa ni 34.2% ikilinganishwa na ukomo wa 56%. Thamani ya sasa ya Deni la Nje pekee *(Net Present Value of External Debt)* kwa Pato la Taifa ni 19.9% ikilinganishwa na ukomo wa 40%. Thamani ya sasa ya Deni la Nje kwa Mauzo ya Nje ni 97.7% ikilinganishwa na ukomo wa 150% na thamani ya sasa ya Deni la Nje kwa Mapato ya Ndani ni 145.3% ikilinganishwa na ukomo wa 250%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia vigezo hivyo, uwiano wa deni lote la ndani na nje kwa thamani ya sasa kwa pato la Taifa *(Present Value of Total Public Debt to GDP)* kwa mwaka 2015/2016 Kenya lilikuwa 45.6%, Tanzania 34.2%, Uganda 24.1%, Rwanda 22.7%. Pia uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa Pato la Taifa Kenya ilikuwa 19.4%, Tanzania 19.9%, Uganda 10.7%, Rwanda 17.3% ambavyo vyote viko chini ya ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba Deni la Taifa linadhibitiwa na linaendelea kuwa himilivu. Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa Deni la Taifa,

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaendelea kufanya ukaguzi maalum na yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha taarifa ambayo itatoa hali halisi ya Deni la Taifa.Kama tulivyoona katika viashiria mbalimbali vya kiuchumi, uchumi wa Tanzania uko imara na tulivu; mfumuko wa bei umedhibitiwa katika wigo wa tarakimu moja, benki zetu bado zina ukwasi wa kutosha kuweza kukopesha wananchi na deni la Taifa linaendelea kuwa himilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa huru ya *IMF* ambayo imetolewa tarehe 9 Januri, 2017 inathibitisha ukweli huu kwa kusema, na ninanukuu: *"Tanzanian's microeconomic performance remains strong, economic growth was robust during the first half of 2016 and is projected to remain at about 7% this fiscal year. Inflation came down below the authority's target of 5% and is expected to remain close to that target while the external current account deficit was revised downward on account of lower imports of capital goods."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko changamoto kadhaa ambazo Serikali inaendelea kuzifanyia kazi na ambazo ziko ndani ya uwezo wa Serikali. Ninawasihi Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwa pamoja katika masuala yote ya maendeleo ya nchi yetu na tutumie taarifa rasmi katika kuwafikishia wananchi ujumbe ulio sahihi. Aidha, kama nilivyoeleza awali, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba uchumi wetu ni tulivu, uko imara na tunategemea utaendelea kuwa hivyo katika kipindi cha muda wa kati. Nirudie kuwahakikishia kuwa hakuna mdororo wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa Kauli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2016 *(The Legal Aid Bill, 2016)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema, kukutana tena hapa siku ya leo tunapoendelea kujadili masuala muhimu ya Kitaifa kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Vilevile naushukuru uongozi wa Bunge kwa kunipa fursa kuwasilisha Muswada huu leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Wahesnimiwa, Alhaji Abdallah Bulembo, Anne Kilango Malecela na Profesa Palamagamba Kabudi kwa kula Kiapo cha Uaminifu leo Bungeni kufuatia uteuzi wao kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanywa na Rais wa Nchi. Nampongeza vilevile Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Balozi. Pia, nampongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma aliyechaguliwa kwa kishindo kuwa Mbunge wa Dimani, kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Makamu wake Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum. Kamati hii imeutendea haki Muswada huu kwani imeuchambua na kuujadili kwa kina kwa lengo la kuuboresha, ili hatimaye tupate sheria bora itakayowasaidia wananchi, hususan wa kipato cha chini na wa vijijini kuifikia haki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuihakikishia Kamati na Bunge lako Tukufu kuwa, kwa asilimia kubwa tumezingatia maoni, michango na ushauri tulioupata ambao umesaidia sana kuimarisha maudhui ya Muswada huu kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali. Vilevile naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watumishi wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa walioipa Wizara yangu katika maandalizi na uandishi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wadau mbalimbali kutoka taasisi na asasi za kiraia zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria nchini, kama vile Chama cha Wanasheria cha Tanganyika *(TLS),* Chama cha Wanasheria Wanawake *(TAWLA),* Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake *(WILAC),* Mfuko wa Huduma za Kisheria *(LSF),* Taasisi ya Watu wenye Ulemavu ya Msaada wa Kisheria na Maendeleo ya Jamii *(DOLASED),* Kamati ya Msaada wa Kisheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(LAC),* Mtandao wa Wasaidizi wa Kisheria *(TAPANET),* Sekretariet ya Msaada wa Kisheria *(LAS),* Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)* na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi na asasi hizi zimeshirikiana kwa kiasi kikubwa na Serikali, hususan Wizara yangu, katika kufikia maelewano na nia moja ya kuhakikisha tunapata sheria muafaka ya msaada wa kisheria ili kukata kiu ya muda mrefu ya hitaji la sheria hii. Kwa kifupi Muswada huu umetokana na ushirikishwaji mpana sana wa wadau wengi na ninasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa Sheria ya Msaada wa Kisheria, umepitia hatua nyingi sana na umechukua muda mrefu hadi kufikia hatua hii ya kujadiliwa na Bunge lako Tukufu. Ni zaidi ya miaka kumi kumekuwa na hitaji la kuwa na sheria hii. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri wenzangu walionitangulia katika Wizara hii kwa msingi mzuri walioujenga ambao nimeutumia kumalizia kazi hii ambayo inakwenda kumaliza kwa kiasi kikubwa kilio cha muda mrefu cha wananchi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili katika kuifikia haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa lengo la kuanzisha kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu mfumo wa kisheria wa kusimamia, kuratibu, kurasimisha na kutambua utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika mashauri yote ya jinai na mashauri ya madai kwa wahitaji. Utaratibu tuliokuwanao kwa miaka mingi kama Serikali, unahusu baadhi tu ya makosa ya jinai, makosa yenye adhabu kubwa kama vile ya kunyongwa hadi kufa na vifungo virefu. Huduma hiyo imekuwa ikitolewa katika ngazi ya Mahakama Kuu pekee na kwa wigo mdogo tu pale inapohitajika kwa maslahi ya haki na kwa maelekezo ya Jaji Mkuu au yeyote yule aliyekasimiwa mamlaka ya kutoa maelekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mashauri ya madai, huduma ya msaada wa kisheria imekuwa ikitolewa na asasi za kiraia na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali tu, kuanzia ushauri wa kisheria, kuandaa nyaraka za kimahakama na hata uwakilishi Mahakamani. Hata hivyo, kazi hii imekuwa

ikifanywa pasipokuwa na uratibu na usimamizi wa utoaji wa huduma hiyo baina ya taasisi, asasi hizo za Serikali, jambo linalosababisha watu wasiokuwa na taaluma ya sheria, makanjanja, vishoka, kuivamia fani na kuharibu sifa nzuri ya taaluma ya sheria inayojengeka miongoni mwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kupitia Muswada huu mfumo wa uratibu katika utoaji huduma hii unaanzishwa na dhana ya utoaji msaada wa kisheria inapanuka kuhusisha utoaji wa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya sheria na haki, kushauri, kuandaa nyaraka za Mahakama, kusuluhisha migogoro na uwakilishi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo miaka ya hivi karibuni, ongezeko kubwa la mahitaji ya huduma ya msaada wa kisheria, ongezeko la idadi ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria. Kutokana na hali hii, Serikali imeona ulazima wa kuanzisha mfumo huu wa kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma hii ili kuhakikisha inatolewa na watu wenye sifa, inatolewa kwa wahitaji halisi na kwa taratibu zinazofahamika na Serikali kuwa na uwezo wa kuona na kutathmini huduma inayotolewa, ili iendane na matakwa ya Kikatiba, hususan Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosisitiza usawa mbele ya sheria bila ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matakwa haya ya Kikatiba, endapo Bunge lako litaipitisha sheria hii siyo tu kwamba nchi yetu itatambuliwa Kimataifa, kutekeleza masuala ya haki za binadamu, bali vilevile tutakuwa tukitekeleza kwa vitendo mikataba na maazimio mbalimbali ya Kimataifa kuhusu umuhimu wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Umma wa mwaka 1986, Azimio la Lilongwe la Msaada wa Kisheria la Mwaka 2004, Tamko la Lilongwe kuhusu Uwezeshaji Wananachi Kuifikia Huduma ya Msaada wa Kisheria katika Mfumo wa Haki Jinai wa mwaka 2004 na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Kanuni na Miongozo ya Umoja wa Mataifa ya Namna ya Kuifikia Haki katika Mfumo wa Haki Jinai wa mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, Muswada huu unalenga kukidhi matakwa ya Katiba yetu na ya mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambayo tumeridhia sisi wenyewe. Kwa Muswada huu tunaweka mfumo madhubuti na endelevu wa msaada wa kisheria ambao utaziba ombwe lililopo la usimamizi na udhibiti na kutoa kwa kiasi kikubwa suluhisho la changamoto ya muda mrefu ya Watanzania wengi kutojua sheria hivyo haki, fursa na wajibu

wao kisheria. Mfumo unaowekwa na sheria inayopendekezwa unakusudia kuhakikisha kuwa huduma ya msaada wa kisheria nchini inaleta matokeo chanya kwa ustawi wa wananchi, hususan wa vijijini na wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili wa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, Muswada huu pia, umelenga kuwatambua Wasaidizi wa Kisheria. Unafuta sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai, Sura ya 21 na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu nane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada ina Ibara ya kuanzia ya 1, 2 na 3 ambazo zinahusu masharti ya awali ambayo ni Jina la Sheria inayopendekezwa; eneo la kutumika kwa sheria husika katika Jamhuri ya Muungano; na mwanzo wa kutumika na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada unaopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ambayo ina Ibara ya 4, 5, 6, 7 na 8 inaweka masharti kuhusu usimamizi na uratibu wa watoa msaada wa kisheria. Aidha, sehemu hii inaanzisha Bodi ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria na kuainisha majukumu ya Bodi hiyo. Vilevile sehemu hii inaunda nafasi ya Msajili wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria, uteuzi wake na majukumu yake. Inaweka pia nafasi za Wasajili Wasaidizi katika ngazi za Mkoa na Wilaya na taratibu pamoja na masharti ya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu yenye Ibara kuanzia ya 9 hadi 18 inahusu masharti ya usajili wa Watoa Msaada wa Kisheria. Ni katika sehemu hii ambapo zimeainishwa sifa mtu kusajiliwa kama Mtoa Msaada wa Kisheria. Utoaji wa cheti cha usajili mara baada ya kusajiliwa kama mtoa msaada wa kisheria, mazingira yatakayosababisha kusitishwa au kufutwa kwa cheti cha usajili na haki ya rufaa dhidi ya uamuzi wa kusitishwa au kufutwa kwa cheti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ambayo ina Ibara za 19 na 20 inahusu masharti mahususi kwa wasaidizi wa kisheria, sifa, majukumu na masharti ya wasaidizi wa kisheria, kutoa ushauri kwa mujibu wa masharti ya Muswada unaopendekezwa. Sifa zilizoainishwa kwa msaidizi wa kisheria zitasaidia wananchi wengi sana kufikiwa na huduma hii kutokana na sifa hizo kuwa ni za ngazi ya chini kabisa kielimu.

Hata hivyo, kila Msaidizi wa Sheria atapitia mafunzo maalum ya sheria kwa mtaala ambao ulishaandaliwa na Chama cha Wanasheria cha Tanganyika. Tayari Wasaidizi wa Sheria zaidi ya 4,700 wamepatiwa mafunzo hayo. Sehemu hii ya Muswada inatoa katazo kwa Wasaidizi wa Kisheria kutoza ada kwa mtu anayesaidiwa na kuwakataza kujihusisha na shughuli zilizotengwa kwa ajili ya Mawakili wa Kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ina Ibara kuanzia ya 21 hadi 36. Sehemu hii inaweka masharti ya mtu anayeweza kuomba msaada wa kisheria, masharti ya jumla ya msaada wa kisheria na msaada wa kisheria katika mashauri ya madai na jinai kwa amri ya Mahakama na Mabaraza mbalimbali yanayojihusisha na utoaji haki. Aidha, sehemu hii inatoa masharti ya upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watoto na watu walio katika Vituo vya Polisi, Magereza na vizuizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita ya Muswada ina Ibara za 37, 38 na 40. Sehemu hii inahusu masuala ya fedha na inajumuisha masharti yahusuyo vyanzo vya mapato bodi, makadirio ya mwaka na vitabu vya hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba iliyo na Ibara kuanzia 41 hadi 45 inahusu masharti mengineyo. Aidha, inatoa masharti kuhusu mamlaka ya Msajili kutoa tangazo kwa mtoa msaada wa kisheria kuthibitisha uwepo wake, wajibu kuhusiana na miiko ya maadili ya kitaaluma kwa watoa msaada wa kisheria na mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kwa lengo la utekelezaji bora wa sheria na kanuni za maadili ya watoa msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane ambayo ina Ibara ya 46 hadi Ibara ya 50 inatoa masharti yatokanayo na masharti ya mpito. Aidha, sehemu hii inafuta sheria ya msaada wa kisheria katika mashauri ya jinai sura ya 21 pamoja na kuainisha masharti ya mpito na yatokanayo kuhusu shughuli zote za huduma ya msaada wa kisheria zilizokuwa zinaendelea kabla ya kupitishwa kwa sheria ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Huduma a Msaada wa Kisheria na kuupitisha kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS – TAMISEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu mpaka tutakapofika wakati wa kulihoji Bunge.

**ISSN 0856 - 35X**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 14*** ***26th August, 2016***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.36 Vol.97 dated 26th August, 2016*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE LEGAL AID ACT, 2016

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement.
2. Application.
3. Interpretation.

PART II
ADMINISTRATION AND COORDINATION OF LEGAL AID PROVIDERS

4. Establishment of the Board.
5. Functions of the Board.
6. The Registrar of legal aid.
7. Functions of the Registrar.

8. Appointment of Assistant Registrars.

PART III
REGISTRATION OF LEGAL AID PROVIDERS

9. Register of legal aid providers.
10. Qualifications for registration as a legal aid provider.
11. Application for registration.
12. Determination of applications.
13. Refusal of registration.
14. Appeals.
15. Certificate of registration.
16. Suspension and cancellation of certificates.
17. Procedure for suspension or cancellation.
18. Supervision of legal aid providers.

PART IV
SPECIAL PROVISIONS ON PARALEGALS

19. Qualifications for paralegals.
20. Legal aid services by paralegals.

PART V
PROVISION OF LEGAL AID

*(a) General provisions*

21. Application for legal aid.
22. Person who may apply for legal aid.
23. General principles of legal aid.
24. Legal aid to be provided by institutions.
25. Unauthorised payments.
26. Records, monitoring and evaluation

*(b) Legal aid in civil proceedings*

27. Legal aid in civil proceedings by order of the court.
28. Notification of other parties.
29. Recovery of costs.
30. Execution of judgments.
31. Costs against aided person.

32. Aided person not required to provide security for costs.

*(c) Legal aid in criminal matters*

33. Legal aid by order of the court.
34. Expenses incurred by advocates.
35. Legal aid for children in police stations or prisons.
36. Legal aid for persons in custody.

PART VI
FINANCIAL PROVISIONS

37. Sources of fund of the Board.
38. Annual estimates.
39. Annual performance report.
40. Books of accounts.

PART VII
MISCELLANEOUS PROVISIONS

41. Registrar may require proof of existence.
42. Obligations relating to professional conduct.
43. Prohibition from political activities.
44. Misuse of funds for legal aid.
45. General offences.
46. Publication of legal aid providers.
47. Powers of the Minister to make regulations.
48. Repeal and saving
49. Transitional arrangement.

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
7th August, 2016

**JOHN W.H.KIJAZI**
*Secretary to the Cabinet*

A Bill

*for*

**An Act to regulate and coordinate the provision of legal aid services to indigent persons, to recognise paralegals, to repeal the Legal Aid (Criminal Proceedings) Act and to provide for other related matters.**

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title and commencement

**1.** This Act may be cited as the Legal Aid Act, 2016 and shall come into operation on such date as the Minister may, by notice published in the *Gazette*, appoint.

Application

**2.** This Act shall apply to Mainland Tanzania.

Interpretation

**3.** In this Act, unless the context otherwise requires:

"advocate" means a practicing advocate;

"aided person" means a person who has been granted legal aid under this Act;

"Assistant Registrar" means Assistant Registrar referred to under section 8;

"Board" means the Board established under section 4;

Cap. 237

"Chief Court Administrator" means the Chief Court Administrator appointed under the Judiciary Administration Act;

"indigent person" means a person whose means are insufficient to enable him to engage a private legal practitioner and includes other categories of persons where the interests of justice so require;

"legal advice and assistance" means an advice or assistance provided to the indigent person on criminal and civil cases based on the relevant law, legal process, procedures and drafting of documents as may be required;

"legal aid" or "legal aid service" includes the provision of legal advice, assistance or representation to indigent persons;

"legal aid provider" means an institution that has been registered under this Act to provide legal aid;

"Minister" means the Minister responsible for legal affairs;

"paralegal" means a person who provides legal aid services under the legal aid provider;

"Permanent Secretary" means a Permanent Secretary of the Ministry responsible for legal affairs; and

"Registrar" means the Registrar referred to under section 6;

"Register" means a Register of Legal Aid providers established under this Act.

## PART II
## ADMINISTRATION AND COORDINATION OF LEGAL AID PROVIDERS

Establishment of the Board

**4.**-(1) There shall is established a Board to be known as the National Legal Aid Advisory Board.

(2) The provisions of the Schedule to this Act shall have effect as to the composition of the Board, tenure of office, proceedings at meetings of the Board and other matters relating to the Board.

(3) Save for the composition of the Board, the Minister shall have power to amend, alter or vary the

Schedule.

Functions of the Board

**5.**-(1) The functions of the Board shall be to-

(a) provide policy guidelines to legal aid providers;

(b) advise the Minister on policy and other matters of relevance with respect to improving legal aid provision;

(c) approve the annual reports of legal aid providers;

(d) determine appeals from the decision of the Registrar;

(e) perform such other functions as may be directed by the Minister.

(2) In performing its functions under this Act, the Board shall maintain as far as practicable, a system of consultation and cooperation with Ministries, Government institutions, legal aid providers or any other public or private bodies established under any written law.

The Registrar of legal aid

**6.**-(1) There shall be the Registrar of legal aid providers.

(2) The Director responsible for legal aid matters in the Ministry responsible for legal affairs shall be the Registrar.

Functions of the Registrar

**7.**-(1) The functions and duties of the Registrar shall be to-

(a) register legal aid providers;

(b) investigate complaints of malpractice, negligence, misconduct or disobedience against legal aid providers;

(c) suspend or cancel registration of any legal aid provider;

(d) keep and maintain the Register of legal aid providers;

(e) inspect any legal aid provider's office with a view to satisfying himself on the type and quality of legal aid services offered;

(f) take appropriate measures for promoting

legal literacy and legal awareness among the public and, in particular, educate vulnerable sections of the society about their rights and duties under the Constitution and other laws;

(g) coordinate and facilitate formulation and accreditation of curriculum for training of paralegals;

(h) coordinate, monitor and evaluate the functions of legal aid providers and give general and specific directions for the proper implementation of legal aid programmes;

(i) keep records and reports regarding legal aid providers;

(j) prepare various reports on legal aid services and other matters for submission before the Board;

(k) facilitate information sharing in accessible format and providing guidelines for networking between legal aid providers and the Government; and

(l) determine disputes between legal aid providers other than advocates, and between legal aid providers and aided persons;

(m) perform any other functions as may be directed by the Minister or the Board as the case may be.

(2) The Registrar shall be the Secretary to the Board.

(3) The Registrar shall in the performance and discharge of his functions and duties under this Act-

(a) be assisted by such number of officers of the Ministry responsible for legal affairs as may be determined; and

(b) be answerable to the Permanent Secretary who shall be the link between the Government and legal aid providers.

Appointment of Assistant Registrars

**8**.-(1) The Permanent Secretary shall, for the purpose of facilitating registration of legal aid providers at the regional and district levels and after consultation with relevant authority, designate for each region or each district, a public officer from amongst public officers within the region or district to be the Assistant Registrar.

(2) Save for section 11(5), the Assistant Registrar appointed under subsection (1) shall, on behalf of the Registrar, register legal aid provider within the region or district for which he is appointed and issue certificates of registration.

(3) The Assistant Registrar appointed under this section shall, in the performance of his functions under this Act, be answerable to the Registrar.

## PART III
## REGISTRATION OF LEGAL AID PROVIDERS

Register of legal aid providers

**9**.-(1) There shall be a Register of legal aid providers which shall contain the names of institutions providing legal aid, the services provided and such other particulars or matters as may be prescribed.

(2) The Registrar shall cause the Register, whether in printed or electronic form, to be available to members of the public at police stations, courts, prisons and such other public places as may be determined by the Minister.

Qualifications for registration as a legal aid provider

**10.**-(1) An institution shall not be registered as a legal aid provider unless it has the following qualifications-

(a) it has been registered under the relevant laws;
(b) the provision of legal aid services is one of its core functions;
(c) it has office premises and office facilities;
(d) it has not less than-
   (i) two advocates;

(ii) one advocate and two paralegals; or
(iii) three paralegals; and
(e) it has been cleared by the body that has registered it as to its records pertaining to management of finances.

(2) Subject to the provisions of subsection (1), an institution with no advocate shall be required to furnish proof of affiliation with another legal aid provider which has an advocate before being registered.

(3) Without prejudice to the generality of subsection (1), the provisions of paragraphs (a) and (b) shall not apply to institutions established by an Act of Parliament or any academic institution accredited under any written law.

Application for registration

**11.**-(1) Subject to the provisions of section 10, an institution applying for registration under this Act shall apply in the manner prescribed in the regulations.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), an application for registration shall be accompanied by-
(a) a copy of the constitution of the institution or any other document establishing the institution;
(b) personal particulars of office bearers, advocates or paralegals;
(c) particulars relating to address and physical location of the head office of the institution;
(d) a copy of a certificate of clearance from a legal provider's registering authority;
(e) an application fee prescribed in the regulations; and
(f) any other particulars or information as may be required by the Registrar.

(3) Where an institution intends to operate as a legal aid provider in more than one district or in the whole region, an application for its registration shall be submitted to the Assistant Registrar designated for that region.

(4) Where an institution intends to operate as a legal aid provider within a certain district, an

application for its registration shall be submitted to the Assistant Registrar for that district.

(5) Where an institution intends to operate as a legal aid provider in more than one region or it has been registered out of the country, an application for its registration shall be submitted to the Registrar.

(6) Where the Assistant Registrar has registered a legal aid provider, he shall make a report to that effect and submit that report to the Registrar.

(7) The Minister shall, by regulations, prescribe the procedures for registration and operations of legal aid providers at regional and district levels in terms of this Act.

Determination of applications

**12**.-(1) The Registrar or as the case may be Assistant Registrar, shall consider and make determination of an application for registration within thirty days after receiving the application.

(2) Pursuant to the provisions of subsection (1), in determining the application, the Registrar or as the case may be Assistant Registrar, may register or refuse to register an institution as a legal aid provider.

Refusal of registration

**13**.-(1) The Registrar or Assistant Registrar may refuse to register an institution as a legal aid provider if he is satisfied that-

(a) it has not met the conditions prescribed under section 10; or

(b) it has given false or fraudulent information in any material particular.

(2) Where the Registrar or Assistant Registrar has refused to register an institution as a legal aid provider, he shall, within twenty one days from the date of such decision, notify the applicant of the reasons for such refusal.

Appeals

**14**.-(1) An institution which is not satisfied with the decision under section 13 may, within twenty one days:

(a) in the case of decision of Assistant Registrar, appeal to the Registrar; and

(b) in the case of decision of the Registrar, appeal to the Board.

(2) The institution which is aggrieved by the decision of the Board may, within thirty days from the date of receiving such decision, appeal to the Minister.

(3) The Minister shall, within thirty days from the date of receiving the appeal consider and determine the appeal.

Certificate of registration

**15**.-(1) The Registrar, or Assistant Registrar shall, after registration of an institution as a legal aid provider and upon payment prescribed fee issue a certificate of registration in the form prescribed in the regulations.

(2) The certificate of registration shall contain-

(a) the name and address of the legal aid provider;

(b) the area of operation of the legal aid provider;

(c) legal status of the institution; and

(d) such terms and conditions in respect of which a certificate is issued.

(3) A certificate of registration issued under subsection (1) shall be a conclusive evidence for the institution to operate as a legal aid provider under this Act.

Suspension and cancellation of certificates

**16**.-(1) Subject to the provisions of section 17, the Registrar may issue a written warning, suspend or cancel a certificate of registration of the legal aid provider.

(2) The Registrar may suspend a certificate of registration of a legal aid provider, if he is satisfied that-

(a) the legal aid provider has committed a professional misconduct or has failed to admonish its employee for professional misconduct or breach of the code of conduct prescribed by the relevant professional body;

(b) the legal aid provider is in breach of the code of conduct prescribed under this Act or under any other written law this;
(c) the legal aid provider operates in variance to its constitution;
(d) the legal aid provider has failed to keep proper records of activities undertaken on behalf of an aided person and the Registrar considers that this shall have an adverse effect on the interests of the aided person generally or in any particular case.

(3) The Registrar may cancel a certificate of registration of a legal aid provider if he is satisfied that-
(a) the registration was obtained by mistake, fraud, undue influence or misrepresentation;
(b) the legal aid provider has failed to comply with the conditions of the registration;
(c) the qualifications for registration has ceased to exist in respect of the legal aid provider;
(d) the office bearer of the legal aid provider has been declared bankrupt, is insolvent or has entered into an arrangement with his creditors;
(e) an advocate or paralegal employed by a legal aid provider has regularly breached professional conduct;
(f) a legal aid provider has engaged in any political activities;
(g) the office bearer of the legal aid provider is convicted of an offence which touches on his integrity, accountability, or is subject to an order made under the relevant body; or
(h) the legal aid provider is not providing, or has not provided, the service for which he is registered to the prescribed standard.

(4) Where the Registrar suspends or cancels certificate of registration, he shall-
(a) notify the relevant legal aid provider of the decision and order such legal aid provider to stop operations; or

(b) as the case may be, remove the name of the legal aid provider from the register.

Procedure for suspension or cancellation

**17.**-(1) Where a legal aid provider is in default of the terms and conditions in respect of which a certificate was issued or is in violation of section **16**, the Registrar may serve to the legal aid provider a default notice in writing specifying the nature of the default.

(2) Upon receipt of the default notice, a legal aid provider shall make representation in writing to the Registrar regarding remedy or rectification of the default.

(3) Where a legal aid provider has failed to remedy or rectify the default within time specified in the default notice or has not made a representation satisfactory to the Registrar, the Registrar shall suspend or cancel a certificate.

(4) A legal aid provider whose certificate has been suspended or cancelled may apply to the Registrar for review of the decision to suspend or cancel the certificate if he is dissatisfied by the reasons for such suspension or cancellation.

(5) A legal aid provider who is aggrieved by the decision of the Registrar to suspend or cancel a certificate may appeal to the Board in accordance with the provisions of section 14.

Supervision of legal aid providers

**18.**-(1) The Assistant Registrar shall, for purposes of this Act, be a supervisor of legal aid providers in the respective region or district.

(2) In the discharge of supervisory duties, the Assistant Registrar shall-

(a) exercise general supervision in accordance with the provisions of this Act;

(b) investigate complaints of malpractice, negligence, misconduct or disobedience and make a report to the Registrar of the facts and circumstances of any such complaints; and

(c) submit to the Registrar, on annual basis,

names of legal aid providers who have ceased to practice.

## PART IV
## SPECIAL PROVISIONS ON PARALEGALS

Qualifications for paralegals

**19**.-(1) A paralegal shall be required to possess any of the following:

(a) a bachelor degree in laws from an accredited institution;

(b) a bachelor of arts in law enforcement from an accredited institution;

(c) a diploma in law or paralegal studies from an accredited institution;

(d) a certificate in law from an accredited institution; or

(2) In addition to the requirement under subsection (1), a paralegal shall undergo necessary training for paralegals.

Legal aid services by paralegals

**20**.-(1) A paralegal may provide legal aid services in accordance with the provisions of this Act.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), a paralegal shall have the following duties:

(a) carrying out educational programmes in national or local languages on legal issues and procedures of concern to the community;

(b) assisting aided person in the procedures to obtain necessary legal documents;

(c) providing advice and assistance in social welfare matters;

(d) guiding an aided person to a proper forum or to access justice;

(e) advising the conflicting parties to seek amicable settlement or referring them to dispute settlement institutions; or

(f) reporting on matters related to breach of peace, violation of law and human rights to

relevant institutions.

(3) A person who intends to provide legal aid services as a paralegal under this Act, shall apply for the registration to the Registrar or as the case maybe to the Assistant Registrar.

(4) Procedures for registration of paralegals under this Act, shall be as prescribed under the regulations.

(5) A paralegal shall not engage in an activity that is reserved for advocates under any written law.

(6) A paralegal shall not charge any fee from an aided person for the provision of legal aid under this Act.

(7) A person who contravenes a provision of this section, commits an offence and shall, upon conviction, be liable to a fine not less than one million shillings or to imprisonment for a term not less than three months, or to both.

PART V
PROVISION OF LEGAL AID

*(a) General provisions*

Application for legal aid

**21.**-(1) An indigent person who intends to receive legal aid may apply to the Registrar, Assistant Registrar or legal aid provider.

(2) The Registrar or Assistant Registrar shall, upon receipt of the application under subsection (1), refer such application to the legal aid provider for provision of legal aid service to the applicant.

(3) An application under subsection (1) shall, with respect to the applicant's eligibility for legal aid services, be assessed in accordance with the legal aid providers procedures.

Person who may apply for legal aid

**22.** An application for legal aid may be made by-

(a) the indigent person;
(b) any other person authorised by the indigent person; or

(c) any person or an institution on behalf of the indigent person where the authority of the indigent person cannot be reasonably obtained.

General principles of legal aid

**23.** Subject to sections 20(6) and 25, the legal advice, assistance or representation through legal aid shall not affect the relationship between the rights of an advocate and a client or any privilege arising out of such relationship.

Legal aid to be provided by institutions

**24.**-(1) Pursuant to the provisions of this Act, legal aid services shall be provided by an advocate or a paralegal on behalf of the legal aid provider.

(2) A person shall not provide legal aid services unless that person is an advocate or paralegal attached to a legal aid provider.

(3) Any person who contravenes the provisions of this section commits an offence and shall, upon conviction, be liable to a fine not less than one million shillings or to imprisonment for a term not less than three months, or both.

Unauthorised payments

**25.**-(1) A legal aid provider shall not demand, request or receive payment from or, in respect of an aided person, in relation to services rendered under this Act, unless such payment is authorised under this Act.

(2) Any person who contravenes the provisions of subsection (1) commits an offence and shall, upon conviction, be liable to a fine not less than two million shillings or to imprisonment for a term not less than **six** months, or both.

(3) In addition to the sentence imposed under subsection (2), a person who is convicted for receiving payment shall be required to refund the amount he received from the aided person.

Records, monitoring and evaluation

**26.**-(1) A legal aid provider shall-

(a) provide legal services with a view to protecting the interests of the aided person;

and

(b) keep proper records of activities undertaken on behalf of an aided person and submit the same to the Registrar annually or as may be directed by the Registrar.

(2) The Registrar or the Assistant Registrar as the case may be, shall monitor and evaluate the activities and the quality of legal services offered by a legal aid provider under sub-section (1).

*(b) Legal aid in civil proceedings*

Legal aid in civil proceedings by order of the court

**27.** Where in any civil proceedings it appears to the presiding judge or magistrate that-

(a) in the interests of justice a person should have legal aid; and

(b) such person has insufficient means to enable him to obtain the legal services,

the presiding judge or magistrate, as the case may be, shall cause such person to obtain legal aid.

Notification of other parties

**28.**-(1) Where a party to civil proceedings is granted legal aid, the legal aid provider shall immediately notify every other party to the proceedings and to the court, of that fact.

(2) Where any other person subsequently becomes a party to the proceedings, the legal aid provider shall give notice to the new party.

(3) Where the legal aid provider withdraws, the legal aid provider shall immediately notify all parties to the proceedings and the court, of that fact.

Recovery of costs

**29.** Where an aided person has been awarded costs in any proceedings, such person shall be entitled to the costs, provided that the legal aid provider may have the right to deduct from the award, the costs he incurred in respect of the proceedings.

Execution of judgments

**30.** A legal aid provider shall take necessary measures to execute a judgment or any settlement in order to recover the proceeds of proceedings.

Costs against aided person

**31.**-(1) Where an aided person receives legal aid for civil proceedings and loses the case, the court shall not award an order of costs against the aided person, unless there are exceptional circumstances.

(2) In determining whether there are exceptional circumstances under subsection (1), the court shall take into account any of the following by the aided person-

(a) conduct that causes the other party to incur unnecessary costs;

(b) unreasonable refusal to negotiate a settlement or participate in alternative dispute resolution;

(c) misleading or deceitful conduct; or

(d) other conduct that abuses the processes of the court.

(3) Where costs are awarded against the aided person, the legal aid provider shall not be liable for payment of such costs.

Aided person not required to provide security for costs

**32.** Notwithstanding the provisions of any written law, an aided person shall not be required to furnish security for costs during the trial or appeal proceedings.

*(c) Legal aid in criminal matters*

Legal aid by order of the court

**33.**-(1) Where in any criminal proceedings, it appears to the presiding judge or magistrate that-

(a) in the interests of justice an accused person should have legal aid in the preparation and conduct of his defence or appeal as the case may be; and

(b) his means are insufficient to enable him to obtain legal services,

the presiding judge or magistrate, as the case may be, shall certify that the accused ought to have such legal aid and upon such certificate being issued, the Registrar shall assign to the accused a legal aid

provider which has an advocate for the purpose of preparation and conduct of his defence or appeal, as the case may be.

(2) Where in any criminal proceedings a child is an accused, the presiding judge or magistrate shall certify that the accused ought to have such legal aid and upon such certificate being issued the Registrar shall assign to the accused an advocate for the purpose of preparation and conduct of his defence or appeal, as the case may be.

(3) The Chief Justice shall, by rules published in the *Gazette*, determine the remuneration of advocates assigned to accused person under the provisions of subsection (1) and (2) and the same shall be paid from the Judicial Fund.

(4) For the purpose of this section "Registrar" means the Registrar of the High Court.

Expenses incurred by advocates

**34**.-(1) Where a legal aid provider which is assigned to an accused person under the provisions of this Act incurs any special expenditure arising out of the performance of its duties, it may submit a claim to the Chief Court Administrator.

(2) The Chief Court Administrator may, if he is satisfied that the full claim or the portion thereof is reasonable, authorize payment to the legal aid provider of such claim or such portion, as the case may be.

(3) Any dispute arising out of the decision of the Chief Court Administrator under subsection (2) may be referred to the Chief Justice, whose decision thereon shall be final.

Legal aid for children in police stations or prisons

**35.** Where a police officer, a prison officer or any other person charged with a duty of supervising the welfare of a child, in execution of his duties, deals with a child as an accused or a convict, he shall cause such child to obtain legal aid.

Legal aid for persons in

**36.** A police station or prison shall designate a mechanism for facilitating the provisions of legal aid

custody

services by legal aid providers to accused or a convict in custody.

## PART VI
## FINANCIAL PROVISIONS

Sources of fund of the Board

**37.** The funds of the Board shall consist of-

(a) any sums that may be appropriated by the Parliament;

(b) any monies raised by way of donations or grants made within and outside the United Republic of Tanzania; and

(c) such sums of money or assets which may vest in or accrue to the Board from other sources by way of fees, grants or in any other way under this Act or any other written law or in respect of the matter incidental to the carrying out of its functions.

Annual estimates

**38**.-(1) The Board shall, before the commencement of a financial year, cause to be prepared, estimates of the revenue and expenditure for the year.

(2) The annual estimates shall make provision for all estimated expenditure of the Board for a financial year concerned, and the Board shall in particular, approve recurrent and development expenditure.

(3) The annual estimates shall be submitted to the Minister who shall cause them to be laid before the National Assembly within three months from the date of their submission to him.

Annual performance report

**39**. The Registrar shall, within three months, prepare and submit to the Minister an annual report on the performance of the Board during the financial year and the Minister shall cause a copy of the report to be laid before the National Assembly.

Books of accounts

**40**.-(1) The Board shall keep proper books of accounts.

(2) Within three months from the end of each

financial year, the Board shall submit to the Controller and Auditor General accounts of the Board together with-

(a) a statement of financial activities and income and expenditure during that financial year; and

(b) a statement of assets and liabilities of the Board existing at the end of such financial year.

(3) The accounts of the Board shall be audited by the Controller and Auditor General.

PART VII
MISCELLANEOUS PROVISIONS

Registrar may require proof of existence

**41**.-(1) Where the Registrar has reason to suspect that a legal aid provider has ceased to exist or he is no longer providing legal aid, he may issue a notice in writing to the office bearers of that legal aid provider or publish a notice in a newspaper widely circulating in Mainland Tanzania, requiring him to submit to the Registrar within a period of thirty days, proof of his existence.

(2) Where the legal aid provider fails to submit to the Registrar proof of his existence, the Registrar shall cancel the certificate of its registration and remove its name from the register.

Obligations relating to professional conduct

**42**.-(1) An advocate who provides legal aid under this Act shall be required to adhere to any rules or codes of conduct of a professional body to which he belongs and his rights, obligations, responsibilities, or duties as a member of such body shall not in any way be affected by the provisions of this Act.

(2) The Minister shall, by notice published in the *Gazette*, provide a code of conduct for legal aid providers and paralegals.

(3) The code of conduct referred to under subsection (2) shall provide for-

(a) the protection of the rights and interests of an

aided person;
(b) duties to the aided person, the Registrar and court;
(c) conflict of interest;
(d) observance of confidentiality;
(e) in the case of professionals, the duty to observe prescribed ethical standards of their respective professional bodies;
(f) probity and ethical conduct; and
(g) any other matter connected therewith.

Prohibition from political activities

**43**.-(1) Subject to the provisions of this Act, no legal aid provider, advocate or paralegal shall engage in any political activities.

(2) A person who contravenes subsection (1), commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not less than five million shillings but not more than ten million shillings or to imprisonment for a term not less than six months but not more than twelve months or to both.

Prohibition of misuse of funds for legal aid

**44**.-(1) Every legal aid provider or any person receiving funds, aid or other kind of assistance for the purpose of providing legal aid under this Act, shall ensure that such funds, aid or assistance received is used for the provision of legal aid under this Act.

(2) Any person who contravenes this section commits an offence and shall, on conviction, be liable to a fine of not less than ten million shillings but not exceeding fifteen million or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding twelve months or to both.

General offences

**45**. A person who:
(a) fraudulently makes, causes or permits to be made, any false or incorrect entry in the Register or any copy of it;
(b) provides legal aid without having qualifications as prescribed under this Act;
(c) makes any statement which is false in a material particular or misleading, with a view

to gaining any advantage or privilege under this Act;
(d) impersonates any person registered or deemed to be registered in terms of this Act;
(e) refuses or fails without lawful cause to appear, having been duly summoned to appear, at an inquiry by the Registrar under this Act; and
(f) obstructs or hinders a member of the Board or the Registrar or of any other person in the exercise of his powers or the performance of his functions under this Act,

commits an offence, and upon conviction, shall be liable to a fine of not less than one million shillings or imprisonment for a term of not less than six months or both.

Publication of legal aid providers

**46**. The Registrar shall, annually, publish in the *Gazette*, in widely circulating newspapers in Mainland Tanzania, and in any other means of communication the names of registered legal aid providers, and legal aid providers whose names have been cancelled.

Powers of the Minister to make regulations

**47**.-(1) The Minister may make regulations for the better carrying into effect of the provisions of this Act.

(2) Notwithstanding the generality of subsection (1), the Regulations made under this Act may provide for-

(a) the procedures for the provision of legal aid to persons detained at police stations, or in remand, prison or other places of lawful custody;
(b) procedures, terms and conditions of registration of legal aid providers and paralegals;
(c) procedures for inspection of legal aid providers;
(d) fees to be paid under this Act;
(e) procedures for management of disputes and complaints under this Act;
(f) the records to be kept by legal aid providers

in relation to legal aid assignments and the reports to be submitted to the Registrar;

(g) the amount payable by an aided person;

(h) procedures for appeal under this Act, and

(i) any other matter which is required to be prescribed under this Act.

Repeal and saving

**48**.-(1) The Legal Aid (Criminal Proceedings) Act is hereby repealed.

Cap. 21

(2) Notwithstanding subsection (1), all orders, rules, guidelines, directives and regulations made under the repeal Act, shall have effect until such other subsidiary legislations are made under this Act.

Transitional arrangement

**49**.-(1) Notwithstanding the provisions of this Act, all legal aid arrangements which are in existence on the date of commencement of this Act shall be continued and concluded as if this Act had not been passed.

(2) All institutions that provide legal aid services shall continue to provide the services until the expiry of the period of twelve months from the date of coming into force of this Act and whereupon they shall cease to provide the services and be required to register in accordance with this Act.

## SCHEDULE

*(Made under section 4(2))*

### COMPOSITION, TENURE OF OFFICE AND PROCEEDINGS OF THE BOARD

Composition

**1**.-(1) The National Legal Aid Advisory Board shall consist of the Chairman and other seven members appointed by the Minister as follows:

(a) a Chairman who is a Judge of the High Court of Tanzania appointed by the Minister in consultation with the Chief Justice;
(b) the Attorney General or his representative not below the rank of law officer;
(c) one representative from legal aid providers;
(d) the Commissioner for Social Welfare or his representative;
(e) the Inspector General of Police or his representative who is not below the rank of the Commissioner;
(f) the Commissioner General of Prisons or his representative who is not below the rank of the Commissioner;
(g) Director of legal services from the Ministry responsible for Local Government Authority or his representative;
(h) a representative of persons with disability; and
(i) one representative from paralegal organisations umbrella body.

(2) The appointing authority shall in appointing members under subparagraph (1) ensure that there is gender representation in the Board.

(3) The Board may co-opt such number of persons to represent any interest as the Board may determine except that the co-opted member shall not have the right to vote.

Vice-Chairman

**2.** The members shall elect one amongst their number to be Vice-Chairman of Board, and any member elected as Vice-Chairman, may subject to his continuing to be a Vice-Chairman, hold office for a term of three years from the date of his election.

Tenure of office

**3.**-(1) The members of the Board shall hold office for a period of three years and shall be eligible for re-appointment for a further period of three years.

(2) A member of the Board may at any time resign his office by giving notice in writing addressed to the Minister, and from the date specified in the notice or, if no date is so specified, from the date of the receipt of the notice by the Minister, he shall cease to be a member.

Vacancy

**4.** Where any member ceases to be a member for any reason before the expiration of his term of office, the appointing authority may appoint another person in his place and the person so appointed shall hold office for the remainder of the term of his predecessor.

Meetings of the Board

**5.**-(1) The Board shall ordinarily meet for the transaction of its business at the time and at the place determined by it, but shall meet at least once in every three months.

(2) The Chairman, or in his absence the Vice-Chairman, shall preside at every meeting of the Board and in the absence of both, the Chairman and the Vice-Chairman, the members present shall appoint one of their number to preside over the meeting.

(3) The Chairman or in his absence the Vice-Chairman, may at any time call special meeting of the Board to deliberate on any matter which he considers to be urgent.

(4) The Chairman, or in his absence the Vice-Chairman may invite any person who is not a member to participate in the deliberations at any meeting of the Board, but the person so invited shall not be entitled to vote.

Quorum

**6.** The Quorum at any meeting of the Board shall be at least five members.

Decision of the Board

**7.**-(1) Matters proposed at a meeting of the Board shall be decided by a majority of the votes of the members present and voting and in the event of any equality of votes the person presiding shall have a second casting vote in addition to his original or deliberative vote.

(2) A decision may be made by the Board without a

meeting by a circulation of the relevant papers amongst the members and the expression of the views of the majority of the members in writing shall be honoured but any member may require that the decision be deferred and the subject matter be considered at a meeting of the Board.

Minutes of the meetings

**8.**-(1) The Board shall cause to be recorded and kept minutes of all business conducted or transacted at its meetings, and the minutes of each meeting of the Board shall be read and confirmed, or amended and confirmed, at the next meeting of the Board and signed by the person presiding at the meeting and the secretary.

(2) Any minutes purporting to be signed by the person presiding at a meeting of the Board shall, in the absence of proof of error, be deemed to be a correct record of the meeting whose minutes they purport to be.

Vacancies not to invalidate proceedings

**9.** The validity of any act or proceeding of the Board shall not be affected by any vacancy among its member or by any defect proceedings in the appointment of any of them.

Orders and directions of the Board

**10.** All orders, directions, notices or other documents made or issued on behalf of the Board shall be signed by-

(a) the Chairman or Vice-Chairman of the Board, as the case may be; or

(b) the Secretary.

Remuneration of members of the Board

**11.** A member of the Board shall be entitled to such remuneration, fees or allowances for expenses as the Minister may, upon recommendations of the Board prescribe from time to time,

Board may regulate proceedings

**12.** Subject to the provisions of this Schedule, the Board may regulate its own proceedings.

______________

**OBJECTS AND REASONS**

______________

At present there is no legal aid framework in the country to regulate and coordinate the provision of legal aid. The State provides limited assistance to accused persons being tried for capital offences such as murder, manslaughter and treason. However, such assistance is mainly limited to the High Court. Various civil society organisations provide for some services ranging from legal advice to legal representation in court. This work is not coordinated between the various organisations and the Government. The schemes run by the civil society organisations are heavily dependent on donor funding which are not always forthcoming and thus impacts negatively on sustainability.

Further, the increase of legal aid providers and paralegals attracts the need to have them regulated and coordinated.

Thus, the Bill seeks to introduce a comprehensive legal framework that will fill the gap and work as a solution in eliminating the preceeding challenges and ensuring that legal aid in the country brings about positive impact in the welfare of individuals especially indigent persons.

For the purpose of appreciating the intended objectives, the Bill is divided into Seven Parts.

Part I contains preliminary provisions which include short title, application and interpretation of various term used in the proposed Bill.

Part II provides for the provisions on administration and coordination of legal aid providers, establishes Legal Aid Advisory Board and its function, also provides for the designation of the Registrar and his functions. Further, it provides for the appointment of the Assistant Registrars and registration of legal aid providers at regional and district level.

Part III provides for the provisions on registration for legal aid providers, outlines the qualifications for registration as legal aid provider, issuance of a certificate of registration to a legal aid provider, circumstances which will lead to suspension or cancellation of certificate of registration, rights to appeal against the decision of suspension or cancelation of certificate.

Part IV of the Bill provides for special provisions on paralegals, their qualifications, duties and the requirement of paralegals to provide legal advice and assistance in accordance with the provisions of the proposed Bill. Paralegals are

restricted from charging fees from any aided person and to engage on activity reserved for advocates.

Part V of the Bill provides for persons who may apply for legal aid, general principles of legal aid, legal aid in civil proceedings and criminal proceedings by order of the Court. Further, it provides for legal aid to children and persons in police stations, prison and any other lawfully custody.

Part VI of the Bill deals with financial provisions. It contains provisions relating to sources of funds of the Board, annual estimates, an annual performance report and books of accounts.

Part VII of the Bill provides for Miscellaneous provisions, power of the Registrar to issue notice to require proof of existence of legal aid providers, obligation relating to professional conduct of legal aid providers, powers of the Minister to make regulations and code of conduct for legal aid providers and paralegals. Further, the Part provides for the repeal, savings and transitional arrangements.

Dar es Salaam,
2nd August, 2016

**HARRISON G. MWAKYEMBE**
*Minister for Constitutional and*
*Legal Affairs*

SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA, 2016

MPANGILIO WA VIFUNGU

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kifungu* *Jina*


1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.


## SEHEMU YA PILI
## USIMAMIZI NA URATIBU WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA


4. Uanzishwaji wa Bodi.
5. Kazi za Bodi.
6. Msajili wa utoaji wa msaada wa kisheria.
7. Kazi za Msajili.
8. Uteuzi wa Wasajili Wasaidizi.


## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA


9. Daftari la watoa huduma ya msaada wa kisheria.
10. Sifa za usajili wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria.
11. Maombi ya usajili.
12. Ushughulikiaji wa maombi.
13. Kukataliwa kwa usajili.
14. Rufaa.
15. Cheti cha usajili.
16. Kusitishwa na kufutwa kwa cheti.
17. Utaratibu wa kusitisha au kufuta.
18. Usimamizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria.


## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MAALUM KWA WASAIDIZI WA KISHERIA


19. Sifa za wasaidizi wa sheria.
20. Huduma ya msaada wa kisheria ya wasaidizi wa kisheria.

SEHEMU YA TANO
UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA

*(a) Masharti ya Jumla*

21. Maombi ya huduma ya msaada wa kisheria.
22. Mtu anayeweza kuomba huduma ya msaada wa kisheria.
23. Kanuni za jumla za huduma ya msaada wa kisheria.
24. Huduma za msaada wa kisheria zinazotolewa na taasisi.
25. Malipo yasiyoruhusiwa.
26. Kumbukumbu, ufuatiliaji na tathmini.

*(b) Msaada wa kisheria katika mashauri ya madai*

27. Msaada wa kisheria katika mashauri ya madai kwa amri ya mahakama.
28. Taarifa kwa upande mwingine.
29. Urejeshwaji wa gharama.
30. Utekelezaji wa hukumu.
31. Gharama dhidi ya mtu aliyesaidiwa.
32. Mtu anayesaidiwa kutotakiwa kutoa dhamana ya gharama ya shauri.

*(c) Msaada wa Kisheria kwenye Mashauri ya Jinai*

33. Msaada wa kisheria kwa amri ya mahakama.
34. Gharama atakazopata wakili.
35. Msaada wa kisheria kwa watoto walio katika vituo vya polisi au magereza.
36. Msaada wa kisheria kwa watu walio kizuizini.

SEHEMU YA SITA
MASUALA YA FEDHA

37. Vyanzo vya mapato ya Bodi.
38. Makadirio ya Mwaka.
39. Taarifa ya mwaka ya utekelezaji.
40. Vitabu vya hesabu.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI MENGINEYO

41. Msajili anaweza kuhitaji uthibitisho wa uwepo wa mtoa huduma.
42. Wajibu kuhusiana na maadili ya kitaaluma.
43. Katazo kuhusu shughuli za kisiasa.
44. Matumizi mabaya ya fedha za misaada ya kisheria.
45. Makosa ya jumla.
46. Kutangazwa kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria.
47. Mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni.
48. Kufutwa Sheria ya Msaada wa Kisheria.
49. Taratibu za mpito.

---

**JEDWALI**

---

---

**TAARIFA**

---

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma ukiwa pamoja na maelezo yake ya madhumuni na sababu.

Dar es Salaam,
7 Agosti, 2016

**JOHN N. KIJAZI**
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

**MUSWADA**
*wa*

**Sheria ya kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watu wasiokuwa na uwezo, kuwatambua wasaidizi wa kisheria, kufuta Sheria ya Msaada wa Kisheria (katika Mashauri ya Jinai) na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria, 2016 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri atateua kupitia Tangazo litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2.** Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"wakili" maana yake ni wakili anayefanya kazi za uwakili;

"mtu anayesaidiwa" maana yake ni mtu anayepatiwa msaada wa kisheria chini ya Sheria hii;

"Msajili Msaidizi" maana yake ni Msajili Msaidizi anayetajwa katika kifungu cha 8.

"Bodi" maana yake ni Bodi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

"Mtendaji Mkuu wa Mahakama" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Mahakama aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama;

"mtu asiye na uwezo" maana yake ni mtu asiye na uwezo wa kumudu gharama za wakili wa kujitegemea na atajumuisha makundi mengine ya watu kama itakavyohitajika kwa maslahi ya utoaji haki;

"ushauri na msaada wa kisheria" maana yake ni ushauri na msaada unaotolewa kwa mtu asiye na uwezo katika kesi za jinai na madai kuhusu sheria husika, taratibu za kisheria na uandaaji wa nyaraka za kisheria;

"msaada wa kisheria" au "huduma ya kisheria" inajumuisha utoaji wa ushauri wa kisheria, usaidizi wa kisheria au uwakilishi kwa watu wasiokuwa na uwezo;

"mtoa huduma ya msaada wa kisheria" maana yake ni taasisi iliyosajiliwa chini ya Sheria hii kutoa huduma ya msaada wa kisheria;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na mambo ya sheria;

"msaidizi wa kisheria" maana yake ni mtu anayetoa huduma ya msaada wa kisheria chini ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria;

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na mambo ya sheria; na

"Msajili" maana yake ni msajili aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 6;

"Rejesta" maana yake ni Rejesta ya watoa msaada wa kisheria iliyoanzishwa chini ya sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## USIMAMIZI NA URATIBU WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA

Uanzishwaji wa Bodi

**4.**-(1) Kutakuwa na Bodi itakayoitwa Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria.

(2) Masharti ya Jedwali la Sheria hii yatatumika kuainisha muundo wa Bodi, muda wa ukomo wa Bodi, uendeshaji wa mikutano na masuala mengine yanayohusiana na Bodi.

(3) Isipokuwa kwa wajumbe wa Bodi, Waziri atakuwa

na mamlaka ya kurekebisha, kusahihisha au kubadilisha Jedwali.

Kazi za Bodi

**5.**-(1) Kazi za Bodi zitakuwa ni:
(a) kutoa miongozo ya kisera kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria kwa ajili ya kuoanisha kazi zao na mipango ya maendeleo ya Taifa;
(b) kumshauri Waziri juu ya masuala ya kisera na mambo mengine yahusianayo na uboreshaji wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria;
(c) kuthibitisha taarifa ya mwaka ya watoa huduma ya msaada wa kisheria;
(d) kuamua rufaa zinazotokana na uamuzi wa Msajili;
(e) kutekeleza majukumu mengine kadri itakavyoelekezwa na Waziri.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Bodi itadumisha kwa kadri itakavyowezekana, mfumo wa mashauriano na ushirikiano na Wizara, taasisi za Serikali, watoa huduma za msaada wa kisheria au vyombo vingine vya umma au binafsi vilivyoanzishwa chini ya sheria yoyote ya Bunge.

Msajili wa utoaji wa msaada wa kisheria

**6.**-(1) Kutakuwa na Msajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria.

(2) Mkurugenzi anayehusika na masuala ya msaada wa kisheria katika Wizara yenye dhamana na mambo ya sheria atakuwa Msajili.

Kazi za Msajili

**7.**-(1) Kazi na majukumu ya Msajili yatakuwa ni:
(a) kusajili watoa huduma za msaada wa kisheria;
(b) kuchunguza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili, uzembe, utovu wa nidhamu au kutotii dhidi ya watoa huduma za msaada wa kisheria;
(c) kusitisha au kufuta usajili wa mtoa huduma yeyote wa msaada wa kisheria;
(d) kuhifadhi na kutunza daftari la orodha ya watoa huduma ya msaada wa kisheria;
(e) kukagua ofisi yoyote ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa huduma ya msaada wa kisheria inayotolewa;

(f) kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kukuza uelewa na ufahamu wa masuala ya kisheria kwa umma hususani kuelimisha makundi ya wanyonge kuhusu haki na wajibu chini ya Katiba na sheria nyingine;

(g) kuratibu na kuwezesha uazishwaji na utambuzi wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wasaidizi wa kisheria;

(h) kuratibu, kufuatilia na kutathmini kazi za watoa huduma ya msaada wa kisheria na kutoa miongozo ya jumla na mahsusi kwa utelekezaji bora wa programu za huduma ya msaada wa kisheria;

(i) kutunza kumbukumbu na taarifa kuhusu watoa huduma ya msaada wa kisheria;

(j) kuandaa taarifa mbalimbalikuhsu huduma ya msaada wa kisheria na masuala mengine ya kuwasilisha kwenye Bodi;

(k) kuwezesha ushirikishwaji wa taarifa kwa njia rafiki na kutoa miongozo ya kimahusiano baina ya watoa huduma za msaada wa kisheria na Serikali; na

(l) kutolea uamuzi migogoro baina ya watoa huduma ya msaada wa kisheria isipokuwa mawakili, na migogoro baina ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wapewa huduma ya msaada wa kisheria;

(m) kufanya kazi nyingine yoyote kama atakavyoelekezwa na Waziri au Bodi.

(2) Msajili atakuwa Katibu wa Bodi.

(3) Msajili katika utendaji na utekelezaji wa kazi na majukumu yake chini ya sheria hii:

(a) atasaidiwa na maafisa wa wizara yenye dhamana na masuala ya kisheria kama itakavyoamriwa; na

(b) atawajibika kwa Katibu Mkuu ambaye atakuwa ni kiungo kati ya Serikali na watoa huduma ya msaada wa kisheria.

Uteuzi wa Wasajili Wasaidizi

**8.**-(1) Katibu Mkuu, kwa madhumuni ya kuwezesha usajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi ya mkoa na wilaya, na baada ya kushauriana na mamlaka husika, atateua katika kila mkoa au wilaya,

mtumishi wa umma kutoka miongoni mwa watumishi wa umma ndani ya mkoa au wilaya kuwa Msajili Msaidizi.

(2) Isipokuwa kwa masharti ya kifungu cha 11(5), Msajili Msaidizi aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1), kwa niaba ya Msajili, atasajili mtoa huduma ya msaada wa kisheria ndani ya Mkoa au Wilaya ambayo ameteuliwa na kutoa cheti cha usajili.

(3) Msajili Msaidizi aliyeteuliwa chini ya kifungu hiki, katika kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii, atawajibika kwa Msajili.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA

Rejesta ya watoa huduma ya msaada wa kisheria

**9.**-(1) Kutakuwa na Rejesta ya watoa huduma ya msaada wa kisheria ambayo itakuwa na majina ya taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria, huduma zinazotolewa na mambo mengine kama yatakavyobainishwa.

(2) Msajili atahakikisha kuwa Rejesta iliyo katika nakala mango au nakala tete inapatikana kwa umma katika vituo vya polisi, mahakama, magereza na maeneo mengine ya umma kama itakavyoamuliwa na Waziri.

Sifa za usajili wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria

**10.**-(1) Taasisi haitasajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria isipokuwa kama itakuwa na sifa zifuatazo:

(a) imesajiliwa chini ya sheria husika;
(b) utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria ni moja ya majukumu yake ya msingi;
(c) ina majengo ya ofisi na vifaa vya ofisi;
(d) ina si chini ya:
   (i) mawakili wawili;
   (ii) wakili mmoja na wasaidizi wa kisheria wawili; au
   (iii) wasaidizi wa kisheria watatu; na
(e) imepitishwa na taasisi iliyoisajili kuhusu kumbukumbu zake za usimamizi wa fedha na mambo mengine kama yatakavyoainishwa na Waziri.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), taasisi

isiyokuwa na wakili itatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa kuwa chini ya uangalizi wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria mwingine mwenye wakili kabla ya kusajiliwa.

(3) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha kwanza (1) kwa ujumla wake, masharti ya aya (a) na (b) hayatatumika kwa taasisi iliyoanzishwa na sheria ya Bunge au taasisi yoyote ya kitaaluma inayotambulika chini ya sheria nyingine.

Maombi ya usajili

**11.**-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 10, taasisi inayoomba usajili chini ya sheria hii, inapaswa kuomba kwa mujibu wa kanuni za Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), maombi ya usajili yanatakiwa kuambatanishwa na-

(a) nakala ya katiba ya taasisi hiyo au nyaraka yoyote iliyoianzisha;
(b) taarifa binafsi za wenye ofisi, mawakili au wasaidizi wa kisheria;
(c) taarifa zinazohusu anwani ya eneo yalipo makao makuu ya taasisi hiyo;
(d) nakala ya hati safi kutoka mamlaka ya usajili wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria;
(e) ada ya usajili iliyobainishwa kwenye kanuni; na
(f) maelezo au taarifa nyingine kama zitakavyohitajika na Msajili.

(3) Pale ambapo taasisi inakusudia kutoa huduma ya msaada wa kisheria katika wilaya zaidi ya moja au katika mkoa mzima, maombi ya usajili wake yatawasilishwa kwa Msajili Msaidizi wa mkoa husika.

(4) Pale ambapo taasisi inakusudia kutoa huduma ya msaada wa kisheria katika wilaya, maombi ya usajili wake yatawasilishwa kwa Msajili Msaidizi wa wilaya husika.

(5) Pale ambapo taasisi inakusudia kutoa huduma ya msaada wa kisheria katika mkoa zaidi ya mmoja au imesajiliwa nje ya nchi, maombi ya usajili wake yatawasilishwa kwa Msajili.

(6) Pale ambapo Msajili Msaidizi amemsajili mtoa huduma ya msaada wa kisheria, ataandaa taarifa na kuiwasilisha taarifa hiyo kwa Msajili;

(7) Waziri, kwa kutumia kanuni, atatoa utaratibu utakaotumiwa na wasajili wasaidizi katika usajili na shughuli

za watoa huduma ya msaada wa kisheria waliosajiliwa katika ngazi Mkoa na Wilaya kwa mujibu wa Sheria hii.

Ushughulikiaji wa maombi

**12.**-(1) Msajili au kwa kadri itakavyokuwa Msajili Msaidizi, atazingatia na kuamua kuhusu maombi ya usajili ndani ya mwezi mmoja baada ya kupokea maombi hayo.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), katika kuamua kuhusu maombi, Msajili au kwa kadri itakavyokuwa Msajili Msaidizi, anaweza kusajili au kutosajili taasisi kuwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria.

Kukataliwa kwa usajili

**13.**-(1) Msajili au Msajili Msaidizi anaweza kukataa kusajili taasisi kuwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria endapo atajiridhisha kwamba-

(a) haijatimiza masharti yaliyoainishwa katika kifungu cha 10; au

(b) imetoa taarifa za uongo au za kupotosha kwa namna yoyote ile.

(2) Endapo Msajili au Msajili Msaidizi amekataa kusajili taasisi kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, anatakiwa ndani ya siku ishirini na moja tangu tarehe ya maamuzi, kumtaarifu mwombaji sababu za kukataa kwake.

Rufaa

**14.**-(1) Taasisi ambayo haitaridhika na uamuzi wa Msajili au Msajili Msaidizi chini ya kifungu cha 13 inaweza, ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea uamuzi huo kukata rufaa kwa Bodi au kwa Msajili kwa kadri itakavyokuwa.

(2) Taasisi ambayo haitaridhishwa na uamuzi wa Bodi inaweza, ndani ya siku thelathini tangu tarehe aliyopokea uamuzi huo, kukata rufaa kwa Waziri.

(3) Waziri, ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea rufaa, atapitia na kutoa uamuzi kuhusu rufaa hiyo.

Cheti cha usajili

**15.**-(1) Msajili au Msajili Msaidizi baada ya kuisajili taasisi kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria na baada ya kupokea malipo ya ada itakayoainishwa, atatoa cheti cha usajili kama itakayoainishwa kwenye kanuni.

(2) Cheti cha usajili kitakuwa na-

(a) jina na anwani ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria;

(b) eneo la kutolea huduma ya msaada wa kisheria;
(c) hadhi ya taasisi; na
(d) vigezo na masharti ambayo cheti hicho kimetolewa.

(3) Cheti cha usajili kilichotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) kitakuwa uthibitisho wa mwisho kwa taasisi kufanya kazi kama mtoa huduma za msaada wa kisheria chini ya Sheria hii.

Kusitishwa na kufutwa kwa cheti

**16.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 17, Msajili anaweza kutoa onyo la maandishi, kusitisha au kufuta cheti cha usajili cha mtoa huduma za msaada wa kisheria.

(2) Msajili anaweza kusitisha cheti cha usajili cha mtoa huduma ya msaada wa kisheria iwapo atajiridhisha kwamba:
(a) mtoa huduma ya msaada wa kisheria ametenda kosa la kitaaluma au ameshindwa kumchukulia hatua za kinidhamu mtumishi wake kwa kukiuka taratibu za kitaaluma au kukiuka maadili yaliyowekwa na chombo husika cha kitaalum;
(b) mtoa huduma ya msaada wa kisheria amekiuka miiko ya kinidhamu iliyoainishwa chini ya Sheria hii au chini ya sheria nyingine yoyote;
(c) mtoa huduma ya msaada wa kisheria anatekeleza majukumu yake kinyume na katiba yake; au
(d) mtoa huduma ya msaada wa kisheria ameshindwa kuhifadhi kumbukumbu sahihi za kazi zilizofanywa kwa niaba ya mtu aliyesaidiwa na Msajili anaona kwamba kitendo hicho kitaathiri maslahi ya mtu aliyesaidiwa kwa ujumla au kwa namna nyingine yoyote.

(3) Msajili anaweza kufuta cheti cha usajili cha mtoa huduma ya msaada wa kisheria iwapo ataridhika kwamba-

(a) usajili umepatikana kimakosa, kwa udanganyifu, kwa ujanja, ushawishi usio halali au kwa taarifa za kupotosha;
(b) mtoa huduma ya msaada wa kisheria ameshindwa kutimiza masharti ya usajili;
(c) sifa za kusajiliwa zimekoma kwa mtoa huduma ya

msaada wa kisheria;

(d) mwenye ofisi ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria ametangazwa kufilisika, amefilisiwa au ameingia katika makubaliano na wadeni wake;

(e) wakili au msaidizi wa kisheria aliyeajiriwa na mtoa msaada wa kisheria amekuwa akikiuka mara kwa mara maadili ya kitaaluma;

(f) mtoa msaada wa kisheria amekuwa akijishughulisha na shughuli za kisiasa;

(g) mwenye ofisi ya kutoa huduma za msaada wa kisheria ametiwa hatiani kwa makosa yanayohusu uadilifu, uwajibikaji wake au amepewa amri chini ya chombo husika; au

(h) mtoa huduma ya msaada wa kisheria hatoi, au hajatoa huduma ambayo amesajiliwa kuitoa kwa kiwango kilichowekwa.

(4) Pale ambapo Msajili atasitisha au kufuta cheti cha usajili:

(a) atamtaarifu mtoa huduma ya msaada wa kisheria kuhusu uamuzi wake na kuamuru mtoa huduma za msaada wa kisheria husika kuacha kufanya kazi hiyo; au

(b) kuondoa jina lake kwenye Rejesta, kadri itakavyokuwa.

Utaratibu wa kusitisha au kufuta

**17.**-(1) Pale ambapo mtoa huduma za msaada wa kisheria atakiuka vigezo na masharti yanayohusiana na kutolewa kwa cheti, au amekiuka masharti ya kifungu cha 16, Msajili anaweza kumpatia mtoa huduma za msaada wa kisheria taarifa ya ukiukwaji kwa maandishi akieleza aina ya ukiukwaji.

(2) Baada ya kupokea taarifa ya ukiukwaji, mtoa huduma za msaada wa kisheria atawasilisha maelezo kwa maandishi kwa Msajili kuhusu kushughulikia au kurekebisha makosa.

(3) Pale ambapo mtoa huduma za msaada wa kisheria atashindwa kushughulikia au kurekebisha makosa ndani ya muda uliowekwa kwenye taarifa ya ukiukwaji au hakuwasilisha maelezo yanayoridhisha kwa Msajili, Msajili atasitisha au kufuta cheti husika.

(4) Mtoa huduma za msaada wa kisheria ambaye cheti chake kimesitishwa au kufutwa anaweza kuomba kwa Msajili kufanya mapitio ya uamuzi wa kusitisha au kufuta cheti endapo hakuridhika na sababu za kusitishwa au kufutwa kwa cheti.

(5) Mtoa huduma za msaada wa kisheria ambaye hajaridhika na uamuzi wa Msajili wa kusitisha au kufuta cheti anaweza kukata rufaa kwa Bodi kwa mujibu wa kifungu cha 14.

Usimamizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria

**18.**-(1) Msajili Msaidizi, kwa madhumuni ya Sheria hii, atakuwa ndiye msimamizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria katika mkoa au wilaya husika.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi, Msajili Msaidizi-

(a) atakuwa na usimamizi wa jumla kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(b) atachunguza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili, uzembe, utovu wa nidhamu au kutotii na kutoa taarifa kwa Msajili kuhusu maelezo na hali ya malalamiko hayo; na

(c) atawasilisha kwa Msajili kila mwaka, majina ya watoa huduma ya msaada wa kisheria ambao wameacha kutoa huduma hiyo.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MAALUM KWA WASAIDIZI WA KISHERIA

Sifa za wasaidizi wa sheria

**19.**-(1) Msaidizi wa kisheria atatakiwa kuwa na moja kati ya yafuatayo:

(a) shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa;

(b) shahada ya sanaa ya utekelezaji wa sheria kutoka katika chuo kinachotambuliwa;

(c) stashahada ya sheria au mafunzo ya usaidizi wa sheria kutoka kwenye chuo kinachotambuliwa;

(d) astashahada ya sheria kutoka kwenye chuo kinachotambuliwa; au

(2) Pamoja na sifa zilizoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1), msaidizi wa kisheria atatakiwa kupata mafunzo mahsusi ya wasaidizi wa kisheria.

Huduma ya msaada wa kisheria wa wasaidizi wa kisheria

**20**.-(1) Msaidizi wa kisheria anaweza kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kujali masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1), msaidizi wa kisheria atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuendesha mafunzo kwa lugha ya taifa au ya asili kuhusu masuala ya kisheria na taratibu zinazohusu jamii husika;

(b) kumsaidia mtu anayehusika kuhusu taratibu za kupata nyaraka muhimu za kisheria;

(c) kutoa ushauri na msaada katika masuala ya ustawi wa jamii;

(d) kumwelekeza mtu anayesaidiwa njia sahihi ya kupata haki yake;

(e) kushauri pande zinazopingana kutafuta suluhu ya migogoro au kuwaelekeza kwenye vyombo vinavyohusika na usuluhishi wa migogoro; au

(f) kutoa taarifa zinazohusu uvunjifu wa amani, ukiukwaji wa sheria na haki za binadamu kwa taasisi husika.

(3) Mtu anayetaka kutoa huduma ya msaada wa kisheria kama msaidizi wa kisheria chini ya Sheria hii, atawasilisha maombi ya kusajiliwa kwa Msajili au kwa kadri itakavyokuwa kwa Msajili Msaidizi.

(4) Utaratibu wa usajili wa wasaidizi wa sheria chini ya Sheria hii utakuwa kama utakavyofafanuliwa kwenye kanuni.

(5) Msaidizi wa kisheria hatajihusisha na kazi zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya wakili chini ya sheria yoyote nyingine.

(6) Msaidizi wa kisheria hatamtoza mtu anayesaidiwa gharama yoyote ya kitaaluma kwa huduma ya msaada wa kisheria inayotolewa chini ya Sheria hii.

(7) Mtu anakayekiuka sharti la kifungu hiki, anatenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

SEHEMU YA TANO
UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA

*(a) Masharti ya Jumla*

Maombi ya huduma ya msaada wa kisheria

**21**.-(1) Mtu anayehitaji kupata huduma ya msaada wa kisheria atawasilisha maombi kwa Msajili, Msajili Msaidizi au mtoa huduma ya msaada wa kisheria.

(2) Msajili au Msajili Msaidizi, baada ya kupokea maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), atayawasilisha kwa mtoa huduma ya Msaada wa kisheria kwa ajili ya kutoa huduma ya kisheria kwa mwombaji.

(3) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) yatatathminiwa, kuhusiana na sifa za mwombaji wa huduma ya msaada wa kisheria, kwa mujibu wa taratibu za mtoa huduma ya msaada wa kisheria.

Mtu anayeweza kuomba huduma ya msaada wa kisheriaa

**22.** Maombi ya huduma ya msaada wa kisheria yanaweza kufanywa na-

(a) mwombaji mwenyewe;
(b) mtu mwingine yeyote aliyeruhusiwa na mwombaji; au
(c) mtu au taasisi yoyote:
  (i) iliyoruhusiwa na mwombaji, kwa niaba ya mwombaji; au
  (ii) kwa niaba ya mwombaji endapo idhini ya mwombaji ni vigumu kupatikana.

Kanuni za jumla za huduma ya msaada wa kisheria

**23.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 20(6) na cha 25, ushauri wa kisheria, usaidizi au uwakilishi katika huduma ya msaada wa kisheria hautaathiri uhusiano kati ya haki za wakili na mteja au nafuu au upendeleo unaotokana na uhusiano huo.

Huduma za msaada wa kisheria kutolewa na taasisi

**24**.-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, huduma za msaada wa kisheria zitatolewa na wakili au msaidizi wa kisheria kwa niaba ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria.

(2) Mtu hatatoa huduma za msaada wa kisheria

isipokuwa kama mtu huyo ni wakili au msaidizi wa kisheria aliye chini ya mtoa huduma za msaada wa kisheria.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki anatenda kosa na, akitiwa hatiani, atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Malipo yasiyoruhusiwa

**25.**-(1) Mtoa huduma ya msaada wa kisheria hatadai, kuomba au kupokea malipo kutoka au kwa niaba ya mtu anayesaidiwa kuhusiana na huduma inayotolewa chini ya Sheria hii, isipokuwa kama malipo hayo yameruhusiwa chini ya Sheria hii.

(2) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kutumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(3) Pamoja na adhabu iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) mtu ambaye atakuwa ametiwa hatiani kwa kupokea malipo yasiyoruhusiwa atatakiwa kurejesha kiasi alichopokea.

Kumbukumbu, ufuatiliaji na tathmini

**26.**-(1) Mtoa huduma ya msaada wa kisheria-

(a) atatoa huduma za sheria kwa lengo la kulinda maslahi ya mtu anayesaidiwa; na

(b) atatunza kumbukumbu sahihi za shughuli zilizofanywa kwa niaba ya mtu aliyesaidiwa na kuwasilisha kumbukumbu hizo kwa Msajili kwa mwaka au kadri itakavyoelekezwa na Msajili.

(2) Msajili au msajili msaidizi kwa kadri itakavyokuwa, atafuatilia na kutathmini kazi na ubora wa huduma za kisheria zinazotolewa na mtoa huduma ya msaada wa kisheria chini ya kifungu kidogo cha (1).

*(b) Msaada wa kisheria katika mashauri ya madai*

Msaada wa kisheria katika mashauri ya madai kwa amri ya mahakama

**27**. Pale ambapo katika shauri la madai, Jaji au hakimu anayeendesha shauri ataona kwamba-

(a) kwa maslahi ya haki mtu anatakiwa kupata huduma ya msaada wa kisheria; na

(b) mtu huyo hana uwezo wa kugharamia huduma za

kisheria,

Jaji au hakimu anayeendesha shauri, kadiri itakavyokuwa, ataamuru mtu huyo kupata huduma ya msaada wa kisheria.

Taarifa kwa upande mwingine

**28.**-(1) Pale ambapo mdaawa katika shauri la madai amepewa huduma ya msaada wa kisheria, mtoa huduma ya msaada wa kisheria atatakiwa kutoa taarifa kwa upande mwingine wowote na kwa mahakama, kuhusu suala hilo.

(2) Pale ambapo mtu mwingine yeyote ambaye amekuwa sehemu katika shauri, mtoa huduma ya msaada wa kisheria atatoa taarifa kwa mdaawa mpya.

(3) Pale ambapo mtoa huduma ya msaada wa kisheria anajiondoa katika shauri, mtoa huduma ya msaada wa kisheria atatakiwa kutoa taarifa kwa wadaawa wengine katika shauri na kwa mahakama, kuhusu suala hilo.

Urejeshwaji wa gharama

**29.** Pale ambapo katika shauri lolote tuzo imetolewa kwa mtu anayesaidiwa, mtu huyo atakuwa na haki ya malipo, isipokuwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria anaweza kupunguza kiasi kutoka kwenye tuzo, gharama alizotumia katika kuendesha shauri hilo.

Utekelezaji wa hukumu

**30.** Mtoa huduma ya msaada wa kisheria atachukua hatua muhimu za kutekeleza hukumu au usuluhishi ili kurejesha gharama za shauri.

Gharama dhidi ya mtu aliyesaidiwa

**31.**-(1) Pale ambapo mtu anayesaidiwa atapokea huduma ya msaada wa kisheria katika shauri la madai na akashindwa katika shauri hilo, mahakama haitatoa amri ya tuzo ya gharama dhidi ya mtu aliyesaidiwa isipokuwa tu katika mazingira maalum.

(2) Katika kuamua kama kuna mazingira maalum chini ya kifungu kidogo cha (1), mahakama itazingatia yafuatao kwa mtu aliyesaidiwa-

(a) mwenendo uliosababisha upande mwingine kuingia gharama zisizo za lazima;

(b) kukataa bila sababu kujadiliana, usuluhishi au kushiriki katika njia mbadala ya utatuzi wa mgogoro;

(c) mwenendo wa upotoshaji au udanganyifu; au

(d) mwenendo wowote ambao unakiuka taratibu za mahakama.

(3) Pale ambapo tuzo za gharama zitatolewa dhidi ya mtu aliyesaidiwa, mtoa huduma ya msaada wa kisheria hatawajibika kulipa gharama hizo.

Mtu anayesaidiwa kutotakiwa kutoa dhamana ya gharama ya shauri

**32.** Bila ya kujali masharti ya sheria nyingine yoyote, mtu anayesaidiwa hatatakiwa kuweka dhamana ya gharama ya shauri wakati wa uendeshaji wa shauri au rufaa.

*(c) Msaada wa Kisheria katika Masuala ya Jinai*

Msaada wa kisheria kwa amri ya mahakama

**33.**-(1) Pale ambapo katika shauri lolote la jinai, jaji au hakimu anayeendesha shauri hilo ataona kwamba-

(a) kwa maslahi ya haki mshitakiwa atatakiwa kupata huduma ya msaada wa kisheria katika kuandaa na kuendesha utetezi au rufaa yake kadiri itakavyokuwa; na

(b) hali yake ya kipato haimuwezeshi kupata huduma za kisheria,

Jaji au hakimu anayeendesha shauri, kadri itakavyokuwa, ataidhinisha kuwa mshtakiwa apatiwe huduma ya msaada wa kisheria na mara baada ya kuidhinisha huduma hiyo kwa mshtakiwa, Msajili atateua mtoa huduma ya msaada wa kisheria mwenye wakili kwa ajili ya kuandaa na kuendesha utetezi au rufaa hiyo, kadri itakavyokuwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), endapo katika shauri lolote la jinai mtoto anashtakiwa, Jaji au hakimu atahakikisha mshtakiwa huyo anapata huduma ya msaada wa kisheria na mara baada ya kuridhia msaada huo Msajili atateua mtoa huduma ya msaada wa kisheria mwenye wakili kwa ajili ya kuandaa na kuendesha utetezi au rufaa, kadiri itakavyokuwa.

(3) Jaji Mkuu, kupitia kanuni zitakazochapishwa katika *Gazeti* la Serikali, ataainisha malipo ambayo yanastahili kulipwa wakili aliyeteuliwa kumsaidia mshtakiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2), na malipo hayo yatatoka kwenye Mfuko wa Mahakama.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "Msajili" maana yake ni Msajili wa Mahakama Kuu.

Gharama atakazopata wakili

**34.**-(1) Pale ambapo mtoa huduma ya msaada wa kisheria aliyeteuliwa kusimamia shauri la mshtakiwa chini ya Sheria hii anatumia gharama zaidi kutokana na kutekeleza majukumu yake, anaweza kuwasilisha madai kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

(2) Mtendaji Mkuu wa Mahakama, endapo atajiridhisha kwamba, sehemu au madai yote ni ya msingi, ataidhinisha malipo yote au sehemu ya madai ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria, kadiri itakavyokuwa.

(3) Mgogoro wowote utakaotokana na uamuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama chini ya kifungu kidogo cha (2) unaweza kuwasilishwa kwa Jaji Mkuu, ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

Msaada wa kisheria kwa watoto walio katika vituo vya polisi au magereza

**35.** Pale ambapo afisa wa polisi, afisa wa magereza au mtu mwingine yeyote mwenye jukumu la kusimamia ustawi wa mtoto, katika kutekeleza majukumu yake, anashughulika na mtoto ambaye kama mtuhumiwa au mfungwa, atahakikisha mtoto huyo anapata huduma ya msaada wa kisheria.

Msaada wa kisheria kwa watu walio kizuizini

**36.** Kituo cha polisi au magereza kitaandaa mazingira wezeshi kwa ajili ya utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria kwa washtakiwa na watu walio kizuizini.

SEHEMU YA SITA
MASUALA YA FEDHA

Vyanzo vya mapato ya Bodi

**37.** Fedha za Bodi zitajumuisha-
(a) fedha zozote zitakazotengwa na Bunge;
(b) fedha zozote zitakazopatikana kwa njia ya michango au misaada ya ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(c) kiasi chochote cha fedha au mali ambacho Bodi inaweza kumiliki au kupata kutokana na ada, tozo, misaada au kwa njia nyingine zozote chini ya

Sheria hii au sheria nyingine yoyote ya Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake;

(d) fedha nyingine zozote zinazoweza kukopwa na Bodi kwa ajili yake.

Makadirio ya Mwaka

**38.**-(1) Bodi, kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha itatayarisha makadirio na mapato na matumizi ya mwaka huo.

(2) Makadirio ya mwaka yataainisha makadirio ya matumizi ya Bodi kwa mwaka husika, na Bodi kwa madhumuni hayo itathibitisha matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

(3) Makadirio ya mwaka yatawasilishwa kwa Waziri ambaye atayawasilisha Bungeni ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwake.

Taarifa ya utekelezaji ya mwaka

**39.** Msajili, ndani ya miezi mitatu ataandaa na kuwasilisha kwa waziri, taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya Bodi kwa kipindi cha mwaka wa fedha na Waziri atawasilisha nakala ya taarifa hiyo Bungeni.

Vitabu vya hesabu

**40.**-(1) Bodi itatunza vitabu sahihi vya hesabu.

(2) Ndani ya miezi mitatu tangu kumalizika kwa kila mwaka wa fedha, Bodi itawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa ya hesabu za Bodi pamoja na:

(a) taarifa ya shughuli za fedha na mapato na maptumizi katika kipindi hicho cha mwaka wa fedha; na

(b) taarifa ya mali na madeni ya Bodi yaliyopo mwishoni mwa mwaka wa fedha husika.

(3) Akaunti za Bodi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI MENGINEYO

Msajili anaweza kuhitaji uthibitisho wa uwepo wa mtoa huduma

**41.**-(1) Pale ambapo Msajili atakuwa na sababu za kutilia shaka kuwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria hayupo au hatoi tena huduma ya msaada wa kisheria anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa mmiliki wa ofisi ya mtoa huduma ya msaada wa kisheria au kuchapisha taarifa katika gazeti linalosambazwa kwa wingi Tanzania Bara, ikimtaka kuwasilisha kwa Msajili uthibitisho wa uwepo wake ndani ya kipindi cha siku thelathini.

(2) Pale ambapo mtoa huduma ya msaada wa kisheria atashindwa kuwasilisha uthibitisho wa uwepo wake kwa Msajili, Msajili atafuta cheti cha usajili na kuliondoa jina lake kwenye Rejesta.

Wajibu kuhusiana na maadili ya kitaaluma

**42**.-(1) Wakili anayetoa msaada wa kisheria chini ya Sheria hii atatakiwa kuzingatia kanuni au miiko ya maadili ya kitaaluma ya chombo kilichomsajili na haki, wajibu wa majukumu yake kama mwanachama wa chombo hicho kwa namna yoyote hayataathiriwa na masharti ya Sheria hii.

(2) Waziri, kupitia *Gazeti* la Serikali, atatunga kanuni za miiko ya maadili kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria.

(3) Kanuni za miiko ya maadili zilizotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) zitaainisha-

(a) ulinzi wa haki na maslahi ya mtu anayesaidiwa;
(b) wajibu kwa mtu anayesaidiwa, Msajili na mahakama;
(c) mgongano wa maslahi;
(d) uzingatiaji wa usiri;
(e) kwa wanataaluma, wajibu wa kuzingatia viwango vya miiko ya maadili vilivyowekwa na vyombo vyao vya kitaaluma;
(f) usahihi na mienendo ya kimaadili; na
(g) masuala mengine yoyote yanayohusiana na hayo.

Katazo kuhusu shughuli za kisiasa

**43**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya sheria hii, mtoa huduma ya kisheria, wakili au msaidizi wa kisheria hatajihusisha na shughuli yoyote ya kisiasa.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi

shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili.

Matumizi mabaya ya fedha za msaada wa kisheria

**44**.-(1) Kila mtoa huduma ya msaada wa kisheria, au mtu yeyote aliyepokea fedha au msaada wowote kwa madhumuni ya kutoa msaada wa kisheria chini ya sheria hii, atahakikisha kuwa fedha au msaada huo aliopokea unatumika kwa ajili kutoa msaada wa kisheria chini ya sheria hii.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi lakini isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au kutumikia kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja.

Makosa ya jumla

**45.** Mtu ambaye-

(a) kwa udanganyifu, atasababisha au kuruhusu kuingizwa kwa taarifa yoyote ya uongo au isiyo sahihi katika Rejesta au nakala yake yoyote;
(b) atatoa msaada wa kisheria bila ya kuwa na sifa zilizoainishwa chini ya Sheria hii;
(c) anayetoa taarifa ya uongo au kupotosha kwa nia ya kupata nafuu, faida au manufaa chini ya Sheria hii;
(d) anayejifanya amesajiliwa au anajionesha kuwa amesajiliwa chini ya Sheria hii;
(e) anakataa au anashindwa pasipo sababu za msingi kutokea baada ya kupokea wito wa kuitwa katika shauri na Msajili chini ya sheria hii; na
(f) anamzuia au kumkwamisha mjumbe wa Bodi au Msajili au mtu mwingine yeyote katika kutekeleza mamlaka au majukumu yake chini ya Sheria hii;
(g) anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Kutangazwa kwa watoa

**46.** Msajili, kila baada ya miezi kumi na mbili, atatangaza kupitia *Gazeti* la Serikali, magazeti

huduma ya msaada wa kisheria

yanayosambazwa kwa wingi Tanzania Bara na njia nyingine yoyote ya mawasiliano, majina ya watoa huduma ya msaada wa kisheria waliosajiliwa na watoa huduma ya msaada wa kisheria waliofutiwa usajili.

Mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni

**47.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa lengo la utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii zitaainisha-

(a) utaratibu wa utoaji huduma ya msaada wa kisheria kwa watu wanaoshikiliwa katika vituo vya polisi, rumande, magereza au wanaozuiliwa kisheria katika sehemu nyingine;
(b) taratibu, vigezo na masharti ya usajili wa watoa huduma na wasaidizi wa sheria;
(c) taratibu za ukaguzi kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria;
(d) ada zitakazolipwa chini ya Sheria hii;
(e) taratibu za kushughulikia migogoro na malalamiko chini ya Sheria hii;
(f) kumbukumbu zitakazohifadhiwa na watoa huduma za msaada wa kisheria kuhusiana na huduma ya msaada wa kisheria na taarifa zitakazowasilishwa kwa Msajili;
(g) kiasi kitakacholipwa na mtu aliyesaidiwa;
(h) taratibu za rufaa chini ya Sheria hii; na
(i) masuala mengine yoyote yatakayopaswa kuainishwa chini ya Sheria hii.

Kufutwa Sheria ya Msaada wa Kisheria Sura ya 21

**48.**-(1) Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), amri, kanuni, miongozo, maelekezo na kanuni zote zilizotolewa chini ya Sheria iliyofutwa zitaendelea kutumika hadi sheria ndogo nyingine zitakapotengenezwa chini ya Sheria hii.

Taratibu za mpito

**49.**-(1) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, taratibu zote za huduma ya msaada wa kisheria zilizopo hadi tarehe ya

kuanza kutumika kwa Sheria hii zitaendelea na kukamilishwa kama vile Sheria hii haijapitishwa.

(2) Taasisi zote zinazotoa huduma za msaada wa kisheria zitaendelea kutoa huduma mpaka itakapoisha miezi kumi na mbili kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo zitasitisha kutoa huduma na kuhitajika kujisajili kwa mujibu wa Shera hii.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 4(2))*

## MUUNDO, MUHULA NA UTARATIBU WA BODI

Muundo

**1**.-(1) Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria itaundwa na Mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine saba watakaoteuliwa na Waziri kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti ambaye atakuwa Jaji wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Waziri kwa kushauriana na Jaji Mkuu;

(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake mwenye cheo cha ngazi si chini ya Afisa wa Sheria;

(c) mwakilishi kutoka taasisi za watoa huduma ya msaada wa kisheria;

(d) Kamishna wa Ustawi wa Jamii au mwakilisha wake;

(e) Inspekta Jenerali wa Polisi au mwakilishi wake mwenye cheo si chini ya ngazi ya Kamishna wa Polisi;

(f) Kamishna Jenerali wa Magereza au mwakilishi wake mwenye cheo si chini ya ngazi ya Kamishna wa Magereza;

(g) Mkurugenzi wa Sheria kutoka wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa;

(h) mwakilishi wa watu wenye ulemavu; na

(i) mwakilishi kutoka taasisi zinazowakilisha wasaidizi wa kisheria.

(2) Mamlaka ya uteuzi katika kuteua wajumbe chini ya aya ya (1) itahakikisha kuwa kuna uwakilishi wa kijinsia katika Bodi.

(3) Bodi inaweza kualika idadi ya watu kuwasilisha maslahi yoyote kama itakavyoona inafaa, isipokuwa mtu aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Makamu Mwenyekiti

**2.** Wajumbe watamchagua mmoja miongoni mwa idadi yao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi, na mjumbe yeyote aliyechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti, anaweza kwa mujibu nafasi yake kama Makamu Mwenyekiti kushikilia ofisi kwa kipindi cha miaka mitatu tangu tarehe ya kuchaguliwa kwake.

Muda wa kuwa madarakani

**3.**-(1) Wajumbe wa Bodi watakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu na watakuwa na sifa za kuteuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(2) Mjumbe wa bodi anaweza kwa wakati wowote kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Waziri, kuanzia tarehe aliyotoa taarifa au kama hakuna tarehe iliyotajwa, kuanzia tarehe ya kupokelewa taarifa hiyo, Mjumbe huyo atakoma kuwa mjumbe.

Ujazaji wa nafasi iliyo wazi

**4.** Pale ambapo mjumbe yeyote atakoma kuwa mjumbe kwa sababu yoyote kabla ya kumalizika kwa muda wake, Mamlaka ya uteuzi inaweza kumteua mtu mwingine katika nafasi yake na atakayeteuliwa atashika madaraka kwa kipindi kilichosalia cha mtangulizi wake.

Vikao vya Bodi

**5.**-(1) Bodi itakutana kwa shunguli zake za kawaida kwa wakati na mahali itakapoamua, lakini itakutana angalau mara moja katika kila miezi mitatu.

(2) Mwenyekiti au asipokuwepo, Makamu mwenyekiti, ataongoza kila mkutano wa Bodi na kama wote Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawatakuwepo, wajumbe waliopo watamteua mmoja miongoni mwao kuongoza mkutano huo.

(3) Mwenyekiti au asipokuwepo, Makamu Mwenyekiti anaweza kwa muda wowote anaweza kuitisha mkutano maaalum waBodi kujadili Suala lolote ambalo anaona ni la dharura

(4) Mwenyekiti au asipokuwepo, Makamu Mwenyekiti anaweza kumualika mtu yeyote ambaye siyo mjumbe katika majadiliano katika mkutano wowote wa Bodi , lakini mtu huyo aliye alikwa hataruhusiwa kupiga kura.

Akidi

**6.** Katika mkutano wowote wa Bodi Akidi ya mkutano itatakiwa kuwa na angalau wajumbe watatu.

Uamuzi wa Bodi

**7.-**(1) Masuala yaliyopendekezwa wakati wa mkutano wa Bodi yataamuliwa kwa uwingi wa kura za wajumbe wa Bodi waliohudhuria na kupiga kura na ikitokea usawa wa kura mtu anayeongoza mkutano atakuwa na kura ya uamuzi wa pili ili kuondoa usawa katika kura za awali.

(2) Uaamuzi unaweza kufanywa na Bodi bila mkutano kwa kusambaza karatasi au nyaraka husika miongoni mwa wajumbe, na maoni ya wajumbe waliowengi yaliyo katika maandishi yataheshimika lakini mjumbe yeyote anaweza akaomba maamuzi hayo yaahirishwe na suala hilo lijadiliwe kwenye Mkutano wa Bodi.

Kumbukumbu za Vikao

**8.**-(1) Bodi itaandika, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za shughuli zilizofanywa katika vikao, na kumbukumbu za kila mkutano wa Bodi zitasomwa na kuthibitishwa, au kurekebishwa na kuthibitishwa kwenye kikao kijacho cha Bodi na kusainiwa na mtu aliyeongoza kikao hicho.

(2) Kumbukumbu zozote zitakazosainiwa na mtu atakayekuwa anaongoza mkutano wa Bodi, baada ya kuthibitishwa kuwa hazina makosa, zitachukuliwa kuwa ndiyo kumbukumbu sahihi za mkutano.

Nafasi wazi kutobatilisha mwenendo

**9.** Uhalali wa kitendo chochote au uendeshaji wa Bodi hautaathiriwa na nafasi yoyote ya mjumbe iliyoachwa wazi miongoni mwa wajumbe au kasoro za uteuzi wa

yeyote kati yao.

Amri na maelekezo ya Bodi

**10.** Amri, maelekezo, taarifa au nyaraka zote zilizoandaliwa au kutolewa kwa niaba ya Bodi zitasainiwa na-

(a) Mwenyekiti au Makamu wa Bodi, kwa vyovyote itakavyo kuwa; au

(b) Katibu.

Maslahi ya wajumbe wa Bodi

**11.** Mjumbe wa Bodi atastahili kulipwa ujira,ada au posho za gharama kama Waziri, baada ya kushauriana na Bodi, atakavyokuwa anaelekeza mara kwa mara.

Bodi kujiwekea kanuni zake

**12.** Kwa kuzingatia vifungu vya Jedwali hili, Bodi inaweza kujiwekea kanuni za kuendesha vikao vyake.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unakusudiwa kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2016. Sheria inayopendekezwa ina madhumuni ya kuanzisha mfumo wa kisheria wa kutoa, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa mashauri ya jinai na madai kwa watu wasiyo na uwezo wa kumudu gharama za huduma za kisheria kwa malipo. Aidha, awali Serikali imekuwa ikitoa huduma ya msaada wa kisheria kwa watuhumiwa wanaoshtakiwa kwa makosa makubwa tu kama vile mauaji, kuua bila kukusudia na uhaini. Huduma hiyo imekuwa ikitolewa na Mahakama Kuu pekee. Asasi mbalimbali za kiraia zimekuwa zikitoa baadhi ya huduma za kisheria kuanzia ushauri wa kisheria na uwakilishi mahakamani. Kazi hii inafanywa pasipokuwa na uratibu baina ya taasisi hizo na Serikali. Utaratibu unaotumiwa na asasi za kiraia kwa kiasi kikubwa unategemea wafadhili ambao si wa kudumu na una matokeo ya muda mfupi.

Kutokana na ongezeko la mahitaji, idadi ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria Serikali imelazimika kuanzisha mfumo huu ili kuboresha huduma hiyo kuwasimamia na kuwaratibu.

Kwa mantiki hiyo, Muswada huu unalenga kuweka mfumo madhubuti na endelevu ambao utaziba ombwe lililopo na kutoa suluhisho la changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa huduma ya msaada wa kisheria nchini inaleta matokeo chanya kwa ustawi wa wananchi, hususani, wa vijijini na wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu na Saba.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inajumuisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa, matumizi na tafsiri ya misamiati na maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada unaopendekezwa.

Sehemu ya Pili inaweka masharti ya usimamizi na uratibu wa watoa huduma ya msaada wa kisheria. Inaanzisha Bodi ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheira na kuainisha majukumu yake. Vilevile, inaweka utaratibu wa uteuzi wa Msajili na majukumu yake.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti ya usajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria, inaainisha sifa za kusajiliwa kama mtoa huduma ya

msaada wa kisheria, utoaji wa cheti cha usajili mara baada ya kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, mazingira yatakayopelekea kusitishwa au kufutwa kwa cheti cha usajili. Aidha, Sehemu hii pia inaainisha haki ya rufaa dhidi ya uamuzi wa kusitishwa au kuftwa kwa cheti. Vilevile, inaweka masharti ya uteuzi wa Msajili Msaidizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Sehemu ya Nne inaainisha masharti mahsusi kwa wasaidizi wa kisheria, sifa, majukumu na masharti ya wasaidizi wa kisheria kutoa ushauri na usaidizi wa kisheria kwa mujibu wa masharti ya Muswada unaopendekezwa. Aidha, inaweka katazo kwa wasaidizi wa kisheria kutoza ada kwa mtu anayesaidiwa na kujihusisha na shughuli zilizotengwa kwa ajili ya mawakili.

Sehemu ya Tano ya Muswada inaainisha masharti ya mtu anayeweza kuomba huduma ya msaada wa kisheria, masharti ya jumla ya huduma ya msaada wa kisheria, huduma ya msaada wa kisheria katika mashauri ya madai na jinai kwa amri ya mahakama. Aidha, Sehemu hii inatoa masharti ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto na watu walio katika vituo vya polisi, magereza na vizuizi mbalimbali.

Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu masharti ya fedha. Masharti hayo yanajumuisha vyanzo vya mapato ya Bodi, makadirio ya mwaka na vitabu vya hesabu. Vilevile, inaainisha mamlaka ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua hesabu za Bodi.

Sehemu ya Saba inaainisha masharti mengineyo. Masharti hayo yanajumuisha mamlaka ya Msajili kutoa tangazo kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria kuthibisha uwepo wake, wajibu kuhusiana na miiko ya maadili ya kitaaluma kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria na mamlaka ya Waziri kutunga kanuni na kanuni za maadili ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria. Vilevile, sehemu hii inaainisha masharti ya kuifuta Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai, Sura ya 21 na kuainisha Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito.

| | |
|---|---|
| Dar es Salaam, | **HARRISON G. MWAKYEMBE** |
| 2 Agosti, 2016 | *Waziri wa Katiba na Sheria* |

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Karibu.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kabisa kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anatuwezesha kila jambo na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajalia Wabunge wetu wapya leo kuweza kuapa hapa akiwemo Mwenyekiti wangu wa Taifa Umoja wa Wazazi Tanzania, Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria, Na. 14 wa mwaka 2016 *(The Legal Aid Act, (No.14) Act of 2016)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya utoaji msaada wa kisheria siyo dhana ngeni katika mizania ya sheria na utoaji haki hapa Tanzania na nchi nyingine. Nchi nyingi hapa Afrika kama vile Kenya, Uganda na Afrika Kusini tayari wana hii sheria. Kwa nchi ya Kenya sheria hii ilitungwa mwaka 2012 na inaitwa *Legal Aid Act, No. 6 of* 2012. Kwa nchi ya Afrika Kusini sheria ilitungwa mwaka 2014, inaitwa *Legal Aid Act, No. 39 of* 2014. Australia sheria hii ilitungwa mwaka 1977 na inaitwa *Legal Services Commission Act,* ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana hii ina msingi wa kikatiba katika Ibara ya 13(1) – (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inatoa Haki mbalimbali za Raia katika vyombo vya utoaji haki zilizojengwa katika misingi ya usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza kabisa katika utendaji wake Kamati iliona ni vema kuishirikisha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa ajili ya kutoa maoni yao kwenye Muswada huu. Tarehe 24/01/2017 Kamati ilipokea maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoka kwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye alitoa mchango mkubwa katika uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati itaendelea kutoa nafasi hii kila mara kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika uchambuzi wa Miswada ili kuongeza tija katika uchambuzi wa Miswada na kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na madhumuni ya Muswada ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2016. Sheria inayopendekezwa ina madhumuni ya kuanzisha Mfumo wa Kisheria wa kutoa, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya Msaada wa Kisheria kwa mashauri ya jinai na madai kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za huduma za kisheria kwa malipo. Awali Serikali imekuwa ikitoa huduma ya msaada wa kisheria kwa watuhumiwa wanaoshitakiwa kwa makosa makubwa tu kama vile mauaji, kuua bila kukusudia na uhaini. Huduma hiyo imekuwa ikitolewa na Mahakama Kuu pekee.

Aidha, Asasi mbalimbali za Kiraia zimekuwa zikitoa baadhi ya huduma za kisheria kuanzia ushauri wa kisheria na uwakilishi Mahakamani. Kazi hii inafanywa pasipokuwa na uratibu baina ya Taasisi hizo na Serikali. Utaratibu unaotumiwa na Asasi za Kiraia kwa kiasi kikubwa unategemea wafadhili ambao siyo wa kudumu na una matokeo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la mahitaji ya idadi ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria, Serikali imeona umuhimu wa kuanzisha mfumo huu ili kuboresha huduma hiyo katika usimamizi na uratibu. Kwa mantiki hiyo, Muswada huu unalenga kuweka Mfumo madhubuti na endelevu ambao utaziba ombwe lililopo na kutoa suluhisho la changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa huduma ya msaada wa kisheria nchini inaleta matokeo chanya kwa ustawi wa wananchi, hususan wa vijijini na wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inajumuisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa, matumizi na tafsiri ya misamiati na maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada unaopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inaweka masharti ya usimamizi na uratibu wa watoa huduma ya msaada wa kisheria. Inaanzisha Bodi ya

Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria na kuainisha majukumu yake. Vilevile, inaweka utaratibu wa uteuzi wa msajili na majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti ya usajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria; inaainisha sifa za kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, utoaji wa cheti cha usajili mara baada ya kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, mazingira yatakayopelekea kusitishwa au kufutwa kwa cheti cha usajili. Aidha, Sehemu hii pia inaainisha haki ya rufaa dhidi ya uamuzi wa kusitishwa au kufutwa kwa cheti. Vilevile, inaweka masharti ya uteuzi wa Msajili Msaidizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inaainisha masharti mahsusi kwa Wasaidizi wa Kisheria; sifa, majukumu na masharti ya wasaidizi wa kisheria kutoa ushauri na usaidizi wa kisheria kwa mujibu wa masharti ya Muswada unaopendekezwa. Aidha, inaweka katazo kwa wasaidizi wa kisheria kutoza ada kwa mtu anayesaidiwa na kujihusisha na shughuli zilizotengwa kwa ajili ya Mawakili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inaainisha masharti ya mtu anayeweza kuomba huduma ya msaada wa kisheria, masharti ya jumla ya huduma ya msaada wa kisheria, huduma ya msaada wa kisheria katika mashauri ya madai na jinai kwa amri ya Mahakama. Aidha, sehemu hii inatoa masharti ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto na watu walio katika Vituo vya Polisi, Magereza na vizuizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu masharti ya fedha. Masharti hayo yanajumuisha vyanzo vya mapato ya Bodi, makadirio ya mwaka na vitabu vya hesabu. Vilevile, inaainisha mamlaka ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua hesabu za bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba inaainisha masharti mengineyo. Masharti hayo yanajumuisha mamlaka ya msajili kutoa tangazo kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria kuthibisha uwepo wake, wajibu kuhusiana na miiko na maadili ya kitaaluma kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni za Maadili ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria. Vilevile, sehemu hii inaainisha masharti ya kuifuta Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai, Sura ya 21 na kuainisha masharti yatokanayo na masharti ya mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa jumla wa Muswada. Kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na Sekretariati ya Kamati, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa sheria kwa kupitia vifungu vyote 49 vya Muswada tarehe 17/1/2017 na kujiridhisha na malengo na madhumuni ya sheria inayotungwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria tarehe 18/1/2017 ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu malengo na madhumuni ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 tarehe 19 na 20 Januari 2017, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Taasisi za Elimu ya Juu, vikundi vya wakulima, asasi za kiraia na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili kusikiliza na kupokea maoni yao kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa kitaalamu wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea maoni mbalimbali ya Wadau kwa muda wa siku mbili mfululizo, Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Maoni ya wadau kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kufanya uchambuzi wa Muswada na hatimaye kutoa maoni Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 25 Januari, 2017 Kamati ilikutana na mtoa hoja, Waziri wa Katiba na Sheria na kumpa nafasi kujibu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi uliofanyika. Yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Serikali ilikubali kuchukua mapendekezo ya Kamati. Yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wadau waliochangia katika Muswada huu wamekubaliana na malengo na madhumuni ya Muswada na kuipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuweka mfumo rasmi wa kisheria wa kuwatambua watoaji huduma ya msaada wa kisheria Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kupitia kifungu kwa kifungu na baada ya kupokea na kuchambua nia na malengo ya Muswada huu, Kamati iliona kwamba kwa maslahi ya Sekta ya utoaji huduma za msaada wa Kisheria Tanzania kuna haja

ya kuvifanyia maboresho vifungu 15 vya Muswada huu kwa kutazama mazingira tuliyonayo hapa Tanzania na kwa kutazama pia Sheria za namna hii zilivyo katika nchi nyingine *(International Comparative Perspective).*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vifungu vilikuwa na makosa ya kiuchapaji na kisarufi na tayari vimeingizwa katika jedwali la marekebisho la Serikali. Kwa mfano, katika Ibara ya 4 (1) ya Muswada, sentensi *"There shall is established"* ina makosa ya kisarufi na kiuchapishaji na Kamati imeshauri isomeke *"There shall be established."* Katika Ibara ya 48 (2) ya Muswada, sentensi inayosomeka "*made under the repeal Act*" ina makosa ya Kisarufi na Kamati imeshauri isomeke *"made under the repealed Act."*

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa kama haya yameonekana katika vifungu mbalimbali vya Muswada na Serikali imeyapokea mapendekezo ya Kamati na kuyajumuisha katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu ambavyo vilihitaji kuboreshwa zaidi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha (3) kuhusu tafsiri, Kifungu cha (5) kuhusu kazi za bodi, Kifungu cha (6) kuhusu Msajili wa Utoaji wa Msaada wa Kisheria na Kifungu cha (8) kuhusu uteuzi wa Wasajili wasaidizi. Maboresho pia yalifanyika katika vifungu vinavyohusu sifa za usajili wa mtoa huduma ya Msaada wa Kisheria (Ibara ya 10), kusitishwa na kufutwa kwa Cheti cha Usajili (Ibara ya 16), utaratibu wa kusitishwa na kufutwa kwa cheti (Ibara ya 16), usimamizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria (Ibara ya 18), sifa za wasaidizi wa sheria (Ibara ya 19), urejeshwaji wa gharama (Ibara ya 29), msaada wa kisheria kwa watoto walio katika Vituo vya Polisi au Magereza (Ibara ya 35), katazo kuhusu shughuli za kisiasa (Ibara ya 43), taratibu za mpito ( Ibara ya 49), muundo na Wajumbe wa Bodi pamoja na masuala ya jumla ya muundo na dhima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, pande zote mbili zilikubaliana kufanya marekebisho kwa ajili ya kuboresha vifungu vyote vilivyokuwa na utata ili viwe bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati katika Muswada huu yamezingatia uchambuzi wa kitaalamu wa Muswada huu uliofanywa na Kamati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha (3) cha tafasiri, kuwe na tafasiri ya neno "*Advocate*" ili tafasiri hii iendane na tafasiri iliyomo katika Kifungu cha (4) cha Sheria ya Tafsiri, Sura ya Kwanza ya Sheria za Tanzania. Katika kifungu hiki, Kamati pia inashauri kutolewa kwa tafasiri ya maneno "*Legal Advice and Assistance*" ambayo yameunganishwa. Kamati inashauri maneno haya yatenganishwe na kupatiwa tafsiri zinazojitegemea maana ni maneno yanayojitegemea na yenye maana tofauti katika fani ya Sheria. Kamati inashauri pia kwamba maana ya "*Legal Aid Services*" yaani huduma za msaada wa kisheria kama ilivyoandikwa kwenye Muswada, ipewe maana kubwa zaidi na kujumuisha utoaji wa elimu, taarifa na uwakilishi wa kisheria ili kuendana na dhima ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha (3) Kamati inashauri Neno "*Lawyer*" lipewe tafasiri na neno "*Paralegal*" pia lipewe tafasiri sahihi ili kuendana na maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 6 (2) Kamati inashauri neno "*The Director*" liondolewe na badala yake litumike neno "*the person*" ili kupanua wigo wa uteuzi wa Msajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kutoka kwa mtu mmoja na kwenda kwa mtu mwingine yeyote katika Watumishi wa Umma ndani au nje ya Wizara ambaye ana sifa ya kuwa Msajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Sheria Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 7 (1) Kamati inashauri kwamba Msajili ashirikiane na Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria na Vyuo vinavyotoa elimu ya utoaji msaada wa sheria, kuandaa mitaala ya mafunzo ya utoaji huduma ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sifa za usajili wa mtoa huduma ya msaada wa kisheria katika Kifungu cha 10, Kamati inashauri kwamba uongezwe wigo wa watu wenye taaluma ya sheria kwa taasisi hiyo kwa kumwongeza Mwanasheria ambaye sio Wakili wa Mahakama Kuu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muda wa kushughulikia maombi ya usajili, Kamati ilipendekeza kuwa badala ya siku 30 zinazopendekezwa kwenye Muswada, ziwe siku 14. Baada ya majadiliano na Serikali, imeonekana iwe siku 21 ili kuleta ufanisi wa kushughulikia maombi kwa pande zote mbili, yaani Serikali na waombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 13 Kamati inapendekeza kwamba notisi ya kukataliwa kusajiliwa kwa mwombaji itolewe ndani ya siku saba baada ya maombi kufanyika. Baada ya majadiliano na Serikali, imependekezwa kwamba notisi ya kukataliwa itolewe baada ya siku 14 ambazo ni utaratibu wa kawaida wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 14 (2) kuhusu rufaa, kamati inapendekeza kwamba Sheria iweke wazi haki ya rufaa kwa mwombaji kama hajaridhishwa na maamuzi ya Msajili na haki hii iwe ni ya kukata rufaa Mahakama Kuu. Kamati inatambua kwamba kukiwa na kifungu kinachosema hivyo *(express provision)* haki itakuwa na nguvu zaidi kuliko kifungu kukaa kimya na kutegemea utaratibu wa mapitio ya Kimahakama, yaani *(Judicial Review)* ambao upo katika misingi ya asili ya utoaji haki *(principles of natural justice)*. Kamati inasisitiza kwamba haki hii ni ya kikatiba na ni vema ikasemwa wazi wazi katika Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16 cha Muswada huu ni moja kati ya vifungu vilivyohitaji majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali. Kifungu hiki kinahusiana na kusitishwa na kufutwa kwa Cheti cha Usajili cha Mtoa huduma wa Msaada wa Kisheria. Baada ya majadiliano na Serikali Kamati inashauri kwamba kabla Cheti cha Mtoa huduma wa Msaada wa Kisheria hakijasimamishwa au kufutwa, Mtoa Huduma wa Msaada wa Kisheria apewe muda wa kutosha wa kushughulikia hilo tatizo na kutoa taarifa kwa Msajili kuhusu hatua alizochukua pale ambapo mwajiriwa wake amefanya makosa ambayo yanaweza kusababisha Mtoa Huduma za Msaada wa Kisheria asitishiwe au kufutiwa usajili moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 16 (1) (f) na Kifungu cha 43 (1) Kamati inashauri neno "*political activities*" yaani shughuli za kisiasa, lipatiwe tafsiri ili kuondoa utata wa maana yake na wigo *(scope)* wa matumizi yake wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 19 kuhusu sifa za wasaidizi wa sheria, Kamati inashauri Sheria iwatambue wasaidizi wa kisheria wenye elimu ya sekondari na wale ambao wamekuwa wanafanya kazi ya usaidizi wa kisheria kwa angalau miaka miwili huku wakiwa na sifa za msingi za kufahamu kusoma na kuandika na wamepokea mafunzo maalumu ya utoaji msaada wa kisheria. Hii itatanua wigo wa kuwa na wasaidizi wengi wa kisheria hasa maeneo ya Vijijini ambapo ni ngumu kuwa na hata wahitimu wa Kidato cha Nne. Kamati pia inashauri vifungu vya 20 (c) na (f) vifutwe kwa sababu

haviendani kikamilifu na majukumu yanayotambulika ya watoa huduma ya msaada wa sheria. Kamati inashauri urasimu wa kutuma maombi ya huduma ya msaada wa kisheria uondolewe katika Kifungu cha 21 (1) na (2), badala yake wenye wahitaji wa msaada wa kisheria waende moja kwa moja kwa mtoa huduma na kupeleka maombi ya kupata msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 27 kuhusu msaada wa sheria, katika mashauri ya madai kwa amri ya Mahakama, Kamati inashauri kuongeza wigo wa Kimahakama kwa kuongeza Mabaraza ya Ardhi, kodi, kazi na taasisi nyingine za utoaji na usimamizi wa haki ili kuongeza wigo wa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 29 kuhusu urejeshwaji wa gharama, Kamati inashauri kwamba mtoa huduma ya msaada wa kisheria awe na haki ya kupokea sehemu ya tuzo ya Mahakama ili kufidia gharama mbalimbali za kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 36 kuhusu msaada wa sheria kuhusu watu walio kizuizini, Kamati inashauri Jeshi la Polisi au Magereza kuweka mazingira mazuri kwa watu walio na uhitaji wa huduma ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 49 kuhusu taratibu za mpito, Kamati inashauri taasisi zote ambazo tayari zinatoa huduma za msaada wa kisheria zitachukuliwa kuwa tayari zimeshasajiliwa na zitapewa Cheti cha Usajili kwa mujibu wa taratibu za sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muundo wa Bodi ya Taifa ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria, Kamati inashauri aongezwe Mjumbe kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika, *(Tanganyika Law Society)* na Mjumbe kutoka Jukwaa la Taifa la Haki za Jinai *(National Criminal Justice Forum)* na kuwatoa katika bodi Inspekta Jenerali wa Polisi na Kamishna Jenerali wa Magereza au wawakilishi wao. Kamati inaamini kwamba uwakilishi wa *TLS* na mtu kutoka Jukwaa la Taifa la Jinai utaleta tija katika bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuzingatia suala la jinsia katika muundo wa bodi hii. Hii itasaidia kujenga uwezo wa wanawake katika nafasi za uongozi na usimamizi bora wa utekelezaji wa sheria hii kwa kutazama suala la utoaji msaada wa kisheria kwa jicho la kutazama makundi maalumu katika jamii ambayo yanahitaji jicho la haki za binadamu; kwa mfano wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeyakubali mapendekezo mengi ya Kamati na kuyaweka katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa katika Bunge hili. Serikali pia imetoa maelezo ya ziada na ufafanuzi katika maeneo ya Muswada ambayo Kamati ilihitaji ufafanuzi. Kamati inaamini kwamba uchambuzi wa kitaalamu uliofanywa katika Muswada huu utasaidia kupatikana kwa sheria bora ya kusimamia sekta ya utoaji huduma za kisheria nchini na kufungua ukurasa mpya kwa watoa msaada wa kisheria Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipa kibali cha kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Harrison G. Mwakyembe, kwa ushirikiano wake wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu ambao kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Kamati. Naomba kutambua mchango wa wadau wafuatao:-

Chama cha Mawakili wa Tanganyika, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania, Mtandao wa Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria Tanzania, Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania, Jumuiya ya Wakristo Tanzania, Sekretarieti ya Msaada wa Sheria, Chuo Kikuu Dodoma, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Chuo cha Biashara, Tawi la Dodoma na Taasisi ya Uwezeshaji wa Msaada wa Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa kutoka Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha Muswada huu. Kwa vile bado muda, naomba niwataje; wa kwanza ni Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa ambaye ni Mwenyekiti na mimi mwenyewe Najma Murtaza Giga, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Juma Hamad Kombo, Mheshimiwa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Giga, majina tafadhali, naomba umalize hotuba.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, niliona muda ninao. Kwa hiyo, namalizia kwa kusema kwamba mwisho kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji wa kazi za Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi ndugu Angelina Sanga, Mkurugenzi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Pius Mboya; Wakurugenzi Wasaidizi ndugu Mossy Lukuvi na ndugu Prudence Rweyongeza; Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni ndugu Stella Bwimbo na ndugu Dunford Mpelumbe; Wanasheria wa Bunge ndugu Stephano Mbutu, ndugu Evelyne Shibandiko, ndugu Rehema Kipera na Msaidizi wa Kamati ndugu Rachel Masima kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa weledi mkubwa na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Giga.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MSAADA WA SHERIA, (NA. 14) WA MWAKA 2016, (THE *LEGAL AID ACT, NO. 14 OF 2016)* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria, Na. 14 wa Mwaka 2016 (The Legal Aid Act, (No.14) Act of 2016).

**1.2 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu Mwezi Novemba, 2016 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 10 Novemba 2016 ili iufanyie kazi, na tarehe 18 Januari, 2017, Waziri wa Katiba na Sheria alifika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu malengo na Madhumuni ya Muswada huu.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, dhana ya utoaji Msaada wa Kisheria siyo dhana ngeni katika mizania ya Sheria na Utoaji Haki hapa Tanzania na nchi nyingine. Nchi nyingi hapa Afrika kama vile Kenya, Uganda na Afrika Kusini tayari wana hii Sheria. Kwa nchi ya Kenya Sheria hii ilitungwa Mwaka 2012 na inaitwa Legal Aid Act, No. 6 ya Mwaka 2012. Kwa nchi ya Afrika Kusini Sheria ilitungwa Mwaka 2014, inaitwa Legal Aid Act, No. 39 ya Mwaka 2014. Australia Sheria hii ilitungwa Mwaka 1977 na inaitwa Legal Services Commission Act, ya Mwaka 1977.

Dhana hii ina msingi wa Kikatiba katika Ibara ya 13(1-6) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977 ambayo inatoa Haki mbalimbali za Raia katika vyombo vya utoaji haki zilizojengwa katika misingi ya usawa.

**1.4 Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**1.5 Mheshimiwa Spika**, kwa mara ya kwanza kabisa katika utendaji wake Kamati iliona ni vema kuishirikisha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa ajili ya kutoa maoni yao kwenye Muswada huu. Tarehe 24/01/2017 Kamati ilipokea maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoka kwa Mnadhimu wa KambiRasmi ya Upinzani Bungeni Mhe.Tundu Lissu ambaye alitoa mchango mkubwa katika Uchambuzi wa Muswada. Kamati itaendelea kutoa nafasi hii kila mara kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Uchambuzi wa Miswada ili kuongeza tija katika Uchambuzi wa Miswada na kuishauri Serikali ipasavyo.

## 2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unakusudia kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2016. Sheria inayopendekezwa ina madhumuni ya kuanzisha Mfumo wa Kisheria wa kutoa, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya Msaada wa Kisheria kwa mashauri ya jinai na madai kwa watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za huduma za kisheria kwa malipo. Awali Serikali imekuwa ikitoa huduma ya msaada wa kisheria kwa watuhumiwa wanaoshtakiwa kwa makosa makubwa tu kama vile mauaji, kuua bila kukusudia na uhaini. Huduma hiyo imekuwa ikitolewa na Mahakama Kuu pekee.

Aidha, Asasi mbalimbali za Kiraia zimekuwa zikitoa baadhi ya huduma za kisheria kuanzia ushauri wa kisheria na uwakilishi Mahakamani. Kazi hii inafanywa pasipokuwa na uratibu baina ya Taasisi hizo na Serikali. Utaratibu

unaotumiwa na Asasi za Kiraia kwa kiasi kikubwa unategemea wafadhili ambao si wa kudumu na una matokeo ya muda mfupi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ongezeko la mahitaji ya idadi ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria, Serikali imeona umuhimu wa kuanzisha Mfumo huu ili kuboresha huduma hiyo katika usimamizi na uratibu. Kwa mantiki hiyo, Muswada huu unalenga kuweka Mfumo madhubuti na endelevu ambao utaziba ombwe lililopo na kutoa suluhisho la changamoto zilizopo na kuhakikisha kuwa huduma ya msaada wa kisheria nchini inaleta matokeo chanya kwa ustawi wa wananchi, hususani, wa vijijini na wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za Mawakili. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Saba.

**2.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada**

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inajumuisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa, matumizi na tafsiri ya misamiati na maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada unaopendekezwa.

**2.2 Sehemu ya Pili ya Muswada**

Sehemu ya Pili inaweka masharti ya usimamizi na uratibu wa watoa huduma ya msaada wa kisheria. Inaanzisha Bodi ya Ushauri ya Huduma ya Msaada wa Kisheria na kuainisha majukumu yake. Vilevile, inaweka utaratibu wa uteuzi wa Msajili na majukumu yake.

**2.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada**

Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti ya usajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria, inaainisha sifa za kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, utoaji wa cheti cha usajili mara baada ya kusajiliwa kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria, mazingira yatakayopelekea kusitishwa au kufutwa kwa cheti cha usajili. Aidha, Sehemu hii pia inaainisha haki ya rufaa dhidi ya uamuzi wa kusitishwa au kufutwa kwa cheti. Vilevile, inaweka masharti ya uteuzi wa Msajili Msaidizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

**2.4 Sehemu ya Nne ya Muswada**

Sehemu ya Nne inaainisha masharti mahsusi kwa wasaidizi wa kisheria, sifa, majukumu na masharti ya wasaidizi wa kisheria kutoa ushauri na usaidizi wa kisheria kwa mujibu wa masharti ya Muswada unaopendekezwa. Aidha, inaweka katazo kwa wasaidizi wa kisheria kutoza ada kwa mtu anayesaidiwa na kujihusisha na shughuli zilizotengwa kwa ajili ya mawakili.

**2.5 Sehemu ya Tano ya Muswada**

Sehemu ya Tano ya Muswada inaainisha masharti ya mtu anayeweza kuomba huduma ya msaada wa kisheria, masharti ya jumla ya huduma ya msaada wa kisheria, huduma ya msaada wa kisheria katika mashauri ya madai na jinai kwa amri ya Mahakama. Aidha, Sehemu hii inatoa masharti ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto na watu walio katika vituo vya Polisi, Magereza na vizuizi mbalimbali.

**2.6 Sehemu ya Sita ya Muswada**

Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu masharti ya fedha. Masharti hayo yanajumuisha vyanzo vya mapato ya Bodi, makadirio ya mwaka na vitabu vya hesabu. Vilevile, inaainisha Mamlaka ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua hesabu za Bodi.

**2.7 Sehemu ya Saba ya Muswada**

Sehemu ya Saba inaainisha masharti mengineyo. Masharti hayo yanajumuisha Mamlaka ya Msajili kutoa tangazo kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria kuthibisha uwepo wake, wajibu kuhusiana na miiko ya maadili ya kitaaluma kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria na Mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni za Maadili ya watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria. Vilevile, sehemu hii inaainisha masharti ya kuifuta Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashauri ya Jinai, Sura ya 21 na kuainisha Masharti yatokanayo na Masharti ya Mpito.

## 3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

**3.1 Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016 na Sekretariati ya Kamati, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa Sheria kwa kupitia vifungu vyote **49** vya Muswada tarehe 17/1/2017 na kujiridhisha na malengo na madhumuni ya Sheria inayotungwa katika Muswada huu.

**3.2 Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria tarehe 18/1/2017 ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu malengo na madhumuni ya Sheria hii.

**3.3 Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 tarehe 19 na 20 Januari 2017, Kamati ilikutana na Wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Taasisi za Elimu ya Juu, Vikundi Vya Wakulima, Asasi za Kiraia na Kambi Rasmi ya Upinzani

Bungeni ili kusikiliza na kupokea maoni yao kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa kitaalamu wa Muswada huu.

**3.4 Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maoni mbalimbali ya Wadau kwa muda wa siku mbili mfululizo Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya Wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Maoni ya Wadau kwa kiasi kikubwa yameisaidia Kamati katika kufanya Uchambuzi wa Muswada na hatimaye kutoa maoni kwa Serikali.

**3.5 Mheshimiwa Spika**, Tarehe 25/1/2017 Kamati ilikutana na mtoa hoja, Waziri wa Katiba na Sheria na kumpa nafasi kujibu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi uliofanyika. Yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Serikali ilikubali kuchukua Mapendekezo ya Kamati. Yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

**3.6 Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Wadau waliochangia katika Muswada huu wamekubaliana na malengo na madhumuni ya Muswada na kuipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuweka mfumo rasmi wa Kisheria wa kuwatambua Watoaji Huduma ya Msaada wa Kisheria Tanzania.

**3.7 Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu kwa kupitia kifungu kwa kifungu na baada ya kupokea na kuchambua nia na malengo ya Muswada huu Kamati iliona kwamba kwa maslahi ya Sekta ya utoaji huduma za msaada wa Kisheria Tanzania kuna haja ya kuvifanyia maboresho vifungu 45 vya Muswada huu kwa kutazama mazingira tuliyonayo hapa Tanzania na kwa kutazama pia Sheria za namna hii zilivyo katika nchi nyingine (International Comparative Perspective).

**3.8 Mheshimiwa Spika**, baadhi ya vifungu vilikuwa na makosa ya kiuchapaji na kisarufi na tayari vimeingizwa katika jedwali la marekebisho la Serikali. Kwa mfano, katika Ibara ya 4 (1) ya Muswada sentensi ‘’**There shall is established**’’ ina makosa ya kisarufi na kiuchapishaji na Kamati imeshauri isomeke ‘’**There is established**’’ au ‘’**There shall be established**’’. Katika Ibara ya 48 (2) ya Muswada sentensi inayosomeka ‘’…made under the repeal Act’’ ina makosa ya Kisarufi na Kamati imeshauri isomeke ‘’...made under the **repealed** Act’’. Makosa kama haya yameonekana katika vifungu mbalimbali vya Muswada na Serikali imeyapokea mapendekezo ya Kamati na kuyajumuisha katika jedwali la marekebisho.

**3.9 Mheshimiwa Spika**, vifungu ambavyo vilihitaji kuboreshwa zaidi ni kama ifuatavyo:- Kifungu cha 3 kuhusu tafsiri, Kifungu cha 5 kuhusu kazi za Bodi, Kifungu cha 6 kuhusu Msajili wa Utoaji Msaada wa Sheria na Kifungu cha 8 kuhusu uteuzi wa Wasajili Wasaidizi. Maboresho pia yalifanyika katika vifungu vinavyohusu sifa za Usajili wa Mtoa huduma ya Msaada wa Kisheria (Ibara ya 10), kusitishwa na kufutwa kwa Cheti cha Usajili (Ibara ya 16), utaratibu wa kusitishwa na kufutwa kwa Cheti (Ibara ya 16), usimamizi wa Watoa huduma ya Msaada wa Kisheria (Ibara ya 18), sifa za Wasaidizi wa Sheria (Ibara ya 19), urejeshwaji wa gharama (Ibara ya 29), Msaada wa Kisheria kwa Watoto walio katika vituo vya Polisi au Magereza (Ibara ya 35), Katazo kuhusu shughuli za kisiasa (Ibara ya 43), taratibu za mpito ( Ibara ya 49), Muundo na Wajumbe wa Bodi pamoja na masuala ya jumla ya muundo na dhima kwa ujumla wake.

**3.10 Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali, pande zote mbili zilikubaliana kufanya marekebisho kwa ajili ya kuboresha vifungu vyote vilivyokuwa na utata ili viwe bora zaidi.

**3.11 Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati katika Muswada huu yamezingatia uchambuzi wa kitaalamu wa Muswada huu uliofanywa na Kamati kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kwenye Kamati.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

**4.1 Mheshimiwa Spika,** katika Kifungu cha Tatu cha Tafasiri kuwe na tafasiri ya neno ''Advocate'' ili tafasiri hii iendane na tafasiri iliyomo katika Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafasiri, Sura ya Kwanza ya Sheria za Tanzania. Katika kifungu hiki Kamati pia inashauri kutolewa kwa tafasiri ya maneno ''Legal Advice and Assistance '' ambayo yameunganishwa. Kamati inashauri maneno haya yatenganishwe na kupatiwa tafsiri zinazojitegemea maana ni maneno yanayojitegemea na yenye maana tofauti katika fani ya Sheria.

**4.2 Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri pia kwamba maana ya ''Legal Aid Services'' yaani ''Huduma za Msaada wa Kisheria'' kama ilivyoandikwa kwenye Muswada ipewe maana kubwa zaidi na kujumuisha utoaji wa elimu, taarifa na uwakilishi wa Kisheria ili kuendana na dhima ya Muswada huu.

**4.3 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha Tatu Kamati inashauri Neno ''Lawyer'' lipewe tafasiri na neno ''Paralegal'' pia lipewe tafasiri sahihi ili kuendana na maudhui ya Muswada huu.

**4.4 Mheshimiwa Spika**, Katika Kifungu cha 6 (2) Kamati inashauri neno ''The Director'' liondolewe na badala yake litumike neno 'The Person'' ili kupanua wigo wa uteuzi wa msajili wa watoa huduma ya msaada wa Kisheria kutoka kwa mtu mmoja na kwenda kwa mtu yeyote katika Watumishi wa Umma ndani au nje ya Wizara ambaye ana sifa ya kuwa Msajili wa watoa huduma ya msaada wa Sheria Tanzania.

**4.5 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 7 (1) Kamati inashauri kwamba Msajili ashirikiane na watoa huduma wa Msaada wa Sheria na Vyuo vinavyotoa Elimu ya utoaji Msaada wa Sheria kuandaa Mitaala ya mafunzo ya utoaji huduma ya Msaada wa Kisheria.

**4.6 Mheshimiwa Spika**, kuhusu sifa za usajili wa mtoa huduma ya Msaada wa Kisheria katika Kifungu cha 10, Kamati inashauri kwamba uongezwe wigo wa watu wenye taaluma ya Sheria kwa Taasisi hiyo kwa kumuongeza Mwanasheria ambaye siyo Wakili wa Mahakama Kuu Tanzania.

**4.7 Mheshimiwa Spika**, kuhusu muda wa kushughulikia maombi ya Usajili, Kamati ilipendekeza kuwa badala ya siku 30 zinazopendekezwa kwenye Muswada ziwe siku 14. Baada ya majadiliano na Serikali imeonekana iwe siku 21 ili kuleta ufanisi wa kushughulikia maombi kwa pande zote mbili, yaani Serikali na Waombaji.

**4.8 Mheshimimwa Spika**, katika Kifungu cha 13 Kamati inapendekeza kwamba notisi ya kukataliwa kusajiliwa kwa Mwombaji itolewe ndani ya siku 7 baada ya maombi kufanyika. Baada ya majadiliano na Serikali imependekezwa kwamba notisi ya kukataliwa itolewe baada ya siku 14 ambazo ni utaratibu wa kawaida wa Serikali.

**4.9 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 14 (2) kuhusu rufaa, Kamati inapendekeza kwamba Sheria iweke wazi haki ya Rufaa kwa Muombaji kama hajaridhishwa na maamuzi ya Msajili na haki hii iwe ni ya kukata Rufaa Mahakama Kuu. Kamati inatambua kwamba kukiwa na kifungu kinachosema hivyo (Express provision) haki itakua na nguvu zaidi kuliko Kifungu kukaa kimya na kutegemea utaratibu wa mapitio ya Kimahakama yaani (Judicial Review) ambao upo katika misingi ya asili ya utoaji haki (Principles of Natural Justice).

Kamati inasisitiza kwamba Haki hii ni ya Kikatiba na ni vema ikasemwa waziwazi katika Sheria.

**4.10 Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 16 cha Muswada huu ni moja kati ya Vifungu vilivyohitaji majadiliano ya kina kati ya Kamati na Serikali. Kifungu hiki kinahusiana na kusitishwa na kufutwa kwa Cheti cha Usajili cha Mtoa huduma wa Msaada wa Kisheria. Baada ya majadiliano na Serikali Kamati inashauri kwamba kabla Cheti cha Mtoa huduma wa Msaada wa Kisheria hakijasimamishwa au kufutwa Mtoa huduma wa Msaada wa Kisheria apewe muda wa kutosha wa kushughulikia hilo tatizo na kutoa taarifa kwa Msajili kuhusu hatua alizochukua pale ambapo Mwajiriwa wake amefanya makosa ambayo yanaweza kusababisha Mtoa huduma za Msaada wa Kisheria asitishiwe au kufutiwa Usajili moja kwa moja.

**4.11 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 16 (1) (f) na Kifungu cha 43 (1) Kamati inashauri neno ''Political activities'' yaani ''Shughuli za Kisiasa'' lipatiwe tafsiri ili kuondoa utata wa maana yake na wigo''Scope'' wa matumizi yake wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

**4.12 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 19 kuhusu Sifa za Wasaidizi wa Sheria Kamati inashauri Sheria iwatambue Wasaidizi wa Kisheria wenye Elimu ya Sekondari na wale ambao wamekua wanafanya kazi ya Usaidizi wa Kisheria kwa angalau Miaka 2 huku wakiwa na sifa za msingi za kufahamu kusoma na kuandika na wamepokea mafunzo maalumu ya Utoaji Msaada wa Kisheria. Hii itatanua wigo wa kuwa na Wasaidizi wengi wa Kisheria hasa maeneo ya Vijijini ambapo ni ngumu kuwa na hata Wahitimu wa Kidato cha Nne.

**4.13 Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inashauri Vifungu vya 20 (c) na (f) vifutwe kwa sababu haviendani kikamilifu na majukumu yanayotambulika ya Watoa Huduma ya Msaada wa Sheria.

**4.14 Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri urasimu wa kutuma maombi ya huduma ya Msaada wa Kisheria uondolewe katika Kifungu cha 21 (1) na (2), badala yake wenye uhitaji wa Msaada wa Kisheria waende moja kwa moja kwa Mtoa huduma na kupeleka maombi ya kupata Msaada.

**4.15 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 27 kuhusu Msaada wa Sheria katika mashauri ya madai kwa amri ya Mahakama, Kamati inashauri kuongeza wigo wa Kimahakama kwa kuongeza Mabaraza ya Ardhi, Kodi, Kazi na Taasisi nyingine za utoaji na usimamizi wa haki ili kuongeza wigo wa huduma za Msaada wa Kisheria kwa Watu wengi zaidi.

**4.16 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 29 kuhusu urejeshwaji wa gharama, Kamati inashauri kwamba mtoa huduma ya Msaada wa Kisheria awe na haki ya kupokea sehemu ya tuzo ya Mahakama ili kufidia gharama mbalimbali za kesi.

**4.17 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 36 kuhusu Msaada wa Sheria kuhusu Watu walio kizuizini, Kamati inashauri Jeshi la Polisi au Magereza kuweka mazingira mazuri kwa watu walio na uhitaji wa huduma ya Msaada wa Kisheria.

**4.18 Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu cha 49 kuhusu taratibu za mpito, Kamati inashauri Taasisi zote ambazo tayari zinatoa huduma za Msaada wa Kisheria zitachukuliwa kuwa tayari zimeshasajiliwa na zitapewa Cheti cha Usajili kwa mujibu wa Taratibu za Sheria hii .

**4.19 Mheshimiwa Spika**, kuhusu Muundo wa Bodi ya Taifa ya Ushauri ya huduma ya Msaada wa Sheria, Kamati inashauri aongezwe Mjumbe kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) na Mjumbe kutoka Jukwaa la Taifa la Haki za Jinai (**National Criminal Justice Forum)** na kuwatoa katika Bodi Inspekta Jenerali wa Polisi na Kamishna Jenerali wa Magereza au Wawakilishi wao. Kamati inaamini kwamba uwakilishi wa TLS na mtu kutoka Jukwaa la Taifa la Jinai utaleta tija katika Bodi.

**4.20 Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuzingatia suala la Jinsia katika Muundo wa Bodi hii. Hii itasaidia kujenga uwezo wa Wanawake katika nafasi za Uongozi na Usimamizi bora wa utekelezaji wa Sheria hii kwa kutazama suala la utoaji Msaada wa Kisheria kwa jicho la kutazama makundi maalumu katika jamii ambayo yanahitaji jicho la haki za binadamu; kwa mfano Wanawake, Watoto na Watu wenye Ulemavu.

**4.21 Mheshimiwa Spika**, napenda kuliaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeyakubali mapendekezo mengi ya Kamati na kuyaweka katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa katika Bunge hili. Serikali pia imetoa maelezo ya ziada na ufafanuzi katika maeneo ya Muswada ambayo Kamati ilihitaji ufafanuzi.

**4.22 Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba uchambuzi wa Kitaalamu uliofanywa katika Muswada huu utasaidia kupatikana kwa Sheria bora ya kusimamia Sekta ya utoaji huduma za Kisheria nchini na kufungua ukurasa mpya kwa Watoa Msaada wa Kisheria Tanzania.

## 5.0 HITIMISHO

5.1 **Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipa kibali cha kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Harrison G. Mwakyembe Mb, kwa ushirikiano wake wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Kamati.

5.3 **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu ambayo kwa kiaasi kikubwa yamezingawa na Kamati. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao:-

- Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS);
- Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA);
- Mtandao wa Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria Tanzania(TANLAP);
- Muungano wa Vikundi Vya Wakulima Tanzania (MVIWATA);
- Jumuiya ya Wakristo Tanzania (CCT);
- Sekretariati ya Msaada wa Sheria (LAS);
- Chuo Kikuu Dodoma (UDOM);
- Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF);
- Chuo cha Biashara (CBE) Tawi la Dodoma na;
- Taasisi ya Uwezeshaji wa Msaada wa Kisheria (LSF).

5.4 **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa kutoka Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha Muswada huu.
**Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa,Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti

3. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb -Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Ussi Pondeza, Mb -Mjumbe
22. Mhe. Ally Salehe,Mb - Mjumbe
23. Mhe. Wanu Hafidhi Ameir, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Taska Mbogo Mb, - Mjumbe
25. Mhe.Tundu Lissu, Mb - Mjumbe Mwalikwa
26. Mhe. Hawa Mchafu, Mb - Mjumbe Mwalikwa

**5.5 Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililllah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Masaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Mkurugenzi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndg. Pius Mboya, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Mossy Lukuvi na Ndg. Prudence Rweyongeza, Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe, Wanasheria wa Bunge Ndg. Stephano Mbutu, Ndg. Evelyne Shibandiko, Ndg. Rehema Kipera na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

**5.6 Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**KATIBA NA SHERIA**
JANUARI 2017

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, hapa wakati ukiwa haupo tulipewa taarifa kwamba mawazo yako uliyapeleka kwenye Kamati na Kamati imeyachukua, bado unayo ya kusema leo? Karibu Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mawazo yangu yapo kama siku zote, lakini kabla sijaanza, naomba niseme jambo ambalo linatutatiza muda mrefu sana. Nilishiriki katika vikao vya Kamati na tarehe ambayo nilikuwa naifahamu mimi kutokana na vikao vya Kamati ni kwamba Muswada huu ungeletwa tarehe 09 ya mwezi wa pili yaani wiki ijayo. Ni jana tu ndiyo tumepata taarifa nilivyokuja kwenye *briefing* kwamba Muswada huu unakuja leo na kwa sababu hiyo, pamoja na kuumwa, sijalala na bado ukweli wa Mungu ni kwamba sijamaliza kazi niliyotakiwa kuifanya kwa *standards* ambazo mmezizoea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitakavyojitahidi kuthibitisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada huu ni muhimu sana. Suala la msaada wa kisheria kwa watu wasiojiweza kiuchumi na kijamii limekuwa na mjadala mkubwa wa kisheria na kikatiba katika nchi mbalimbali. Wazo la kuwa na utaratibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa watu maskini unaogharamiwa na Serikali lilitolewa kwa mara ya kwanza na mwanamke wa kwanza kuwa wakili katika Jimbo la California nchini Marekani, Clara Shortridge Foltz, aliyesema, wakati wa Maonyesho ya Ulimwengu ya Chicago, mwaka 1893, kwamba, naomba kunukuu:

*"For the conviction of the accused person every weapon is provided and used, even those poisoned by wrong and injustice. But what machinery is provided for the defense of the innocent? None, absolutely none."* Yaani, "Kwa lengo la kumtia mtuhumiwa hatiani kila silaha inatolewa na inatumiwa, hata zile

ambazo zimetiwa sumu ya ubatili na uonevu. Lakini utaratibu gani umewekwa kwa ajili ya utetezi wa wasio na hatia. Hamna, hamna hata kidogo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ishirini baadaye, yaani mwaka 1913, Jimbo la California lilianzisha Ofisi ya kwanza ya Mlinzi wa Umma *(Public Defender's Office)* kwa ajili ya kutoa utetezi kwa watu wasiojiweza kiuchumi. Lakini hata kabla ya hapo, Marekebisho ya Sita ya Katiba ya Marekani ya Mwaka 1789, yaliweka msingi wa kikatiba wa Serikali kutoa msaada wa kisheria kwa watu maskini, naomba ninukuu hayo Marekebisho ya Sita ya Katiba ya Marekani:

*"In all criminal prosecutions, the accused shall enjoy the right to a speedy and public trial, by an impartial jury of the state and district wherein the crime shall have been committed … and to be informed of the nature and cause of the accusation…, and to have the assistance of counsel for his defense."* Yaani, "Katika mashtaka yote ya jinai, mtuhumiwa atakuwa na haki ya kesi yake kuendeshwa kwa muda muafaka na hadharani, mbele ya baraza lisilokuwa na upendeleo la jimbo na wilaya alikofanyia makosa… na kujulishwa aina na maelezo ya tuhuma dhidi yake… na kupatiwa msaada wa wakili kwa ajili ya utetezi wake."

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ilichukua karibu karne moja na nusu kwa mahakama za Marekani kuweka msimamo juu ya suala hili. Katika kesi maarufu ya Powell dhidi Alabama ya mwaka 1932, Jaji Sutherland wa Mahakama Kuu *(Supreme Court)* ya Marekani alielezea hatari ya kushtaki watu wasiokuwa na hatia lakini hawana haki ya kupatiwa wakili kwa sababu ya umaskini wao kwa maneno yafuatayo:

*"Even the intelligent and educated layman has small and sometimes no skill in the science of law. If charged with crime, he is incapable, generally, of determining for himself whether the indictment is good or bad. He is unfamiliar with the rules of evidence. Left without the aid of counsel, he may be put on trial without proper charge, and convicted upon incompetent evidence, or evidence irrelevant to the issue or otherwise inadmissible. He lacks both the skill and knowledge adequately to prepare his defense, even though he have a perfect one. He requires the guiding hand of counsel at every step in the proceedings against him. Without it, though he be not guilty, he faces the danger of conviction because he does not know how to establish his innocence."*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani: "Hata mlei mwenye akili na aliyesoma ana maarifa kidogo, au wakati mwingine hana maarifa kabisa katika sayansi ya sheria. Kama akishtakiwa kwa jinai, hana uwezo, kwa ujumla, wa kufahamu yeye mwenyewe kama hati ya mashtaka ni nzuri au mbaya. Hana uelewa wa kanuni za ushahidi. Akiachwa bila msaada wa Wakili, anaweza kushtakiwa bila hati sahihi ya mashtaka na kupatikana na hatia kwa ushahidi usio halali, au ushahidi usio na uhusiano wowote na suala linalobishaniwa, au ushahidi ambao haukubaliki kisheria. Hana maarifa au uelewa wa kutosha wa kuandaa utetezi wake, hata kama ana utetezi kamilifu kabisa. Anahitaji kuongozwa na mkono wa wakili katika kila hatua ya mashtaka dhidi yake. Bila hilo, hata kama hana hatia, anakabiliwa na hatari ya kukutwa na hatia kwa sababu hafahamu namna ya kuthibitisha uadilifu wake."

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya miaka thelathini baadaye, Jaji Hugo Black wa mahakama hiyo alirejea umuhimu wa msaada wa kisheria kwa watu maskini katika kesi nyingine maarufu ya Gideon dhidi Wainwright ambapo alisema:

*"The right to be heard would be, in many cases, of little avail if it did not comprehend the right to be heard by counsel. From the beginning, our state and national constitutions and laws have laid great emphasis on procedural and substantive safeguards designed to assure fair trials before impartial tribunals (and courts) in which every party to the case stands equal before the law. This noble ideal cannot be realized if the poor person engaged in a case has to face his or her opponent without a lawyer to assist him or her."*

Yaani haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu itakuwa, katika kesi nyingi, ya msaada mdogo kama haikujumuisha haki ya kusikilizwa kupitia Wakili. Tangu mwanzoni kabisa, katiba na sheria zetu za majimbo na ya Taifa zimeweka msisitizo kwenye ulinzi wa kimwenendo na wa kimsingi uliolengwa kuhakikisha mashauri ya haki mbele ya mabaraza (na mahakama) zisizokuwa na upendeleo ambapo kila upande kwenye kesi unasimama kwa usawa mbele ya sheria. Tarajio hili tukufu haliwezi kutekelezwa endapo mtu maskini mwenye kesi inabidi amkabili mpinzani wake bila kuwa na mwanasheria wa kumsaidia."

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mahakama ya Juu ya Marekani kuweka msimamo huo, nchi hiyo iliweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtuhumiwa wa makosa ya jinai ambaye hana uwezo wa fedha za kulipia wakili, anapatiwa wakili aliyelipiwa kwa fedha za umma. Utaratibu huo ndio unaoitwa Ofisi ya Mlinzi wa Umma na tangu wakati huo umeenea katika nchi

mbalimbali duniani zikiwemo Kenya, Nigeria, Afrika Kusini, Brazil, Ujerumani, Hungary na Uingereza, kutaja chache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zinazojali usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu zimetunga sheria zinazolazimisha mamlaka za nchi kutoa msaada wa kisheria kwa kila mtu anayekabiliwa na mashtaka ya jinai au ambaye haki na wajibu wake inafanyiwa maamuzi na mahakama au vyombo vingine vya kimahakama. Kama ilivyosema Mahakama ya Juu ya Marekani katika Gideon dhidi ya Wainwright:

*"… in our adversarial system of criminal justice, any person haled into court, who is too poor to hire a lawyer, cannot be assured a fair trial unless counsel is provided for him."* Yaani, "… katika mfumo wetu kinzani wa haki jinai, mtu yeyote anayeburuzwa mahakamani ambaye ni maskini asiyeweza kuweka Wakili, hawezi kuhakikishiwa kusikilizwa kwa ukamilifu isipokuwa tu kama atapatiwa Wakili."

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu haikufuata utamaduni huu wa kuanzisha Ofisi ya Mlinzi wa Umma. Badala yake, mwaka 1969, Bunge hili lilitunga Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa Mashtaka ya Jinai, yaani, *The Legal Aid (Criminal Proceedings) Act,* Sura ya 21 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania. Hii ndio Sheria inayopendekezwa kufutwa na kubadilishwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa kifungu cha tatu (3) cha Sheria hii kiliweka masharti ya 'mamlaka ya uidhinishaji' kuidhinisha mtuhumiwa wa makosa ya jinai kupata msaada wa Wakili pale ambapo mamlaka ya uidhinishaji inaona inafaa kufanya hivyo kwa maslahi ya utendaji haki na kwa sababu mtuhumiwa hana uwezo wa kifedha wa kuweka Wakili, katika hali ya Tanzania, ni watuhumiwa wa makosa ya mauaji na makosa mengine yenye adhabu ya kifo tu ndio ambao wamekuwa wanapatiwa msaada wa Wakili aliyelipwa kwa fedha za umma, kama inavyoelekezwa na kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo. Hii ni licha ya Mahakama Kuu ya Tanzania, katika kesi ya Thomas Mjengi dhidi ya Jamhuri na Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika kesi ya Moses Muhagama Lawrence dhidi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutamka kwamba kila mtuhumiwa wa makosa ya jinai asiyekuwa na uwezo ana haki ya kupatiwa msaada wa Wakili bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli za Majaji maarufu niliowanukuu na msimamo wa Mahakama zetu za juu katika kesi nilizozitaja, zinathibitisha umuhimu wa kila mtu kupata msaada wa Wakili pale ambapo haki na wajibu wake inafanyiwa maamuzi na mahakama au baraza au chombo kingine

kinachohusika. Kwa sababu ya umuhimu huo, hata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, imetamka waziwazi kwamba:

"Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria." Katiba yetu inasisitiza kwamba kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba: "Wakati haki na wajibu kwa mtu yeyote inapohitajika kufanyiwa maamuzi na mahakama au chombo kingine kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu…." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa haki ya kikatiba ya usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu ilitazamia Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ingeleta Muswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa kila Mtanzania. Badala yake, Serikali hii imeleta Muswada wa sheria ya kudhibiti wanaotoa msaada wa kisheria kwa Watanzania; dhana hizi mbili zina tofauti kubwa inayohitaji ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, badala ya kutamka wazi kwamba kila mtu ana haki ya kupatiwa msaada wa kisheria utakaolipiwa kwa fedha za umma, Muswada huu umenakili matakwa ya kifungu cha 3 na cha 4 cha Sheria ya sasa. Tofauti pekee ni kwamba, kwa Muswada huu, msaada wa kisheria unaweza sasa kutolewa hata kwa wadaawa maskini katika mashauri ya madai. Kwa sababu hiyo, haki ya kupata msaada wa kisheria bado inabakia mateka wa 'mamlaka ya uidhinishaji' kama ilivyo sasa chini ya sheria inayopendekezwa kufutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mtu maskini anayehitaji msaada wa kisheria anaweza kupeleka maombi yake kwa watoaji msaada huo kwa mujibu wa marekebisho ya aya za 21 na 22 za Muswada huu, bado ukweli unabaki kwamba haki ya kuomba kupatiwa msaada sio haki ya kupatiwa msaada huo. Muswada huu hauna masharti yoyote ya kuwalazimisha watoa msaada wa kisheria kukubali kila maombi yanayopelekwa kwao. Hii ni sawasawa kwa sababu watoaji msaada wa kisheria hawana uhakika wa kurudishiwa gharama watakazotumia katika kuendesha kesi ya mtu waliyempatia msaada. Aya ya 29 ya Muswada inayoweka utaratibu wa kulipa gharama za kesi kwa mtu anayepewa msaada haitoi masharti kwamba mtoa msaada wa kisheria lazima arudishiwe gharama zake hata pale ambapo mpewa msaada amerudishiwa gharama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, aya ya 34 inayozungumzia utaratibu wa gharama zitakazotumiwa na Mawakili kwa ajili ya kuendeshea kesi, inapendekeza kwamba gharama zinazoweza kulipwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ni zile zinazoitwa 'gharama mahsusi' tu, na sio gharama za kawaida za uendeshaji wa kesi na mashauri ya madai. Muhimu zaidi, aya hiyo haijaweka masharti kwamba hata hizo zinazoitwa 'gharama mahsusi' ni lazima zilipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya ya aya ya 34, vilevile, yamechukuliwa kama yalivyo kutoka kifungu cha 5 cha sheria inayopendekezwa kufutwa na kubadilishwa na Muswada huu. Kwa maneno mengine, hakuna mabadiliko yoyote ya maana yanayopendekezwa na Muswada huu kuhusu suala hili. Badala yake, vifungu vya sheria ya sasa yenye umri wa takriban miaka 48, vimepakwa rangi mpya na kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu kama mambo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa pili wa Muswada huu ni kwamba Serikali imekwepa kabisa kuanzisha taasisi mahsusi itakayokuwa na wajibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa gharama ya Serikali. Badala yake, Muswada unapendekeza kuendelea na utaratibu wa sasa ambapo msaada wa kisheria hutolewa, kwa kiasi kikubwa na taasisi zisizo za kiserikali na au Mawakili binafsi kwa kutumia utaratibu wa '*assigned counsel*' chini ya sheria ya sasa. Chombo pekee cha umma kinachopendekezwa kuundwa chini ya Muswada huu ni Bodi ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria ambayo itakuwa na jukumu la uratibu wa masuala ya msaada wa kisheria. Bodi hii haina mamlaka wala wajibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Bunge lako Tukufu lielewe upungufu wa Muswada huu, hatuna budi kulinganisha na utaratibu uliowekwa na jirani zetu wa Kenya. Mwaka jana, Kenya ilitunga Sheria ya Msaada wa Sheria *(The Legal Aid Act, 2016),* ambayo ilianza kutumika tarehe 10 Mei, 2016. Sheria hiyo imeanzisha taasisi mahsusi, inayoitwa *National Legal Aid Service,* ambayo inatakiwa kutoa msaada wa kisheria unaogharamiwa na Serikali kwa watu wanaostahili kupata msaada huo, katika masuala ya madai, jinai, watoto, Katiba, masuala yenye maslahi ya umma na masuala mengine yatakayoamuliwa na mamlaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaostahili kupatiwa msaada wa kisheria kwa gharama ya umma wametajwa chini ya sheria hiyo ya Kenya kuwa ni watu maskini ambao ni wakazi wa Kenya na ambao ni raia wa Kenya, watoto, wakimbizi, wahanga wa biashara ya usafirishaji watu *(human trafficking),* wakimbizi wa ndani ya nchi *(internally displaced persons)* na watu

wasiokuwa na utaifa *(stateless persons)*. *National Legal Aid Service* ya Kenya haina tofauti na Ofisi ya Mlinzi wa Umma katika nchi nyingine tulizozitaja mwanzoni. Licha ya kukopa mambo mengi kutoka Sheria ya Msaada wa Sheria ya Kenya, Muswada ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu haupendekezi kuundwa kwa chombo mahsusi cha aina ya *National Legal Aid Service* au *Office of the Public Defender.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tatu la Muswada huu udhibiti wa Serikali. Kwa utaratibu wa sheria ya sasa, vyombo vinavyotoa msaada wa kisheria kwa watu maskini ni taasisi zisizo za Kiserikali kama vile *Legal and Human Rights Centre, Tanzania Women Lawyers' Association, Tanganyika Law Society, Envirocare, National Organization for Legal Aid, Lawyers' Environmental Action Team* na Taasisi nyingine za aina hiyo. Pamoja na Taasisi hizi, *the Legal Aid Committee,* yaani, Kamati ya Msaada wa Kisheria ya Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nayo imetoa msaada wa kisheria kwa watu maskini kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zote hizi hazihitaji kuandikishwa mara tu baada ya kutimiza masharti ya usajili wa Taasisi hizo. Muswada huu unapendekeza sasa kwamba yeyote anayetaka kutoa msaada wa kisheria sasa lazima aandikishwe na Msajili wa Bodi ya Ushauri wa Msaada wa Kisheria asipoandikishwa hawezi kutoa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sikupata muda wa kumalizia. Nitamalizia mchana huu na maoni yangu yote yatakapokamilika yataletwa kabla ya Bunge la saa 11, naomba kushukuru kwa kunipa fursa hii ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tundu Lissu na pole kwa kuugua.

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, MHESHIMIWA TUNDU A.M. LISSU, KUHUSU *MUSWADA WA SHERIA YA MSAADA WA KISHERIA, 2016* (*THE LEGAL AID ACT, 2016*)** (Kanuni ya 84(6) ya *Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016*) **KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,
Kama nitakavyojitahidi kuthibitisha mbele ya Bunge lako tukufu, Muswada huu ni muhimu sana. Suala la msaada wa kisheria kwa watu wasiojiweza kiuchumi na kijamii limekuwa na mjadala mkubwa wa kisheria na kikatiba katika nchi

mbali mbali. Wazo la kuwa na utaratibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa watu maskini unaogharamiwa na serikali lilitolewa kwa mara ya kwanza na mwanamke wa kwanza kuwa wakili katika Jimbo la California, Marekani, Clara Shortridge Foltz, aliyesema, wakati wa Maonyesho ya Ulimwengu ya Chicago, mwaka 1893, kwamba: *"For the conviction of the accused every weapon is provided and used, even those poisoned by wrong and injustice. But what machinery is provided for the defense of the innocent? None, absolutely none."* Yaani, *"Kwa lengo la kumtia mtuhumiwa hatiani kila silaha inatolewa na inatumiwa, hata zile ambazo zimetiwa sumu ya ubatili na uonevu. Lakini ni utaratibu gani umewekwa kwa ajili ya utetezi wa wasio na hatia. Hamna, hamna hata kidogo."*

Miaka ishirini baadae, yaani mwaka 1913, Jimbo la California lilianzisha Ofisi ya kwanza ya Mlinzi wa Umma (Public Defender Office) kwa ajili ya kutoa utetezi kwa watu wasiojiweza kiuchumi.

Lakini hata kabla ya hapo, Marekebisho ya Sita ya Katiba ya Marekani ya mwaka 1789, yaliweka msingi wa kikatiba wa serikali kutoa msaada wa kisheria kwa watu maskini: *"In all criminal prosecutions, the accused shall enjoy the right to a speedy and public trial, by an impartial jury of the state and district wherein the crime shall have been committed … and to be informed of the nature and cause of the accusation …, and to have the assistance of counsel for his defense."* Yaani, *"Katika mashtaka yote ya jinai, mtuhumiwa atakuwa na haki ya kesi yake kuendeshwa kwa muda muafaka na hadharani, mbele ya baraza lisilokuwa na upendeleo la jimbo na wilaya alikofanyia makosa … na kujulishwa aina na maelezo ya tuhuma dhidi yake … na kupatiwa msaada wa wakili kwa ajili ya utetezi wake."*

Hata hivyo, ilichukua karibu karne moja na nusu kwa mahakama za Marekani kuweka msimamo juu ya suala hili. Katika kesi maarufu ya *Powell dhidi Alabama*[1] ya mwaka 1932, Jaji Sutherland wa Mahakama ya Juu (Supreme Court) ya Marekani alielezea hatari ya kushtaki watu wasio na hatia lakini hawana haki ya kupatiwa wakili kwa sababu ya

[1] 287 U.S. 45 (1932)

umaskini wao kwa maneno yafuatayo: *"Even the intelligent and educated layman has small and sometimes no skill in the science of law. If charged with crime, he is incapable, generally, of determining for himself whether the indictment is good or bad. He is unfamiliar with the rules of evidence. Left without the aid of counsel, he may be put on trial without proper charge, and convicted upon incompetent evidence, or evidence irrelevant to the issue or*

*otherwise inadmissible. He lacks both the skill and knowledge adequately to prepare his defense, even though he have a perfect one. He requires the guiding hand of counsel at every step in the proceedings against him. Without it, though he be not guilty, he faces the danger of conviction because he does not know how to establish his innocence."*

Yaani: *"Hata mlei mwenye akili na aliyesoma ana maarifa kidogo, au wakati mwingine hana maarifa kabisa katika sayansi ya sheria.*

*Kama akishtakiwa kwa jinai, hana uwezo, kwa ujumla, wa kufahamu yeye mwenyewe kama hati ya mashtaka ni nzuri au mbaya. Hana uelewa wa kanuni za ushahidi. Akiachwa bila msaada wa wakili, anaweza kushtakiwa bila hati sahihi ya mashtaka, na kupatikana na hatia kwa ushahidi usio halali, au ushahidi usio na uhusiano wowote na suala linalobishaniwa, au ushahidi ambao haukubaliki kisheria. Hana maarifa au uelewa wa kutosha wa kuandaa utetezi wake, hata kama ana utetezi kamilifu kabisa. Anahitaji kuongozwa na mkono wa wakili katika kila hatua ya mashtaka dhidi yake. Bila hilo, hata kama hana hatia, anakabiliwa na hatari ya kukutwa na hatia kwa sababu hafahamu namna ya kuthibitisha uadilifu wake."*

Zaidi ya miaka thelathini baadae, Jaji Hugo L. Black wa Mahakama hiyo alirejea umuhimu wa msaada wa kisheria kwa watu maskini katika kesi nyingine maarufu ya *Gideon dhidi Wainwright*[2] ambapo alisema:

*"The right to be heard would be, in many cases, of little avail if it did not comprehend the right to be heard by counsel. From the beginning, our state and national constitutions and laws have laid great emphasis on procedural and substantive safeguards designed to assure fair trials before impartial tribunals (and courts) in which every party to the case stands equal before the law. This noble ideal cannot be realized if the poor person engaged in a case has to face his or her opponent without a lawyer to assist him or her."*

Yaani: *"Haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu itakuwa, katika kesi nyingi, ya msaada mdogo kama haikujumuisha haki ya kusikilizwa kupitia wakili. Tangu mwanzoni kabisa, katiba na sheria zetu za majimbo na ya taifa zimeweka msisitizo kwenye ulinzi wa kimwenendo na wa kimsingi uliolengwa kuhakikisha mashauri ya haki mbele ya mabaraza (na mahakama) zisizokuwa na upendeleo ambapo kila upande kwenye kesi unasimama kwa usawa mbele ya sheria.*

[2] 372 U.S. 335 (1963)

*Tarajio hili tukufu haliwezi kutekelezwa endapo mtu maskini mwenye kesi inabidi amkabili mpinzani wake bila kuwa na mwanasheria wa kumsaidia."*

Mheshimiwa Spika,
Baada ya Mahakama ya Juu ya Marekani kuweka msimamo huo, nchi hiyo iliweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtuhumiwa wa makosa ya jinai ambaye hana uwezo wa fedha za kulipia wakili, anapatiwa wakili aliyelipiwa kwa fedha za umma. Utaratibu huo ndio unaoitwa Ofisi ya Mlinzi wa Umma, na tangu wakati huo umeenea katika nchi mbali mbali duniani zikiwemo Kenya, Nigeria, Afrika Kusini, Brazil, Ujerumani, Hungary na Uingereza.

Mheshimiwa Spika,
Nchi zinazojali usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu zimetunga sheria zinazolazimisha mamlaka za nchi kutoa msaada wa kisheria kwa kila mtu anayekabiliwa na mashtaka ya jinai au ambaye haki na wajibu wake inafanyiwa maamuzi na mahakama au vyombo vingine vya kimahakama. Kama ilivyosema Mahakama ya Juu ya Marekani katika *Gideon dhidi ya Wainwright*, "*… in our adversarial system of criminal justice, any person haled into court, who is too poor to hire a lawyer, cannot be assured a fair trial unless counsel is provided for him.*" Yaani, "*… katika mfumo wetu kinzani wa haki jinai, mtu yeyote anayeburuzwa mahakamani ambaye ni maskini asiyeweza kuweka wakili, hawezi kuhakikishiwa kusikilizwa kwa ukamilifu isipokuwa tu kama atapatiwa wakili.*"

Mheshimiwa Spika,
Nchi yetu haikufuata utamaduni huu wa kuanzisha Ofisi ya Mlinzi wa Umma. Badala yake, mwaka 1969, Bunge hili lilitunga *Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa Mashtaka ya Jinai*, yaani, *the Legal Aid (Criminal Proceedings) Act, Sura ya 21 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania*. Hii ndio Sheria inayopendekezwa kufutwa na kubadilishwa na Muswada huu.

Ijapokuwa kifungu cha 3 cha Sheria hii kiliweka masharti ya 'mamlaka ya uidhinishaji' kuidhinisha mtuhumiwa wa makosa ya jinai kupata msaada wa wakili pale ambapo mamlaka ya uidhinishaji inaona inafaa kufanya hivyo kwa maslahi ya utendaji haki na kwa sababu mtuhumiwa hana uwezo wa kifedha wa kuweka wakili, katika hali ya Tanzania, ni watuhumiwa wa makosa ya mauaji na makosa mengine yenye adhabu ya kifo tu ndio ambao wamekuwa wanapatiwa msaada wa wakili aliyelipwa kwa fedha za umma, kama inavyoelekezwa na kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo.

Hii ni licha ya Mahakama Kuu ya Tanzania, katika kesi ya *Thomas Mjengi dhidi ya Jamhuri*[3], na Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika kesi ya *Moses Muhagama Laurance dhidi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar*[4] kutamka kwamba kila mtuhumiwa wa makosa ya jinai asiyekuwa na uwezo ana haki ya kupatiwa msaada wa wakili bila malipo.

Mheshimiwa Spika,
Kauli za majaji maarufu niliowanukuu, na msimamo wa mahakama zetu katika kesi nilizozitaja, zinathibitisha umuhimu wa kila mtu kupata msaada wa wakili pale ambapo haki na wajibu wake inafanyiwa maamuzi na mahakama au baraza au chombo kingine kinachohusika. Kwa sababu ya umuhimu huo, hata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano[5], imetamka wazi wazi kwamba: *"Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria."*[6]

Katiba yetu imesisitiza kwamba kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba *"wakati haki na wajibu kwa mtu yeyote inapohitajika kufanyiwa maamuzi na mahakama au chombo kingine kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu…."*[7]

Mheshimiwa Spika,
Kwa kuzingatia umuhimu wa haki ya kikatiba ya usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu ilitazamia serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ingeleta muswada wa sheria ya msaada wa kisheria kwa kila Mtanzania. Badala yake, Serikali hii imeleta Muswada wa sheria ya kudhibiti wanaotoa msaada wa kisheria kwa Watanzania. Dhana hizi mbili zina tofauti kubwa inayohitaji ufafanuzi.

Kwanza, badala ya kutamka wazi kwamba kila mtu ana haki ya kupatiwa msaada wa kisheria utakaolipiwa kwa fedha za umma, Muswada huu umenakili matakwa ya kifungu cha 3 na cha 4 cha Sheria ya sasa.[8] Tofauti pekee ni

[3] [1992] TLR 157
[4] Criminal Appeal No. 17 ya 2002
[5] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2 ya Marejeo ya Sheria za Tanzania.
[6] Ibara ya 13(1)
[7] Ibara ya 13(6)(a)
[8] Aya ya 33(1)

kwamba, kwa Muswada huu, msaada wa kisheria unaweza sasa kutolewa hata kwa wadaawa maskini katika mashauri ya madai.[9]

Kwa sababu hiyo, haki ya kupata msaada wa kisheria bado inabakia mateka wa 'mamlaka ya uidhinishaji' kama ilivyo sasa chini ya Sheria inayopendekezwa kufutwa.

Ni kweli, Mheshimiwa Spika, kwamba mtu maskini anayehitaji msaada wa kisheria anaweza kupeleka maombi yake kwa watoaji msaada huo kwa mujibu wa marekebisho ya aya za 21 na 22 za Muswada huu, bado ukweli unabaki kwamba haki ya kuomba kupatiwa msaada sio haki ya kupatiwa msaada huo.

Muswada huu hauna masharti yoyote ya kuwalazimisha watoaji msaada wa kisheria kukubali kila maombi yanayopelekwa kwao.

Na hii ni sawa sawa kwa sababu watoaji msaada wa kisheria hawana uhakika wa kurudishiwa gharama watakazotumia katika kuendesha kesi ya mtu waliyempatia msaada. Aya ya 29 inayoweka utaratibu wa kulipa gharama za kesi kwa mtu anayepewa msaada haitoi masharti kwamba mtoa msaada wa kisheria lazima arudishiwe gharama zake hata pale ambapo mpewa amerudishiwa gharama zake.

Aidha, aya ya 34 inayozungumzia utaratibu wa gharama zitakazotumiwa na mawakili kwa ajili ya kuendeshea kesi, inapendekeza kwamba gharama zinazoweza kulipwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ni zile zinazoitwa 'gharama mahsusi' tu, na sio gharama za kawaida za uendeshaji wa kesi na mashauri ya madai. Muhimu zaidi, aya hiyo haijaweka masharti kwamba hata hizo 'gharama mahsusi' ni lazima zilipwe.

Mheshimiwa Spika,
Mapendekezo haya ya aya ya 34, vile vile, yamechukuliwa kama yalivyo kutoka kifungu cha 5 cha Sheria inayopendekezwa kufutwa na kubadilishwa na Muswada huu. Kwa maneno mengine, Mheshimiwa Spika, hakuna mabadiliko yoyote ya maana yanayopendekezwa na Muswada huu kuhusu suala hili. Badala yake, vifungu vya Sheria ya sasa yenye umri wa takriban miaka 48, vimepakwa rangi mpya na kuletwa mbele ya Bunge lako tukufu kama mambo mapya.

[9] Aya ya 27

Mheshimiwa Spika,
Upungufu wa pili wa Muswada huu ni kwamba Serikali imekwepa kabisa kuanzisha taasisi mahsusi itakayokuwa na wajibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa gharama ya serikali. Badala yake, Muswada unapendekeza kuendelea na utaratibu wa sasa ambapo msaada wa kisheria hutolewa, kwa kiasi kikubwa, na taasisi zisizo za kiserikali, na/au mawakili binafsi kwa kutumia utaratibu wa 'assigned counsel' chini ya Sheria ya sasa.[10] Chombo pekee cha umma kinachopendekezwa kuundwa chini ya Muswada huu ni Bodi ya Ushauri ya Msaada wa Kisheria ambayo itakuwa na jukumu la uratibu wa masuala ya msaada wa kisheria. Bodi hii haina mamlaka wala wajibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika,
Ili Bunge lako tukufu lielewe mapungufu ya Muswada huu, hatuna budi kulinganisha na utaratibu uliowekwa na jirani zetu wa Kenya. Mwaka jana, Kenya ilitunga *Sheria ya Msaada wa Sheria* (*the Legal Aid Act, 2016*), ambayo ilianza kutumika tarehe 10 Mei, 2016. Sheria hiyo imeanzisha taasisi mahsusi, inayoitwa National Legal Aid Service, ambayo inatakiwa kutoa msaada wa kisheria unaogharamiwa na Serikali kwa watu wanaostahili kupata msaada huo, katika masuala ya madai, jinai, watoto, katiba, masuala yenye maslahi ya umma na masuala mengine yatakayoamuliwa na Mamlaka hiyo.

Watu wanaostahili kupatiwa msaada wa kisheria kwa gharama ya umma wametajwa kuwa ni watu maskini ambao ni wakazi wa Kenya na ambao ni raia wa Kenya, watoto, wakimbizi, wahanga wa biashara ya usafirishaji watu (human trafficking), wakimbizi wa ndani ya nchi (internally displaced persons) na watu wasiokuwa na utaifa (stateless persons). National Legal Aid Service ya Kenya haina tofauti na Ofisi ya

Mlinzi wa Umma katika nchi nyingine tulizozitaja mwanzoni. Licha ya kukopa mambo mengi kutoka kwenye Sheria ya Msaada wa Sheria ya Kenya, Muswada ulioko mbele ya Bunge lako tukufu haupendekezi kuundwa kwa chombo mahsusi cha aina ya National Legal Aid Service au Office of the Public Defender.

---

[10] Angalia Sehemu ya III na IV ya Muswada.

Mheshimiwa Spika,
Tatizo la tatu la Muswada huu udhibiti wa serikali. Kwa utaratibu wa Sheria ya sasa, vyombo vinavyotoa msaada wa kisheria kwa watu maskini ni taasisi zisizo za kiserikali kama vile Legal and Human Rights Centre (LHRC), Tanzania Women Lawyers' Association (TAWLA), Tanganyika Law Society (TLS), Envirocare, National Organization for Legal Aid (NOLA), Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) na taasisi nyinginezo za aina hiyo. Pamoja na taasisi hizi, the Legal Aid Committee (LAC), yaani, Kamati ya Msaada wa Kisheria ya Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nayo imetoa msaada wa kisheria kwa watu maskini kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika,
Baada ya uchanbuzi huo, naomba kuwasilisha,

...........................
**TUNDU A. M LISSU (MB)**
**WAZIRI KIVULI**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimepewa orodha hapa ya wachangiaji. Kwa hiyo, tutaanza na wachangiaji waliopo halafu tutaendelea baadae na utaratibu mwingine. Tutaanza na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Anna Gidarya ajiandae na Mheshimiwa Ajali Akbar atafuata.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa kwanza kwenye Muswada huu ambao nauona ni wa muhimu sana kwa mustakabali wa wananchi maskini wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka ku-*declare interest,* Mheshimiwa Waziri aliyeleta Muswada huu hapa Bungeni leo ni ndugu yangu mimi wa damu, ni pacha wangu lakini kwa hili natofautiana nae. Sasa hivi amekuwa Waziri karibu mwaka mmoja na mwezi, alikuwa wapi kuleta Muswada huu toka mwanzo na Mawaziri wengine waliomtangulia walikuwa wapi kuleta Muswada mzuri kama huu hapa Bungeni? Naomba nitofautiane naye ndugu yangu na Mawaziri wote waliotangulia, walikuwa wapi kuleta Muswada mzuri kama huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Mheshimiwa Tundu Lissu mdogo wangu anasema hizi Taasisi za kujiandikisha amezitaja nyingi Chuo Kikuu wapi na wapi

lakini kwangu mimi Chunya kijijini Taasisi hazipo, hamna Taasisi hizi Chunya kwa hiyo Mkombozi ni Muswada huu, sasa Waziri Mwakyembe alikuwa wapi nimetofautiana naye kweli kweli, ulikuwa wapi ndugu yangu?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe *experience* yangu kwenye masuala mawili, matatu. Kwenye uchaguzi uliopita huu, nimekwenda Kata ya Matwiga naenda kuomba kura kwa wapiga kura. Nimekuta hapo mtu ananikimbilia wa jamii ya wafugaji anasema baba yake amekamatwa amewekwa ndani na Mtendaji. Anasema umeweka mifugo yako mahali ambapo haparuhusiwi *(tresspass)*, anasema Mtendaji, kama hukutoa shilingi milioni tano kwa mifugo yako hii nakupeleka Polisi kesho uende Mahakamani sasa dawa yake ni Muswada huu. Nilimfuata huyu Mtendaji kwenda kumuomba amuachie yule mfugaji kwa sababu mfugaji hana kosa na mfugaji hajui sheria akamtoa, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, juzi hapa niko Wilayani Chunya natekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, niko na Mkuu wa Wilaya anaitwa Bi. Rehema Madusa mchapakazi kweli huyu mama. Kuna Ma-*DC* ambao wanagongana na Wabunge lakini mimi na *DC* huyu tuko kitu kimoja. Ameniita anasema, Mbunge njoo kuna tatizo, tatizo gani? Anasema kuna wafugaji wametoka wilaya nyingine wamekuja huku, wanakula mazao ya wakulima, wameshikiana mikuki wanataka kupigana, tumeita Kikao mimi niko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikamwambia Mkuu wa Wilaya tatizo hapa ni Mwenyekiti wa Kijiji. Mwenyekiti wa Kijiji anawaita wafugaji njooni wekeni mifugo yenu hapa, wanampa chochote, anawaruhusu. Kumbe ardhi ile siyo ya wafugaji ni ya wakulima. Kwa hiyo, tatizo kubwa katika ugomvi ambao nimeuona hapa nchini wa wakulima na wafugaji ni aidha Mtendaji au Mwenyekiti wa kijiji. Sasa hawa wakulima wetu, wafugaji wetu sheria hawajui, huu ndiyo tiba yake, muarobaini wake ndiyo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwambia vijijini kama kwangu mimi Chunya, mfugaji awe wa kabila lolote awe Msukuma au awe nani hajui sheria kabisa kabisa. Anachoambiwa na Mwenyekiti, anachoambiwa na Mtendaji ndiyo hicho hicho. Sasa huu ndiyo tiba yake hiyo. Nakushuru sana Mheshimiwa Mwakyembe umeuleta pamoja na kwamba nimekulaumu, lakini pia nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haki za binadamu, Mheshimiwa Ritta leo asubuhi alikuwa analalamika anasema Mkoani Iringa watoto wadogo wanabakwa sana. Kwanza Mungu alivyomuumba mwanadamu, Mungu akatofautiana na Malaika mmoja. Huyo Malaika amekuwa Shetani. Imefika Watanzania siku hizi wanatenda mambo ambayo hata Shetani anashangaa. Unaendaje kubaka mtoto wa miaka mitatu? Shetani mwenyewe hajawahi kutenda dhambi kama hiyo, hajawahi anawashangaa wanadamu na ndiyo maana labda hata mvua tunakosa kwa sababu tunatenda mambo ambayo hata Shetani hatendi. Sasa wanaobaka watoto muarobaini wao ndiyo huo umefika. Wanawaonea wananchi, haki za binadamu, muarobaini wao umefika. Wanaowaonea akinamama kwenye mirathi muarobaini wao umefika, wanaowaonea wakulima na wafugaji kwenye ardhi yao, muarobaini wao ndiyo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana, nasema hawa watakaoteuliwa kwangu mimi, hawa wasaidizi watoa msaada bila malipo, Mawakili bila malipo; watakaokuwa kwangu Chunya nimefurahi Mheshimiwa Waziri amesema tayari wameshapata mafunzo kwa hiyo, iliyobaki ni kusajiliwa na waanze kazi. Mimi kwangu Chunya watakaoanza, nina mambo mawili; la kwanza nitaomba Kamati yangu ya mfuko wa Jimbo tuwanunulie pikipiki ya kuweza kusambaa vijijini kwenda kutoa msaada kama huu. Kama haitawezekana mfuko wa Jimbo kutoa fedha hizi, mimi nitatoa hela yangu ya mshahara niwanunulie pikipiki ili waweze kutoa msaada huo wa sheria kwa wananchi wote wanaotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hata sura yangu inaonesha nimefurahi sana Muswada huu kuja sasa hivi. Naomba Wabunge wenzangu wa vyama vyote tuunge mkono upite haraka iwe sheria ili tuweze kuwasaidia wananchi ambao wananyanyaswa, wanateswa kwa sababu tu hawajui sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambalaswa. Mheshimiwa Anna Gidarya simuoni. Nadhani Mheshimiwa Susan Lyimo badala ya Mheshimiwa Anna Gidarya. Mheshimiwa Susan Lyimo. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana. Kwanza natoa pongezi kwa Chama changu kwa kuweza kupiga magoli mengi kule magoli 19 kwa 1 na pia nawapongeza Wabunge wote hasa ndugu yangu Juma ambae ameweza kushinda kwa kishindo kule Unguja-Dimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kwa kweli ni muhimu sana na Muswada huu kama walivyosema wenzangu kwa kweli umechelewa sana. Ni Muswada ambao unalenga watu ambao hawana uwezo wa kupata huduma za kisheria. Ni Muswada ambao utaweza kusaidia watu wengi sana masikini, walemavu na kila watu na wafungwa ambao hata wako kule Magerezani ambao wanashindwa hata kuandika nanihii za kukata rufaa ambao wamejaa na ambao huwezi kusema kwamba kweli wote wamefungwa kwa makosa hayo lakini wana-*right* ya kukata rufaa lakini wanashindwa kutumia rufaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba Muswada huu umepanua wigo na umepanua wigo wa kuleta watu wengi kuweza kudai madai yao kwa kufuata sheria hii na nasema umepanua wigo kwa sababu ukifuata sura, Muswada ambao ulikuwa unatoa mamlaka kama haya kwenye sura ya 21 ambayo ni sheria ambayo ni *The Legal Aid* ambayo ilikuwa inatoa kwa ajili ya sheria ya makosa ya jinai pekee sasa hivi Muswada huu umepanua wigo na unatoa siyo makosa ya jinai ya mauaji tu au wale ambao wamehukumiwa kifungo bali unakwenda mpaka kutoa kwenye kesi za madai. Pia Muswada huu siyo kwamba utatoa huduma Mahakama Kuu tu, lakini Muswada huu unakwenda mpaka kwenye Mahakama za Wilaya, kwa hiyo ni Muswada ambao unatakiwa kupongezwa na ambao ni lazima tuangalie namna ya kuupitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo yote hayo, lakini nimepata wasiwasi wa mambo kama matatu hivi ndani ya Muswada huu. Ukiuangalia Muswada huu utaona kwamba mara utakapoanza kutumika wananchi wengi sana watakuja kudai huduma hiyo. Wananchi wengi watataka huduma za Mawakili, watataka huduma za hizo Taasisi ambazo zimeandikishwa kwa ajili ya kutetea haki zao. Sasa najaribu kuangalia wigo wa kesi ambazo ziko katika Mahakama zetu, wigo wa kesi chukulia kesi ambazo ziko Mahakama ya Wilaya tu au chukulia kesi ambazo ziko Mahakama kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu wengi ambao wako pale watataka hiyo huduma ya Wakili ambao atakuja kunanii sasa utaona kwamba kuanzia kifungu cha 21 mpaka 36 nimejaribu kukiangalia lakini sijaona sehemu ambayo Muswada huu umeelekeza ni makosa ya aina gani ambayo yatataka kupata

msaada huu. Sasa ukiacha hiyo vinginevyo itakuwa ni *chaos* kwa sababu kila mtu atataka kupata msaada huo na makosa ambayo yanatakiwa yapatikane msaada huo hayakuainishwa kwenye sehemu yoyote ile. Kama ni lengo la Serikali kwamba makosa ambayo yataainishwa yawe yanatakiwa kupata msaada yatatengenezwa kwenye kanuni, sijaona pia Mamlaka (*provision)* yoyote ambayo imeipa bodi, kuishauri kutengeneza hizo kanuni ili kuainisha ni makosa gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kuishauri kwamba ni lazima basi pawepo na *provision* ambayo itaipa Mamlaka Bodi ya kuhakikisha kwamba inachambua ni makosa gani ambayo yanahitajika kutolewa msaada huu vinginevyo itakuwa ni *chaos* na itakuwa ni watu wengi ambao watahitaji huo msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa sababu niliangalia sheria mbalimbali na nikakuta sheria ya Afrika Kusini ambayo imetoa uwezo kama huo kwamba imetoa uwezo kwa bodi na bodi ile wametengeneza *regulations*, wame-*identify* makosa gani ambayo yanatakiwa yapewe msaada na ndiyo ambayo yanafuatwa, kwa hiyo na hapa ningeshauri pia na sisi tungeiga hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika la tatu, ambalo naliona, ukiangalia sheria ya 21 ambayo imefutwa, sheria ile imetoa madaraka kwa Mawakili ili Msajili wa Mahakama Kuu ndiyo ambaye anaweza kuchagua ofisi yoyote ya Uwakili kumwakilisha yule ambaye ameomba kuomba huduma hiyo ya msaada ambao anautaka. Kwa hiyo, ofisi yoyote ya Wakili ambayo imeandikishwa basi ilikuwa ina utaratibu kwamba hata kama ni Wakili wako mikoani walikuwa wanaamriwa kwenda kutetea hizo kesi za mauaji au zile ambazo zina adhabu ya vifo sasa ilikuwa *centralized, registrar* alikuwa na madaraka hayo, lakini ukiangalia kwenye hii sheria inasema kwamba mtu ambaye anahitaji kutoa huduma za kusaidia basi inabidi aombe kwenye bodi. Kwa hiyo, ina maana kwamba Taasisi zote ambazo zinataka kutoa huduma, ofisi za Mawakili ambazo zinataka kutoa huduma hii inabidi ziombe kule kwenye bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tatizo ambalo naliona ni kama ofisi hizi zisipotaka kuomba itakuwaje kwa sababu sasa hivi sheria ambayo ipo ya sura ya 21 Mawakili hawaombi, wanaamriwa kwa sababu ni Maafisa wa Mahakama wanaamriwa kwenda na bado hapo hapo wanakwenda kwa kinyongo kwa sababu fedha ambazo wanalipwa ni kidogo sana kwa kila kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia sura hii utakuta kwamba Wakili sasa hivi analipwa kwa kesi elfu 40, elfu 60 sasa utakuta kwamba ni hela ndogo

sana na hakuna *motivation* ya kuwafanya Mawakili au ofisi hizo ziombe. Sasa kitu gani ambacho sheria hii imekifanya ambacho kitawafanya Mawakili waweze kuomba au Taasisi zinaweza kuwafanya kwamba wakimbilie kuomba ili kutoa huduma kwa hawa ambao watatakiwa kupewa hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe kwa sababu hawezi wakili akapoteza muda wake wote pale hajui atalipwa nini ndiyo anayekwenda kutoa msaada lakini analipwa nini? Kwa hiyo sheria hii haikugusa chochote. Naomba kwamba Waziri aliangalie hilo na atakapokuja ku-*sum up* aweke kipengele hicho vinginevyo nitaleta mapendekezo ya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, ni suala ambalo sasa hivi hii itakuwa ni ofisi kubwa sana, itakuwa ni *institution* kubwa sana. Haitakuwa kwenye kiwango cha bodi kama hivi ambavyo sheria inasema, haitakuwa kwamba ni mwakilishi mmoja tu kama ni *Paralegal* ambao wako kule wilayani basi hao hao ambao watafanya kazi. Sasa hiki ni kitu ambacho kinatakiwa pawe na *independent board, institutions* ambayo itashughulika kabisa na suala hili la kutoa hizi huduma. Hapa amezungumza Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambayo ni mifano ambayo iko kwenye nchi nyingine. Nchi nyingine *South Africa* wana-*independent board, institutions* kabisa ambayo inatoa hii misaada kwa watu wote ambao wanahitaji huduma za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kusema kwamba tunaweka ki-*board* tu au Wakala tu, ni lazima pawe na ofisi *special office* ambayo itatoa hizi huduma vinginevyo tutakuwa tunafanya masihara masihara tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na naunga mkono mapendekezo ambayo yametolewa na Mwenyekiti wa Kamati kwamba ufafanuzi wa baadhi ya mambo ya Mwanasheria ni nani? *Paralegal* ni nani? Sheria hii ita-*cover* Mahakama zipi? Lazima ufafanuzi huo utolewe kwa sababu imeacha wazi, mtu anaweza kusema nataka kwenda hata *Primary Court,* jinsi mapendekezo haya yalivyo ina maana ana-*cover* mpaka *Primary Court,* kwa hiyo ni lazima ufafanuzi huu utolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja baada ya marekebisho hayo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nadhani mlisikia taarifa ya Spika jana pia na leo kuhusu changamoto ya muda. Siku hizi ambazo kabla ya tarehe 3 ambapo leo tumekubaliana kutengua kanuni, muda tunaendelea nao kama Bunge la kawaida ama kama tulivyozoea kwisha saa saba na kuanza saa 11.

Sasa kwa mfano sheria ya leo ama Muswada wa leo unatakiwa kwisha leo maana yake kila mchangiaji akichangia kwa dakika 15 tutakuwa na saa moja tu ya kuchangia na wachangiaji wanne. Kwa sababu hiyo Waheshimiwa Wabunge napendekeza kwamba kama tutakubaliana, watu wachangie dakika 10 hilo ni la kwanza.

La pili, nataka kutumia kanuni ya 28(2) ili tuweze kupata watu kidogo wa kuchangia, sasa kanuni hii imeweka masharti ya nikitaka kuongeza nusu saa kulihoji Bunge. Kwa hivyo, nitawahoji. Kwa hiyo, liko katika utashi wenu kama wa kuchangia waongezeke ama watatosha hao wanne tutakaporejea jioni.

*(Hoja ilitolewa ili iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa, nadhani tumekubaliana kwamba tutarudi baadaye. Waheshimiwa Wabunge mmekataa kuendelea na Bunge kwa hiyo tutaendelea baadaye sasa mbona mnapiga kelele tena?

Sasa nitawataja watakaochangia baadaye. Tutakuwa na Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Anatropia Theonest hao ni wachangiaji watatu. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. Mheshimiwa Susan nilipokutaja ulikuwa haupo nikamtaja Mbunge mwingine, kwa hiyo nataja hawa waliopo sikujua kama umesharudi ili nikurudishie nafasi yako kwa hiyo Wabunge wanne waliotajwa ndiyo watakaochangia baadaye. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, niliombwa mwongozo na Mheshimiwa Heche leo asubuhi. Baada ya kupitia Kanuni na yale aliyokuwa ameyataja Mheshimiwa Heche kuhusu hali iliyopo Kagera kwenye tetemeko na kwamba kuna Wananchi wanalala nje. Mheshimiwa Heche aliniomba mwongozo kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) ambayo inaweka masharti kwamba kiti ama Spika atatoa mwongozo kwa kutumia kanuni hii pale ambapo jambo litakuwa limetokea Bungeni mapema. Kwa sababu hiyo mwongozo wangu, namshauri Mheshimiwa Heche atumie kanuni nyingine kwa ajili ya kuhakikisha jambo hilo

linashughulikiwa ipasavyo, lakini kanuni ya mwongozo inahusu mambo yaliyotokea mapema Bungeni.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.

*(Saa 8.40 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na michango. Tutaanza na Wabunge niliokuwa nimewataja kabla hatujasitisha shughuli za Bunge. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nikutakie mwenyewe kheri ya mwaka mpya, Mawaziri wote, Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kufanikisha kuingia mwaka 2017. Tunapenda kumshukuru Mungu kwa pamoja kwa kutupa uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie hoja ya Muswada wa Sheria wa *Legal Aids.* Muswada huu Waheshimiwa Wabunge umekuja wakati muafaka na ni Muswada muhimu sana kwa wananchi wote wa Tanzania ambao utasaidia kuwawezesha kupata haki zao muhimu kuanzia akinamama, watoto, vijana, walemavu na watu wote wa Tanzania, Muswada huu umekuja wakati muafaka kwa sababu watu wengi wamekuwa wakikosa haki zao za msingi kwa sababu tu hawajui watazipata wapi au hawana uelewa wa kutafuta hizo haki zao. Sasa kuleta Muswada huu kwa wananchi wa Tanzania ni muhimu na utawasaidia wengi kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko haki zao za msingi za wananchi wa Tanzania ambao wamekuwa wakizikosa kila siku. Mfano mdogo tu, mtu anaweza akakamatwa na polisi asipelekwe Mahakamani kwa muda wa siku tatu wakati Sheria inasema kwamba mtuhumiwa anapokamatwa na polisi anatakiwa ndani ya masaa 24 awe amepelekwa mahakamani. Hata hivyo, kwa sababu mtu anakuwa hajui kwamba ana haki ya kudai kwamba kwa nini sijapelekwa mahakamani na nimeshakaa hapa kituo cha polisi kwa muda wa

siku tatu; kwa sababu anakuwa hajui jinsi sheria inavyosema, anafikiria kwamba ni haki kwa polisi kumshika mtuhumiwa na kumweka pale kituo cha polisi kwa siku tatu bila kumpeleka mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa na Muswada huu, watu wengi watapata elimu. Ukija pia upande wa akinamama, akinamama wengi wamekuwa wanakosa haki zao za msingi kwa sababu tu hawazielewi na hawajui jinsi ya kuzitafuta. Kwa kuwa na Muswada huu, akinamama wengi wataamka, watafahamu haa! Kumbe hata mimi nina haki hii! Mfano mdogo tu; mama anaweza akafiwa na mume wake lakini unakuta kwamba kikao cha familia kinakaa, kina-*control* ile mali ambayo imeachwa na mume wake wakati mama huyo ana haki na ile mali na wakati sheria inasema kwamba sio lazima mama awe anafanya kazi na mume anafanya kazi ndiyo aweze kupata zile haki za msingi. Kitendo tu cha mama kuchemsha maji ya moto na kumchemshia bwana chai asubuhi kina-*contribute* kumfanya yule bwana aende kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea kwamba yule bwana amefariki unakuta vikao vinakaa na kudai kwamba yule mama haku-*contribute* kitu na kwamba yule mama si sehemu ya ile mali. Kwa kuleta Muswada huu, akinamama wengi wataelimika, wataelimishwa. Kwa sababu inakwenda mpaka vijijini unakuta kule vijijini akinamama wamekuwa wakidhulumiwa. Unaweza ukakuta mume wake alikuwa anamiliki shamba lakini anapofariki kikao cha ukoo kinakaa na kinadai kwamba mwanamke huwa harithi ardhi. Hii ni ardhi ya ukoo, kwa hiyo, mwanamke haruhusiwi kuitumia. Lakini kwa kuwa na Sheria hii, akinamama wengi wataamka, wataelewa jinsi ya kwenda kudai hizo haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija pia kwa upande wa watoto. Watoto wengi wamekuwa wanadhulumiwa. Utamkuta baba anazaa mtoto wa nje, anapomzaa yule mtoto wa nje anamtelekeza; kwa kuwa na sheria hii, wale watoto wataelimishwa jinsi ya kudai haki zao kwa sababu mtoto wa nje mara nyingi anaambiwa kwamba yule mzazi akifa hawezi kurithi mali. Ukija kwenye sheria zote, Sheria za Serikali na Sheria za dini zetu zinamhesabu kwamba ni mtoto wa nje. Hata kama akiwa Muislamu ataelimishwa kwamba “wewe mwambie baba yako akuandikie urithi” kwamba atakapokufa utarithi kitu fulani ili uweze kupata haki yako. Pia yule mtoto ataelimishwa kwamba mwambie baba yako akutambue kisheria kwamba wewe ni mtoto wake ili atakapokufa uweze kudai haki yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija pia kwa upande wa walemavu, utakuta majengo mengi humu nchini kwetu yanajengwa hayana miundombinu ya kuwawezesha wale walemavu kufika kwenye zile ofisi, lakini kama sheria zetu zitakaa vizuri na wale watafundishwa zile sheria jinsi ya kuzidai, wataifanya Serikali iweke sheria muafaka kwamba mtu anapojenga jengo kama ni hoteli lazima aweke miundombinu ya walemavu. Haki hii pia itakwenda pia kwenye magereza. Tumekuja kuona kwamba watu wengi ndani ya magereza wanafungwa na wanashindwa hata jinsi ya kuandika *appeal,* akija kwenda kuomba kwamba nataka ku-*appeal* kesi yako anaambiwa kwamba muda umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kupitisha Sheria hii, hawa ma-*legal aids* watakwenda kule magereza, watakuwa wanatoa elimu, wale wafungwa walioko kule magereza wataweza kujua kwamba "natakiwa nifuate *procedure* gani ili niweze ku-*appeal* kesi yangu". Hata wale pia watakaokuwa kituo cha polisi watafahamu kwamba hii kesi yangu natakiwa nifuate njia gani ili niweze ku-*appeal* kwenye hii kesi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu Muswada ndugu zangu, Wabunge wenzangu na Watanzania wote naomba tuunge mkono, umekuja wakati muafaka, wakati wa zama za utandawazi. yako mambo mengi, yako mambo ya ugaidi yanayoendelea duniani, naombeni tuunge Muswada huu mkono ili uweze kupita ili mwananchi wa kawaida aweze kusaidiwa kupata haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nauunga mkono Muswada huu, naunga hoja hii, nauunga Muswada huu naona umekuja wakati muafaka. Naomba na wenzangu muunge mkono Muswada huu ili wananchi wetu na watu wetu mpaka wa hali ya chini, vijijini mpaka huko kwenye Kata zetu waweze kupata ile elimu. Yako mambo mengi ambayo kwa mfano kwa mwanamke ziko sheria nyingi, Sheria za mpango wa uzazi, ukija kwenye mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu imeingia; mikataba ya wanawake kuna vitu vingi ambavyo wanawake hawavifahamu lakini ujio wa Muswada huu utawafanya wale waliosomea mambo ya wanawake na hizi Taasisi za *Legal Aids* ambazo sasa hivi tunazo kama hizo *TAWLA,* ambazo zinatoa msaada kwa sasa hivi, itazifanya ziende mpaka vijijini kuwaelimisha wanawake ili waweze kujua ile mikataba ya kimataifa inasemaje juu ya mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu, mwanamke anayo haki ya kupanga uzazi, sio lazima apite kwenye Wizara ya Afya akapange uzazi. Ziko Sheria za Kimataifa na *protocol* zake ambazo zinampa mamlaka mwanamke

kupanga uzazi kwamba anahitaji watoto wangapi. Ziko Sheria nyingine za Kimataifa zinampa mamlaka mwanamke anapoolewa hahitaji kubadili jina lake kutumia jina la mume wake. Kwa hiyo, vitu kama hivyo wanawake wanatakiwa waelimishwe na kuja kwa Muswada huu kutawafanya wale ambao wanazijuia hizo sheria waweze kwenda kule vijijini kuwaelimisha hao akinamama ili waweze kupata hiyo elimu ambayo itakuwa inatolewa. Sijajua zimebaki dakika ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia suala la wazee. Zipo Sheria za wazee ambazo zimepitishwa na Bunge hili Tukufu ambazo wazee kule vijijini hawazifahamu na wengine wala hawajui kwamba kuna Sheria ambazo sisi tumezipitisha. Kwa mfano tu suala la kwamba wazee wapate matibabu bure. Wazee wengi kule vijijini; kwanza unakuta zile hospitali zenyewe ambazo zina-*offer* hayo matibabu bure hazipo. Unaweza ukakuta mara nyingi ni zahanati za watu binafsi, kwa hiyo mzee anapokwenda pale inabidi alipe. Kwa ujio wa Muswada huu hawa watoa msaada wa kisheria wataweza kwenda mpaka vijijini ambako wataweza kuwaelimisha hawa wazee kwamba tazama zipo sheria ambazo zimepitishwa na Bunge ambazo mzee unatakiwa utibiwe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wale wazee itawasaidia wao kudai haki zao za msingi, kudai watibiwe bure na kuidai Serikali yao. Tukiangalia tu kwa mfano mdogo, nikija kwenye suala la watoto; tukiangalia kwamba nchi yetu ya Tanzania inao uhaba wa magereza za watoto. Watoto wanapofungwa, natoa mfano mdogo wa kule Arusha; iko nyumba imekodiwa ya mtu ambayo watoto huwa wakifungwa wanawekwa pale sasa inahesabiwa kwamba pale ni magereza. Nchi nzima hii ya Tanzania ina magereza matatu tu ya watoto wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii *legal aids* ikipitishwa, wale wanaofahamu mikataba ya kimataifa ya watoto wataweza kuwasaidia hawa watoto kudai mambo yao ya msingi na kuelewa kwamba ziko Sheria za Kimataifa ambazo zinam-*guide* mtoto na zinamlinda mtoto ili aweze kupata haki zake za msingi. Watakwenda mpaka kule vijijini tunawaona watoto wengi wanakosa kwenda shule, wanakosa chakula, wanakuwa wanatembea tembea tu mtaani, lakini ikipita hii *Legal Aids* wale watoa huduma wataweza kwenda kule vijijini watawaelimisha, wataweza kujua haki zao za msingi. Wataweza kujua kwamba hata kama sina mzazi natakiwa nidai haki zangu za msingi Serikalini na wataweza kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la wanafunzi; wanafunzi pia watafundishwa huu Muswada wa *Legal Aids,* wataelewa haki zao za msingi. Tunazo *education grants* na tunayo Mikataba ya Kimataifa ambayo inalinda pia inamlinda mwanafunzi, Walimu ambazo hawa *legal aids* ambao ni wataalam katika hayo masuala wataweza pia kuwafundisha hao watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hao *legal aids,* siwezi kuzungumzia tu suala la wanawake upande mmoja, wataweza pia kuwaelimisha wanaume ili waweze kutoa haki zao za msingi kwa watoto wao, wazee wao na kwa akinamama. Hawa *legal aids* wataweza pia kuwaelimisha zile sheria kandamizi ambazo zinamkandamiza mwanamke kama vile vipengele fulani fulani vilivyoko kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Ibara ya 13, 14 na 15 inaonesha kumuengua mtoto wa kike kumtofautisha na mtoto wa kiume. Ujio wa Sheria hii ya *Legal Aids* itawafanya wale *legal aids* waweze kuwafundisha wasichana waweze kuelewa na waweze labda kudai marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ili isiweze kuweka tofauti kati ya mtoto wa kiume na mtoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana tumeona mifano mingi. Mara nyingi hata kwenye shule, watoto wa kike wanapopata mimba wao ndiyo huwa wanafukuzwa shule; yule mtoto wa kiume anabaki shuleni anaendelea. Hata kama wanasoma shule moja unakuta kwamba yule mtoto wa kike ndiyo anayeharibikiwa, anafukuzwa shule lakini yule mtoto wa kiume yeye anabaki anaendelea na shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ujio wa Sheria hii utawafanya wale watakaokuwa wanatoa somo la hii *legal aids* na misaada hii ya Sheria kuwaelimisha watoto wa shule angalau sheria zikabadilishwa kama basi watoto wanasoma shule moja na imetokea matatizo, mmoja amekuwa mjamzito, basi wahusika wote wakae nje ya shule sio anakaa mtoto mmoja wa kike, wa kiume yule anabaki anaendelea na shule yule wa kike anakuwa ameharibikiwa na maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nisemee suala la watoto wa mitaani ambao pia nao wataweza kudai haki zao za msingi kwa sababu watakuwa wamepata elimu. Nimesemea suala la vijana, watadai haki zao za msingi. Watakuwa wamepata elimu, watasaidiwa. Mambo pia ya mifugo, mashamba, mkulima atadai haki zake, mfugaji atadai haki zake za msingi. Serikali itakuwa na sheria nzuri ambayo itaweza kutenganisha maeneo ya wafugaji na maeneo ya wakulima kwa sababu wakulima watapata elimu kutoka kwa hawa *legal aids…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Taska Mbogo. Ila nadhani wanawake watataka suala la majina uwaachie wafanye uchaguzi. Wengine tunapenda kubadilisha sisi wenyewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest ajiandae. Tutamalizia na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kusema kuna msemo wa kiingereza unasema kila kitu kinakuja kwa sababu zake na leo asubuhi tulipoanza hapa tulianza na swali kuhusu mambo ambayo yametokea Zanzibar ambayo ya upigaji, uoneaji, unyanyasaji wa wananchi na tukashuhudia Serikali ikisema hata haijui kwamba hayo mambo yanatokezea na ikasema kwamba mambo hayo hata hayajawahi kuripotiwa polisi na kwa hivyo wao hawajui chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *only two hours later* tunaletewa Muswada wa Msaada wa Kisheria kwamba upande mmoja haki zinavunjwa, watu wanakoseshwa haki zao, wananyanyaswa, wanapigwa, hakuna kinachoendelea lakini upande mwingine wanajitengenezea mazingira ya kulinda wananchi wake. Kwa maana hiyo tunaambiwa kwamba kuna raia wa namna mbili nchi hii. Kuna raia wa Zanzibar ambao ni haki yao kuonewa na Serikali kila siku kukataa na asubuhi nilisema hapa Bunge hili imefika wakati iundwe Tume, Waziri akakwepa hakujibu kabisa, lakini upande huu mwingine wanatengenezewa haki ya ku-*access justice*. Upande ule kule *justice is denied to them. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Katiba na Sheria na *natahasaf* kusema kwamba Muswada huu ni Muswada muhimu sana kwa ajili ya Tanzania na ningetamani Muswada kama huu baadaye uwepo Zanzibar. Umuhimu wake ni kwamba unatengeneza mazingira ambayo watu wetu kwa miaka wamewekwa nyuma sana, elimu ya uraia, elimu ya haki haijafikishwa kwao kiasi ambacho wengi wanadhulumiwa, wanaonewa bila ya kujua waende wapi au wafanye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge mmoja asubuhi hapa alimwambia Waziri wa Katiba na Sheria kwamba alikuwa wapi siku zote, lakini kila kitu kinakuja na wakati wake. Kila kitu na zama zake. Hata hivyo, mimi mwenyewe nilimwambia Mheshimiwa Waziri kama kwamba Muswada huu utakuja vizuri, utamjengea *legacy* yeye kama Waziri kwamba ameweza kuleta Muswada huu ambao unahitajika sana na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo moja ambalo litatukabili. Muswada huu unakiuka utaratibu wa Muswada wa mwaka 1969 ambao tulikuwa tunazungumzia masuala ya jinai peke yake. Hapa sasa tunakwenda pia masuala ya madai. Hapa maana yake tunafungua wigo mkubwa sana. Wenzetu Kenya hawakufungua kwenye suala la madai, wenzetu Malawi hawakufungua kwenye suala la madai, lakini sisi tumefungua kwenye suala la madai, maana yake sasa *administration* itakuwa kubwa, kazi itakuwa kubwa ya kufanya, elimu itahitajika kubwa sana, wakati ukweli kwa mujibu wa watu wenye uzoefu wa *legal aid* ni kwamba sehemu kubwa yale mashirika makubwa sana yanasimamia kesi kumi mpaka kumi na tano kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna mashirika machache sana ambayo yanafika sehemu kubwa. Tuna *paralegals* ambao watafika au wanafika mpaka vijijini. Hata hivyo, kuna tatizo hilo la kufungua upana mkubwa sana, wanasheria wanaweza wakasema *flood gates* sasa sijui kama nia yetu tutaweza kuitimiza kuchukua madai na jinai pamoja lakini maadam sheria inawekwa, wacha tuone itafanya kazi vipi, itasimamiwa baadaye. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sheria hii *is not the best that we could have done,* ingeweza kuimarishwa kwa sababu tumepata bahati hatuku *re-invent the wheel.* Mheshimiwa Tundu Lissu leo hapa amezungumzia historia ya Marekani ya miaka mingi ya *legal aid,* lakini tusiende mbali twende hapo Kenya tu, kama tungeweza kwenda ndani wenzetu wamefanya nini, wamekwama wapi? Nafikiri tungeweza kufanikiwa, lakini sheria hii imekuwa katika mchakato kwa zaidi ya miaka kumi hivi sasa, kwa bahati mbaya hawa Kamati ya Katiba inayosimamia hivi sasa haikupata fursa ya kujifunza wenzetu wengine wanafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu waliokwenda Afrika Kusini na kwengine kwenye Kamati hii wote wameondoshwa kwenye Kamati hii, kwa hivyo, hawakutuwezesha kupata uzoefu wowote ule ambao wameupata huko walikokwenda kufanya *study. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana asubuhi akapongezwa sana Mheshimiwa Tundu Liissu kwa sababu *he is the only surviving* na analazimisha kuja kwenye Kamati yetu tu, kwa sababu yeye siyo mjumbe wa Kamati yetu; lakini ametusaidia sana kwa sababu *he is the only surviving* ambaye alikwenda katika *training* au kufanya utafiti Afrika Kusini na akabakia kwenye Kamati hii. Kwa hivyo, kwa mfano Kenya, *board* inayosimamia haikufanywa kuwa *governmentally,* imefanywa kuwa ni *board* huru ina muhuri wake inaweza kushtaki na kushtakiwa na haiko moja kwa moja kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wamefanya Mkurugenzi wa *Board* anagombea kwa sifa; hateuliwi. Kwa hivyo, kuna ule uhuru wa *board* yenyewe, tumekuwa tuki-*force*, tunasema kwamba *board* hii inaweza ikafanya maamuzi ya kutetea watu, tunajiuliza je, ikitokea kwamba inayoshtakiwa ni Serikali au kosa lililopo ni kubwa kama kosa la uhaini, kosa la ugaidi huyu mtu ambaye; hii *board* ambayo mlolongo wake unakwenda mpaka kwa Katibu Mkuu na tuli-*attempt* hata katika Kamati hata kutaka kum-*distance* Katibu Mkuu lakini ikaonekana kama waleta hoja wakaona kama ni ngumu. Tukajiuliza inawezekana vipi katika hali kama hiyo, mtu kama huyu kutetewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho Kenya wamefanya ambacho mimi mwenyewe nilivunjika moyo, ni kujaribu kufanya ushawishi wa kwamba tuhakikishe tunakuwa na *legal aid fund;* ama kwa kuwa na sheria nyingine au itajwe kuliko ilivyosema *section* 37 ambayo inaelezea namna ambavyo pesa zitapatikana. Tunajua kuna shida ya ku-*approve* pesa hapa kwa mashirika haya ambayo ni kama yako pembezoni. Mwaka jana hapa tulilalamika sana watu wa katiba na sheria na hata tukataka kumtetea Mheshimiwa Waziri kwamba Tume ya Haki za Binadamu iongezewe pesa na mpaka mwaka huu haikuongezewa pesa hata ya kufanya *activity* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana tume mwaka mzima huu, itakuwa imekaa ofisini tu, najiuliza tulete mambo haya mengine, kwa maana nyingine tunaweza tukarudia yale yale tena tusiipe *legal entity,* fedha za kutosha na kwa hivyo haitofanya kazi za kutosha itakuwa kama ile Tume ya haki za Binadamu. Kwa maana nyingine watakuwa wanawategemea wale *legal aid provider's* ambao hao wanakwenda kuomba pesa kwa wafadhili wetu wa kawaida *traditionally founders* sijui wa-Sweden, wa- Norway ndio wanaotuendesha hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo ningependa kuona kwamba wale Wabunge wanakuwa *serious* katika Serikali itakapoleta pendekezo, wale wanaoshangilia hapa kwamba sasa watatetewa, watapata haki za kutetewa

na kitu gani waje waishike Serikali koo hapa mpaka hiki chombo kipate fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho Kenya wamefanya na sisi tungeweza kukifanya ni kwamba sheria yao iko *liberally* zaidi. Kwa mfano, wameweka utaratibu kwamba kila kituo ambacho ni *holding center* kama cha watoto, kama ni polisi au kama ni magereza kunakuwa na *form* za *readymade* zipo, mtu akifika kama vile Marekani unaposimamishwa unavyoambiwa haki yako ni moja mbili tatu, basi na hiyo iwepo, kwamba ukifika gerezani, ukifika polisi usomewe haki zako, halafu upewe *option* uambiwe kuna uwezekano wa kupata *legal aid*, unataka au hutaki, alafu iwe *recorded* katika *register* kwamba huyu kapewa fursa hiyo na ameikataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo Mheshimiwa Waziri akasema lakini hiyo itapita kwenye mamlaka nyingine, Wizara nyingine, tukasema Serikali inasemezana, wasemezane ili hili liwepo tuweze kujua kitu kizuri ambacho wenzetu wameweza kukifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho kilitatiza kidogo ni suala la pale mtu anayekwenda mahakamani lakini akashindwa kesi na kwa hivyo hapatakuwa na *cost* ambazo zitakuwa *awarded* na Mahakama na kwa hivyo ataondoka pakavu. Sasa sijui Waziri amekuja na pendekezo gani katika hili kwa maana mimi nilipenda *statement* yake moja alisema *issue* sio kum- *reimburse fully advocate* au mtu ambaye anakwenda kumtetea mtu lakini angalau arudie katika hali yake inayofanana kabla hajaenda kule kwa gharama aliyoipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametuletea *amendment* hapa inambana Wakili, Wakili atakwenda mahakamani, tunajua sasa hivi aibu kusema hivi sasa anapata kiasi gani, lakini atakwenda mahakamani pengine akishinda kesi, atakuwa *awarded cost* ambayo tulisema ziwe *awarded* sio kwa yule ambaye alitetewa lakini ziwe *awarded* kwa Wakili, lakini akishindwa *case* anaondoka patupu, sasa huyo sijui hii imefikiriwa vipi kuweza kuhakikisha kwamba inawezekana kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho kabisa ni suala zima la namna ambavyo sasa hivi tulipigania kwamba wale ambao sasa hivi wapo wana-*exist* sijaona *schedule of amendment* lakini tumesema wale ambao wana-*exist* sasa hivi wasiwe *labored* ku-*register* upya. Moja kwa moja wachukuliwe kwamba wao *automatically* ni *legal providers* na wachukuliwe wawe *registered* moja

kwa moja. Wasiwe *labored* kuanza tena ku-*apply* kwa sababu uki-*apply* ina maana mwenye mamlaka anaweza kukukatalia au anaweza kukubalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na nitafurahi kama Muswada huu utatendewa haki ya yale marekebisho ambayo tuli-*suggest* katika Kamati na naamini utaweza kusaidia sana Watanzania hasa wale wanyonge. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, nimejulishwa badala ya Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa atachangia Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote nitaomba kutumia muda wangu kuomba ufafanuzi kutoka kwako utatuambia muda utakaoona unafaa; ni muda gani tunaweza kuleta *schedule of amendment* kwa sababu tumeleta *amendment* zetu tukaambiwa tumechelewa. Kwa kuwa suala la utungaji wa sheria unahitaji *consensus,* kwa hiyo tunaomba tujue lini tulete ili kwa pamoja tutunge sheria. Badala ya kubaki wengine na manunguniko kwamba tulikuwa na mapendekezo yetu na hayajaweza kuwa *accommodated,* naomba hilo ulichukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye Muswada, katika nia njema ya kutaka twende pamoja,tuwe na uelewa mmoja, nina mapendekezo kadha wa kadha ambayo Waziri akiona yanafaa, anaweza kuyachukua. Mfano tukianza na kifungu cha 4(2) kinaongelea *members wa board,* tukienda kwenye *schedule* yake ambayo iko ukurasa wa 23 anaongelea *composition* ya *board members.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa sana ni kwa namna gani *Tanganyika Law Society* inaweza isiwe mdau katika hii *board.* Ningependekeza wao kama watu ambao wana *mandate* au wanalinda maadili au wako *concerned* na maadili ya hao Wanasheria na Mawakili wawe sehemu ya kikundi hiki au wawe sehemu ya *board* katika Muswada huu tunaoupendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili ambacho nimekiona ni cha msingi kipengele cha sita (6) mnaongelea nani awe *Registrar;* sina wasiwasi na sifa za *Registrar* kwa sababu inaonekana atatoka atakuwa ni mtu ambaye amekuwa ana-*deal* na *legal affairs* sina shida na hiyo. Maana yake atakuwa na *background* ya kisheria na suala analoenda ku-*deal* nalo kimsingi lina-*deal* na mambo ya sheria. Swali langu linakuja kwa *assistant registrar* ambaye inakuja

kipengele cha 8(1) kinaongelea wale ma-*assistant registrar* watachukuliwa kwenye wilaya na mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipengele hiki hakioneshi umuhimu wa kuwa na watu ambao *background* zao ni za kisheria, naona huu ni upungufu na kama tunaona inafaa tuongeze neno kwamba wachukuliwe watu ambao wamekuwa wana-*deal* na *legal affairs* kwenye Ofisi za Wakuu wa Wilaya, kwenye Ofisi za Wakuu wa Mikoa kuna watu wenye *background* za kisheria tuwatumie hao watu wanaweza ku-*play role* nzuri na tukapata matokeo tarajiwa zaidi ya kuchukua *just anybody*. Hayo ndio mapendekezo yangu katika kipengele cha nane (8).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi nakuja kipengele cha 14, ambacho kinaongelea mamlaka ya rufaa, kwamba mleta maombi sasa maombi yake yasipokubaliwa, *Assistant Registrar* akikataa maombi yake anaweza ku-*appeal* kwa *Registrar*. *Registrar* akikataa anaweza ku-*appeal* kwa *board, board* ikikataa ana-*appeal* kwa Waziri na huo ndio mwisho wa mamlaka husika, nadhani hii hapa tume-*over look* Waziri hawezi kuwa *final say*. Ni rahisi sana unaweza ku-*corrupt the whole population* ambayo tunayoongelea, lakini siyo rahisi ku-*corrupt the High Court*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza *High Court* iwe ndio ya mwisho badala ya kuishia kwa Waziri. Vinginevyo tutakuwa tunaanza kutengeza vitu ambavyo havitakaa vizuri na vitaleta manunguniko; kama mnaona inafaa Mheshimiwa Waziri nashauri tuiongeze hiyo kitu, japo nimeileta nimeona mwenzangu ameleta kwenye *schedule of amendment* mkiichukua hiyo inaweza ikatuleta matokeo chanya katika kile tunachokitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 16 ambacho nimeona ni kizungumkuti, kipengele kidogo cha 3(f) kinamzuia *a legal aid provider* kutojihusisha na *any political activities,* kikisomwa sambamba na kipengele cha 43 asijihusishe na mambo ya kisiasa. Tunataka *definition,* ni mambo yapi ya kisiasa mnayaongelea, tunataka uelewa wa pamoja, mambo yapi ya kisiasa tunayaongelea, kwa sababu ninachoweza kuona nimeona watu wakifanya mambo ya kisheria, wakitoa msaada wa kisheria ni Mawakili nguli na maarufu nchini bado wanafanya mambo ya kisiasa, sasa tunataka uelewa wa pamoja. Isije ikawa ni changa la macho kwamba kuna watu wanabanwa au kuna watu wataanza kuonewa ati wana milengo fulani ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo kama hatuwezi kuwa na uelewa wa pamoja katika hilo nitaona tuna lengo la kuonea watu kadha wa kadha au kuna vitu tunajaribu kujificha nyuma yake tukitumia mlengo wa kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 20, ni *special provision paralegals*. Hawa *paralegals* inaelezea ni watu gani, lakini imeenda imejikuta hiki kipengele cha 20 kinatoa vitu viwili ambavyo vina-*contradict one another*. Mfano kipengele cha 20(2)(c) kinamwelekeza *paralegal* kutoa msaada wa kuandaa *legal document* na hiyo kimsingi ndio kazi yake kama msaidizi wa masuala ya kisheria anaandaa *document*. Sasa ni wakati gani *paralegal* ataachana na kazi anayofanya *advocate*. Mmeenda kwenye kipengele cha 3(5) mnasema *paralegal* asijihusishe na mambo yanayofanywa na *advocate* mnaona *contradiction.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 2(b) kinamruhusu kuandaa *legal document,* lakini tunaenda kipengele cha (5) kinasema asijihusishe na mambo yanayofanywa na *advocate;* ambayo naona *there are two contradicting things* hapa. Mnamwambia andaa *legal document* lakini *at the same time,* mnamwambia asijihusishe na mambo yanayohusiana na mambo ya kisheria. Lazima tuangalie kipi sasa kisimame, kipi kiondoke na nikipishe kingine kuliko kwenda na hivi viwili ambavyo vinatuletea *contradiction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 36 kimeeleza vizuri, kutoa msaada wa watu ambao wapo kwenye mahabusu. Mara nyingi tumeona watu ambao wanakuwa wamekamatwa, wapo chini ya polisi watu ambao wanapaswa kuandika maelezo yao, wamekuwa haki zao hazifuatwi, ikiwa ni pamoja na kupewa aidha mwanasheria au *legal aid for this matter*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba hiki kipengele kiwekwe basi, hata kwenye kesi za mwenendo wa makosa ya jinai, ili wale mawakili au wanasheria au ma-*paralegals* wawepo wakati mtuhumiwa anahojiwa na polisi. Kitu ambacho hakifanyiki leo, watu wanaku-*harass,* watu wanatishwa na mawakili wakifanikiwa kuingia mle ndani wanaambulia matusi na kejeli na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano iko dhahiri, tunakumbuka kilichotokea kwa mawakili kule Arusha kwenye kesi ya Loliondo, *it is the same thing,* wakili amejitolea kwenda kwa mteja wake kumsikiliza na yeye amewekwa ndani. Kwa hiyo, kama kweli tuna nia ya dhati ya kutoa msaada wa kisheria kwa watu hawa basi hivi vipengele tuvifuate kadiri ambavyo tumeviweka kwenye Miswada yetu au kadri tulivyoandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nataka tuongee bayana hata hizi faini ambazo tumewaweka watu, unaona faini zinakuja *five milions, ten millions, six months;* au faini ya *five billions* mpaka *ten millions* au *six months* tuangalie *relationship*. Mtu ambaye amechukua pesa, kwa mfano kama huyu *paralegal* ambaye amechukua fedha kwa mtu anayemsaidia; mnamwambia kama amechukua fedha kwa mtu anayemsaidia faini yake, iwe ni miezi mitatu ngoja nirudi vizuri hapa; nataka tupate uhusiano mzuri kati ya faini, kati ya fedha zinazotozwa na kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusifanye kwa ajili ya kuwakomoa watu au tusifanye vitu kwa ku-*beep* watu watakuwa wanaomba pesa kwa wahisani wanaona vifungo au faini ni vidogo, wanapiga pesa nyingi lakini wakijua kwamba wanaenda kulipa kitu kidogo. Nataka tupate uhusiano kati ya faini na makosa yanayofanyika. Nakushukuru, nimemaliza *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana ambao ni Muswada wa huduma ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme naunga mkono Serikali kuleta Muswada huu kwa asilimia mia moja na kwa mtazamo wangu ni kwamba Muswada huu umechelewa sana kuletwa. Ulipaswa kwamba uwe umeshaletwa siku nyingi sana, kwa sababu ni Muswada muhimu sana sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu, kwa sababu ni Muswada unaokwenda kusaidia wananchi wetu ambao kimsingi hawana uwezo wa kulipa gharama za mawakili na wanahitaji kupata huduma za kisheria. Pia wote tunafahamu kwamba matatizo ya kisheria ambayo yanaweza kumfanya mtu ajikute yupo mahakamani kwenye mkondo wa kisheria yanaweza kumkuta mtu yeyote yule, bila kujali hali ya kiuchumi, au hali yoyote ile. Pia kuna ushahidi wa kutosha kwamba kuna wananchi wetu wengi tu ambao wamejikuta wanapata matatizo ikiwemo hata kuhukumiwa kufungwa, lakini kimsingi ni kwa sababu tu hawakupata msaada huu muhimu wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kutoa mchango wangu kwa baadhi ya vifungu vya Muswada huu, ambavyo naona inabidi viboreshwe. Muswada huu unakwenda kuwatambua kisheria taasisi ambazo zitakuwa zinatoa huduma za kisheria na ndani ya taasisi hizi kutakuwa na mawakili

kutakuwa na wanasheria na kutakuwa na wasaidizi wa kisheria ambao wanaitwa *paralegals*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa *paralegals* wasaidizi wa kisheria sasa hivi tunao lakini Muswada huu ndio unakwenda sasa kuwatambua kisheria na hawa wako maeneo karibu yote ya vijijini, wilaya zote kwenye kata mpaka vijijini, sasa hivi wapo lakini Muswada huu unakwenda kuwatambua kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo naomba liboreshwe kwenye kifungu cha 19 ni sifa za hawa ma-*paralegal* (wasaidizi wa kisheria) ambao kimsingi wako maeneo yetu ya kata na vijijini kule. Muswada unasema kwamba hawa wasaidizi wa kisheria watakaokuwa wanakaa na wananchi huko vijijini na kimsingi watakuwa wanatoa usaidizi huu wa kisheria bila kuwatoza gharama wale wateja wao wanaohitaji msaada kisheria, sheria inataka wawe na sifa zifuatazo; wawe na *degree* ya sheria, wawe na *diploma* ya sheria, wawe na *certificate* ya sheria.

Mheshimiwa Spika, sipingi vigezo hivi, sipingi wawe na *degree, diploma* au *certificate* lakini nilikuwa naomba tuboreshe, kwamba tusibague wale ambao wana elimu chini ya hapo. Kwa mfano watu ambao wana elimu ya kidato cha nne na darasa la saba; kwa sababu katika Kamati tuliita wadau mbalimbali na baadhi ya wadau hawa zilikuwa ni taasisi ambazo tayari sasa hivi zina ma-*paralegal,* zina hawa wasaidizi wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata ushuhuda kwamba sasa hivi nchi yetu tuna wasaidizi wa kisheria, hawa ma-*paralegal,* waonaweza wakafika takribani 9,000 nchi nzima wamesambaa kwenye kata na vijiji, na walio wengi elimu yao ni kidato cha nne na darasa la saba, na kuna maeneo mengine wengine hawakumaliza hata darasa la saba, ilimradi wanajua kusoma na kuandika, lakini pia wamepata mafunzo ya kisheria ya kuwa *paralegal.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliweza kupata mfano wa *paralegal* mmoja, (msaidizi wa kisheria) ambaye alikuwa maeneo ya watu wa kabila la Wahadzabe ambaye aliweza kuwasaidia Wahadzabe wenzake wasiweze kudhulumiwa ardhi na mwekezaji, wakati huyu ni *paralegal* ambaye amepewa mafunzo na hajakwenda shule hata darasa la saba na kimsingi anajua tu kusoma na kuandika na amepewa mafunzo ya u-*paralegal.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mapendekezo yangu hapa ni kwamba sawa wawe na *degree,* wawe na *diploma,* wawe na *certificate,* lakini tusibague wale wa kidato cha nne, wale wa darasa la saba, hata wale

wanaojua tu kusoma na kuandika ilimradi katika maeneo yao wanaweza wakapata mafunzo ya kisheria na wakatoa huduma za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizingatia hawa ma-*paralegal* (wasaidizi wa kisheria) ni watu ambao wanaishi vijijini na jamii kule kule. Kwa hiyo, tuki-*restrict* sana, *degree* na *diploma,* tunaweza tukawaengua watu muhimu sana ambao wangeweza kusaidia wananchi wetu katika maeneo ya vijijini na maeneo ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho napendekeza mabadiliko ni kifungu cha 27(b). Kifungu hiki kinawapa mamlaka Majaji na Mahakimu kuamua kesi inapokuja mbele yao kuweza kufanya *analysis* na kuona kwamba huyu mtu anahitaji msaada wa kisheria na kuagiza Msajili amtafutie usaidizi wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza haki hii ifikishwe pia kwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata. Kwa sababu watu wetu wa vijijini kule wana mashauri mengi, mengine yanahusu ardhi, migogoro ya ardhi, ambayo hawaendi mahakamani kwanza, wanaenda kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata. Kwa hiyo, wale Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi za Vijiji na Kata hata Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya pia sheria hii iwape uwezo wa kuona kwamba shauri hili linahitaji msaada wa kisheria au shauri hili halihitaji msaada wa kisheria. Kwa hiyo, isiishie kwa Majaji na Mahakimu peke yao, bali uwezo huu upelekwe mpaka kwa Wenyaviti wa Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho napendekeza maboresho ni kifungu cha 49(2). Kama kilivyo sasa kwenye muswada kinasema kwamba baada ya sheria hii kupitishwa na kuwa sheria, wale wote ambao sasa hivi wanatoa huduma ya msaada wa kisheria baada ya miezi 12 wanatakiwa wasimamishe huduma zao waombe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ikibaki kama ilivyo kuna hatari ya wananchi ambao sasa hivi wanahudumiwa na ambao baada ya miezi 12 kesi zao zitakuwa hazijaisha kukosa haki ya kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ni kwamba muswada huu wa sheria utambue kwamba wale wote ambao ni taasisi halali zinazotoa *legal aid* sasa hivi sheria hii mpya izitambue *automatically,* kwamba waendelee kutambulika na sheria mpya kuwa ni watoa huduma halali wa msaada wa kisheria badala ya kuwaambia kwamba baada ya miezi 12 wajisajili upya kwa sababu kitendo cha kujisajili upya kinaweza kikafanya shughuli zao zisimame na

zile kesi walizokuwa wanaendelea nazo ziishie hapo; italeta usumbufu na kukosesha haki wananchi wetu ambao tayari walikuwa na mashauri ambayo yanaendelea kuhudumiwa.

Kwa hiyo, sheria hii mpya iwatambue *automatically* na waendelee kutoa hizo huduma muhimu za kisheria ambazo wananchi wetu kwa kweli wanazihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho napendekeza kifanyiwe maboresho ni kifungu cha 16(3), ambacho kama kilivyo sasa kwenye muswada kinasema kwamba hii taasisi inayotoa msaada wa kisheria ambayo ndani yake kuna Mawakili, kuna Wanasheria, kuna *Paralegal* ni kwamba mmojawapo kati ya hawa watu, hawa *office bearer,* aidha awe wakili au mwanasheria au *paralegal* akifanya kitendo chochote kinachokiuka maadili ya taaluma basi taasisi nzima inafungiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho yangu hapo ni kwamba tuweze kutenganisha makosa ambayo yamefanywa na *individual* wakili au mwanasheria au *Paralegal* yasiiadhibu taasisi nzima ikafungiwa kwa sababu ya kosa la mtu mmoja. Unaweza kukuta taasisi ina mawakili saba, ina wanasheria kumi, ina *paralegal* 20, kwa hiyo mwanasheria mmoja akifanya kitendo cha kukiuka maadili basi, eti taasisi nzima ifungiwe. Naona halijakaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maboresho yangu hapa ni kwamba, taasisi isifungiwe kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa sababu tu eti wakili mmoja au mwanasheria mmoja au *paralegal* wa ndani ya taasisi hiyo amefanya kitendo cha kukiuka. Badala yake huyo mtu mmoja ambaye amefanya kitendo hicho yeye ndiye aadhibiwe, kama ni kufukuzwa kazi na hiyo taasisi yake basi yambo hilo lifanyike, lakini taasisi nzima isiadhibiwe kwa kosa la mtu mmoja na tukiruhusu jambo hili litasababisha watu wetu kukosa haki muhimu ambayo tunaihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla niseme kwamba, sisi ni wawakilishi wa wananchi wa hali zote na tuna wananchi wengi kimsingi ambao kiukweli kabisa hali zao haziwawezeshi kumudu kulipia mawakili na kumudu huduma za kisheria ambazo zinalipiwa kwa gharama. Kwa hiyo, muswada huu lengo lake kubwa ni ku-*enhance access to justice* kwa watu wasio na uwezo wa kifedha wa kuwalipia mawakili na gharama nyingine za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa vyovyote vile mwakilishi yeyote yule ambaye anawakilisha watu wa aina hii hawezi kupinga muswada huu, atauunga mkono kwa sababu unakwenda kutoa suluhisho la wananchi wake anaowawakilisha ambao kimsingi hawana uwezo wa kulipia mawakili; na sasa hivi Serikali inakuja na programu ambayo watu hawa sasa wataweza kupata huduma hiyo bila kulipia, bila gharama yoyote. Kwa hiyo ni muswada ambao kimsingi unapaswa kuungwa mkono kwa nguvu zote na wawakilishi wote wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema naunga mkono kwa asilimia mia moja muswada huu, na ninasema muswada huu umechelewa sana, ulipaswa uje siku nyingi sana. Nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tumefika mwisho wa michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa muda ambao tunao. Sasa nitamkaribisha mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja hii mbele yetu. Hoja imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 13, Wabunge wanane kwa kuongea na wengine Wabunge watano kwa maandishi, wote nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuiangalia hii michango iliyokuja hapa, naomba tu kusisitiza kwamba wananchi wetu wengi hawajui kusoma na kuandika na sheria zetu zote zimeandikwa. Lakini pili, sheria zetu nyingi ziko katika lugha ya kiingereza, Watanzania wengi lugha hiyo ni ngeni kwao, hawaijui. Tatu, tuna mila na desturi zilizopitwa na muda ambazo wala hazitambuliwi na sheria za nchi za sasa, lakini kutokana tu na sintofahamu iliyopo maeneo mengi nchini kwetu mila hizo na desturi zilizopitwa na wakati bado zinatumika na kuumiza watu wengi sana hasa katika masuala ya ndoa, mirathi, umiliki wa mali kama vile ardhi, talaka, masuala ya *adoption* ya watoto na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zetu sehemu kubwa hazikubali utetezi kwamba hukujua sheria. Tunasema *ignorance of the law is not a defence.* Mpaka pale sheria kwa maneno yake itake wewe uwe na hiyo taarifa, iwe inataka hiyo *knowledge* uwe nayo. Kwa yote haya au katika hali hii tunahitaji sana huduma hii ya msaada wa kisheria ambayo imeshuka mpaka kwa wananchi wetu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mchango wa Kamati ya Katiba na Sheria, lakini nitagusia na mingine michache badae, ambayo inajibu maoni mengi yaliyojitokeza hapa, siwezi kuyarudia-rudia tena. Kamati ya Katiba na Sheria wamekuja na hoja ya kwamba katika kifungu chetu cha tafsiri neno "*advocate*" liendane na tafsiri iliyomo katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri *(Interpretation of Laws Act)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya tulijadiliana na Kamati na kimsingi tumeyakubali, lakini sisi tumeona ni vema zaidi tutumie sheria iliyo karibu zaidi na muswada huu ambayo ni Sheria ya Mawakili *(The Advocates Act, Cap. 341)*. Kwa hiyo, ni mapendekezo yetu kuwa tafsiri ya neno hilo kama ilivyo kwenye sheria mama badala ya Sheria ya Tafsiri itumike na itasomeka kama ifuatavyo; *"Advocate has the meaning ascribed to it under the Advocates Act."*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Kamati imesema maneno *Legal Advice* na *Legal Assistance* yatenganishwe katika kifungu kile cha tafsiri. Maoni haya pia tulijadiliana na Kamati. Tumekubaliana kuyaondoa na kuacha maneno *Legal Aid Services* ambayo tayari tafsiri yake imeshatolewa katika muswada huu na inajumuisha maneno *legal advice* na '*legal assistance'* kama sehemu ya *legal aid services.* Na ninaishukuru sana *Tanganyika Law Society* ndio waliotoa hiyo tafsiri. Sasa itasomeka, *Legal Aid Services include the provision of legal education and/or information legal advice assistance or legal representantion to indigent persons."*

Mheshimiwa Naibu Spika, neno "*Lawyer*" katika hichohicho kifungu cha tafsiri, lipewe tafsiri ili kutofautisha hawa wenzetu waliosomea sheria na *paralegals* yaani wasaidizi wa sheria. Tumeona neno sahihi la kuwatengenisha wenye Shahada ya Sheria na Wasaidizi wa Sheria, neno lenyewe ni Mwanasheria *(Lawyer)*. Hivyo, tunapendekeza tafsiri ya neno Lawyer isomeke kama ifuatavyo, *"Lawyer means any person who is a holder of a Bachelor Degree in laws or its equivalent and provides legal services under the legal aid provider in accordance with this act."*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile neno "*Paralegal*" Kamati ilitaka litafsiriwe. Mapendekezo yameafikiwa hivyo, tunatafsiri neno "*Paralegal*" kama ifuatavyo; *Paralegal means a person who is accredited and certified to provide legal aid services in accordance with provisions of this act.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, tumeshauriwa tuondoe, sasa tuko katika kifungu cha 6(2), tuondoe neno "*director*" badala yake tuweke neno "*person.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeafiki maoni ya Kamati na neno *director* limeondolewa na badala yake tumetumia neno *person.* Inaleta maana nzuri zaidi na sisi tumekubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inataka kifungu cha 7 kiboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni haya yameafikiwa, hata hivyo tumeongeza maneno ukienda kwenye kifungu cha 7, "*In consultation with a legal aid providers educational and training accreditation bodies*" ili kupanua wigo wa *consultation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilitaka wigo wa kusajili watu wenye taaluma ya sheria uongezwe, upanuliwe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili kwa kweli tumekubaliananao tumeliboresha kama ifuatavyo, tunataka *two advocates, one advocate and one lawyer, one advocate two paralegals, one lawyer, two paralegals or three paralegals.* Tumeona tuchukue *scenarios* mbalimbali ili hii huduma iweze kutolewa kwa urahisi popote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kifungu cha 13 Kamati inapendekeza kwamba *notice* ya kukataliwa kusajiliwa kwa mwombaji itolewe ndani ya siku saba baada ya maombi kufanyika, lakini baada ya majadiliano tulikubaliana na Kamati kwamba, *notice* ya kukataliwa itolewe baada ya siku 14 ambazo kwa kweli ni utaratibu wa kawaida katika Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 14, sheria iweke wazi haki ya rufaa ya mwombaji kama hajaridhishwa na uamuzi wa Waziri. Hili limeguswa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa maandishi na hata kwa kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni la rufaa dhidi ya uamuzi wa Waziri. Hata hivyo, kimsingi misingi ya haki ya asili *(principles of natural justice)* inampa fursa mtu kufungua shauri mahakamani hata bila kuelekeza, hivyo uamuzi wa Waziri hauwezi ukawa *final and conclusive,* hauwezi kuwa wa mwisho kama inavyofafanuliwa kwenye Sheria ya *Law Reform (Fatal Accidents and Miscellaneous Provisions) Act;* na tayari limekuwa likitendeka, umekwishakuwa utamaduni nchini hapa, hakuna uamuzi wa Waziri ambao hauwezi kupelekwa

mahakamani, na ndio utaratibu tunaoutumia katika sheria zetu. Sasa tukitaka kuwa *very prescriptive* pia sheria yetu haitaonekana *very tide*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 16 kuna ushauri kwamba mtoa huduma apewe muda wa kutosha kushughulikia tatizo na kutoa taarifa kwa Msajili kuhusu hatua alizochukua kabla ya Msajili kufuta leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na maoni ya Kamati, hivyo kimeongezwa kifungu kidogo cha (4) kitakachosomeka kama ifuatavyo; *"Notwithstanding the provisions of sub-section three the registrar shall not cancel a certificate of registration of the legal aid provider if it had notified the registrar in respect of paragraph (d), (e), (g) and has taken necessary internal measures to rectify the situation."*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala ambalo limebeba *interest* ya Waheshimiwa wengi ambalo pia, Kamati iligusia. Shughuli za siasa zifafanuliwe katika kifungu cha 16(1)(f) na vilevile ukienda kifungu cha 43 na Waheshimiwa Wabunge wengi mmeliongelea hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge tumeyaelewa, tumeyaafiki hivyo tunapendekeza kuwa kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya na kisomeke kama ifuatavyo ili kuondoa hizi hisia za kisiasa; *"A legal aid provider has discriminated aided person* yaani hicho ni kifungu kidogo cha (f), *a legal aid provider has discriminated aided person in terms of gender, religion, race, tribe or political affiliation."* Nafikiri mmelielewa hilo kwamba tumeipanua zaidi ili mtoa huduma huyo kwa kweli asioneshe upendeleo wa aina yoyote katika mazingira yoyote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 19; sheria iwatambue wasaidizi wa kisheria iwatambue wasaidizi wa kisheria wenye elimu ya sekondari na wale ambao wamekuwa wakifanya kazi hizo kwa zaidi ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yameafikiwa na kifungu hicho kimefanyiwa marekebisho hivyo tunakubaliana na mapendekezo hayo. Kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo, nitaomba kukisoma:-

*"19(1) A paralegal shall be required to possess any of the following:-*

*(a) Any Bachelor Degree say for a Bachelor Degree in Laws or its equivalent from an accredited institution."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapana hili nafikiri sasa nimejibu yote mawili. Kuna hii moja ya siasa nimeshaieleza, kuna hii nyingine ambayo naisisitiza nisije nikawa nimeichanganya, ya kwamba tutambue hata wale wa shule za sekondari limeongelewa mwishoni hapa na Mheshimiwa Zedi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waheshimiwa twende wote pamoja kwenye haya masahihisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, 19 tumeibadilisha sasa isomeke badala ya ile iliyopo huko. *19(1) A paralegal shall be required to possess any of the following:-*

*(a) Any bachelor degree save for a bachelor degree in laws or is equivalent from an accredited institution;*

*(b)Any diploma or certificate from an accredited institution; or*

*(c) Any certificate of secondary education.*

(2) *In addition to the requirement under sub-section one, a paralegal shall undergo necessary training as maybe prescribed in the regulations.*

*(3) Notwithstanding the generality of the provisions of sub-sections 1 and 2 any person who has been a paralegal for at least two years and has undergone training and the current arrangement prior to the coming into force of this Act, shall qualify as a paralegal for the purpose of this section."*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamelalamika watu wengi, lakini nafikiri tumeona sasa tuirekebishe kwa njia hiyo na; *19(4) subject to sub-section three the registrar shall have power to recognize and accredit paralegals trained under a registered legal aid provider.*

*(i) Who meets the basic requirements set out in the provisions of section 19(1) and;*

*(ii) In accordance with the proved curriculum."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20(c) na (f) vifutwe, havina mantiki, Kamati ilipendekeza hiyo. Tumeliangalia hilo kwa pamoja na sisi tumekubali vipengele hivyo (c) na (f) vimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati na Kambi ya Upinzani nao wameleta mawazo yao kwamba urasimu wa kutuma maombi ya kupatiwa msaada wa kisheria uondolewe. Kwa kweli mapendekezo haya sisi hatukuyapinga kwa sababu lengo sisi tupate sheria ambayo kila Mtanzania ataiona ni rafiki. Kifungu hicho pamoja na maelezo yake ya pembeni vimefutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo, ni kifungu cha 21-

*21(1) "An indigent person who intends to receive legal aid may approach any legal aid provider and apply for legal aid services.*

*(2) upon receipt of an applicationmade under subsection 1 the legal aid provider shall proceed processing the case."*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tusaidie, hayo marekebisho unayotusomea yapo kwenye Jedwali la Marekebisho au hapana?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ndiyo yote yapo.

**NAIBU SPIKA:** Kwenye Jedwali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Yah, yapo kwenye Jedwali. Wasiwasi wangu tu ni kwamba nikiyaacha pengine yatajirudia tena wakati tukiingia kwenye Kamati, nilitaka niwe *as detailed as possible*. Kifungu cha 20 (c); tumeshaongea hiyo, na ninafikiri tumemaliza hiki kifungu cha 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hoja ya kwamba tusiishie tu kwenye Mahakama, kuna umuhimu kwa wigo wa kupatiwa msaada wa kisheria katika Mabaraza ya Ardhi, Kodi na taasisi nyingine na huko tuwe na msaada wa kisheria. Mapendekezo ya kuongeza wigo wa mamlaka zitakazoelekeza mtu kupatiwa msaada wa kisheria yameafikiwa; mapendekezo hayo yatasomeka kama ifuatavyo:-

*"The presiding judge, a magistrate or chairman of the land, labour and tax tribunal and any other tribunal as the Minister may, by order published in the Gazette determine or adjudicatory body, shall cause such person to obtain legal aid."*

Na pia mapendekezo yameafikiwa ya kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo pia; *"Where the legal aid provider withdraws or is discharged by the client the legal aid provider shall immediately notify all parties to the proceedings and record of the facts."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani vilevile imeenda kifungu cha 29 hicho kilikuwa cha 21 kwamba mtoa huduma awe na haki ya kupokea sehemu ya tuzo ya Mahakama ili kufidia gharama. Mmemsikia hapa akiongelea Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Tundu Lissu. Maoni haya yameafikiwa, hata hivyo kanuni zitaweka utaratibu wa namna mtoa huduma ya msaada wa kisheria atakavyorejeshewa gharama alizotumia. Kifungu hicho kimefanyiwa marekebisho na kitasomeka kama ifuatavyo na nitaelezea kidogo:-

*"Where cost are awarded in any proceedings such cost shall be placed in the funds of the board provided that legal aid provider may have right to deduct from the awards the cost incurred in respect of the proceedings in the manner prescribed in the regulations."*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunapenda ifahamike kuwa msaada wa kisheria ni huduma inayotolewa kwa watu wasio na uwezo kwa maana ya kuwasaidia na si kwa maana ya kufanya biashara kwa lengo la kupata faida. Na hilo naomba nilisisitize kwa sababu hata alipokuwa anaongea Wakili Tundu Lissu hapa kwa kweli hakuongea kama Mbunge aliongea kama Wakili kabisa akiona kama Mawakili wanakuwa *short changed,* hapana. Hili ni suala la kujitolea na kila mtu ana wajibu wa kujitolea na hili ndio eneo pekee ambalo Mawakili vilevile lazima waoneshe *social responsibility.* Kama makampuni yanafanya hivyo *under corporate social responsibility* na sisi Mawakili katika eneo hilo.

Mhesimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Kanuni za Sheria ya Mawakili zinatoa motisha na kuwatambua Mawakili wanaotoa huduma ya msaada wa kisheria kwa kuwapa *CLE points (Continuing Legal Education)* ambazo mtu anazipata za mafunzo endelevu ya sheria kwa kutoa huduma ya msaada wa sheria. Na *point* hizi zina umuhimu wake, pamoja na mambo mengine humsaidia Wakili katika kuhuisha leseni yake ya kufanya shughuli zake za Uwakili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 36 kwamba Jeshi la Polisi na Magereza waweke mazingira ya kuwapatia msaada wa kisheria watu walio vizuizini, limeongelewa hapa. Mapendekezo haya kimsingi tumeyaafiki na kifungu hiki kitasomeka kama ifuatavyo:-

*36(1) The Police Force or Prison Services shall designate a mechanism for facilitating the provision of legal aid services by legal aid providers to accused or convict in custody in the manner to be prescribed in the regulations.*

*(2) Regulations made under subsection 1 shall be prepared in consultation with Minister responsible for Home Affairs.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 43 tumeombwa tuangalie namna ya kukiboresha hicho kifungu kama tulivyofanya kwenye kifungu cha 16 kuhusu masuala ya siasa. Kifungu cha 43(1) kinafutwa na kuandikwa upya ili kilingane na kile kingine kama ifuatavyo:-

*"Subject to the provisions of this Act no legal aid provider, advocate, lawyer or paralegal shall provide legal aid on the basis of discriminating aided person on his gender, religion, race, tribe of political affiliation."*Tumeona hiyo inaweza kuondoa kidogo *friction* hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati na Kambi ya Upinzani wameendelea kwenye kifungu cha 42 kwamba taratibu za mpito; taasisi zote ambazo zinatoa huduma za msaada zichukuliwe kuwa tayari zimesajiliwa na kupewa cheti kwa mujibu wa sheria hii. Ndugu zangu tumelijadili hili, tumeona mantiki yake, maoni yameafikiwa na kifungu hiki kimeboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kwenye jedwali kuhusu muundo wa bodi; kuna bodi mbili hapa inasemwa lazima ziongezwe. Maoni haya pia yameafikiwa na muundo wa bodi umerekebishwa kwa kuzingatia maoni ya Kamati yetu. Maoni yao ilikuwa ni kwamba kuwepo na mjumbe mmoja kutoka Chama cha Mawakili yaani *Tanganyika Law Society* na mjumbe mmoja kutoka Jukwaa la Haki Jinai; mtaona katika marekebisho tuliyoyafanya ambayo mmeyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Adadi Rajab pamoja na Kambi ya Upinzani, Serikali imekwepa kuanzisha taasisi mahususi ya kusimamia masuala ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini kama ilivyo kwa Kenya. Sasa kama kila kitu tuwe kama Kenya na wao watakuwa kama Tanzania lini? Sasa haya ni ya kwetu yanatuhusu sisi, utaratibu wa utoaji wa msaada wa kisheria hauna viwango ambavyo ni lazima vifanane au vilingane kati ya nchi moja na nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini msaada wa kisheria umekuwa ukitolewa kwa muda mrefu sana na kwa ufanisi mkubwa. Kilichokuwa kinakosekana kwakweli ilikuwa ni uratibu na utaratibu wa kuiona hili eneo likienda vizuri bila mikwaruzano hasa sasa hivi ambapo inapanuka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuangalia uwezo wa nchi yetu kila jambo linaanza kwa utaratibu na kwa hatua. Kwa kuanzia Serikali imeanzisha utaratibu tuliokuja nao na tunauona huu utaratibu ni muafaka, basi endapo mazingira yataruhusu na ninyi ndio Waheshimiwa Wabunge tulete hapa mapendekezo, tupanue wigo kama ilivyo kwenye nchi zingine kama kweli wenzetu ambao wameanza juzi tu kama nao wataendelea vizuri na kuwa watu wa kuigwa. Na inawezekana kabisa nchi nyingi nazo zikaiga kwetu baadaye kutokana na ufanisi wake kadri tunavyo endelea kutekeleza hili suala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa yeye amefika mbali kidogo kwamba atatumia Mfuko wa Jimbo kununulia vijana watakaokuwa wanatoa msaada wa kisheria pale pikipiki. Nampongeza sana kwa mawazo hayo, hata mimi mwenyewe nitawanunulia vijana wangu watakaofanya *legal aid* pikipiki ili waweze kumfikia kila mtu mwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 21 hadi 36 havioneshi ni makosa gani ya kutolea msaada wa kisheria. Hayo ni maoni yaliyotolewa na Balozi Mheshimiwa Adadi Rajab. Muswada huu ukiusoma umetoa masharti kuhusiana na masuala ya kutolea msaada wa kisheria. Nina maana hapa ukiangalia kifungu cha 27 kinatoa ufafanuzi wa namna ya utoaji wa msaada wa kisheria katika mashauri ya madai na kifungu cha 33 kinatoa ufafanuzi kuhusu mashauri ya makosa ya jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nina muda kidogo sasa nimalizie tu kusema Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Tundu Lissu kwakweli ametusaidia sana kwenye Kamati na mimi nilikuwepo hapo, lakini aliyokuja kuyasema leo kwa kweli sikubaliani nayo sana maana ametupa historia ndefu sana ya haki na msaada wa kisheria Marekani na kununukuu matamko mbalimbali ya Majaji wa *Supreme Court* ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili niliseme kidogo tu kwamba kwakweli kwa kipindi sasa hili Bunge naona kama kipimo halisi cha usomi hapa ni watu kuzama kwenye *google* na kuibuka na nukuu chungu mbovu za kizungu na wazungu lakini bila kuzingatia *context,* muktadha, bila kuzingatia mazingira na hata *historicity* ya hizo nukuu zenyewe. Nasema hivyo kwa sababu kipindi chote ambacho Mheshimiwa Tundu Lissu, mdogo wangu namuheshimu sana amekitolea mfano ni toka mwaka 1893 mpaka miaka ya 1960 ambacho ni kipindi cha ubaguzi wa rangi uliokubuhu Marekani. Na ukiongelea *legal aid* kipindi hicho haikuwa *legal aid* kwa mtu mweusi; ni mzungu na hauwezi kuwa mfano mzuri kwetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalichukulia hili suala kiwepesi sana, ni rahisi kupotosha vijana. Marekani katiba yao ni ya mwaka 1787 lakini Wamarekani imewachukua miaka 178 mtu mweusi kupata haki ya kupiga kura, tuanze kusema hayo ukweli. Sasa utapata *best practice* pale? Sisi ndio tunatakiwa tuigwe mfano na Marekani, tumepata uhuru mwaka 1961; 1961 hiyo hiyo mwarabu, mhindi na yeyote aliekuwepo hapa Tanganyika alipiga kura na wengi wazungu na wahindi wakawa kwenye Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mweusi amepiga kura marekani mwaka 1965 ndiyo maana nasema hiyo *legal aid* ilikuwa wapi? Halafu mimi kilichonisikitisha ni kule kunukuu sana *Supreme Court* ya Marekani, hiki ni chombo ambacho kimechangia sana kukandamiza haki ya watu weusi Marekani, na mimi nataka nimuombe mdogo wangu Tundu Lissu kama anaenda kutoa *lecture* Marekani asiseme haya mambo unaweza ukatupiwa mawe hivi hivi. Haiwezekani watu zaidi ya miaka 200 mnanyanyaswa halafu leo mtu unakuja una *sugarcoat* hiyo historia, sio vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba akasome pengine naona bwana mdogo wangu yupo hapa mbele hebu aandike hii kesi ya Dred Scott dhidi ya Sandford ya mwaka 1857 ambayo ni uamuzi wa *Supreme Court* ukisema kamwe mtu mweusi zao la mtumwa akawa raia wa Marekani, hiyo ni *supreme court* na hiyo usifikiri kwamba *extremity* hiyo ilikuwepo miaka ya 1800 ni mpaka 1965 *supreme court* ikiwa *very negative* kwa weusi. Sasa mimi kwenye haki hizi msaada wa kisheria tukiwa-*quote* sana watu hawa tunatoa picha tofauti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ningeomba tu Waheshimiwa Wabunge, tukiwanukuu sana wazee wetu kwa mfano, akina Mwinamila, Nyungu ya Mawe, Mkwawa, akina Nyerere, wameongea mengi mazito sana jamani yanayohusu haki na ndiyo waliyokuwa wanapigani – akina Kinjekitilie, lakini hawa akina sijui Winterbottom na kadhalika na *quotations* ndefu huku wanawakandamiza watu wetu, hiyo mifano haifai kwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema, kuna neno moja amesema, nchi zinazojali usawa mbele ya sheria kwenye hotuba yake na haki ya kusikilizwa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakyembe, tafadhali naomba umalizie.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia tu kwamba kuna hoja nzuri ambayo aliisema Mheshimiwa Tundu Lissu nilitaka

niizungumzie kidogo tu kwamba alisema nchi zinazojali usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa zimetunga sheria zinazolazimisha mamlaka za nchi kutoa msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi hatuhitaji kulazimishwa, sisi tumekuja kwa hiari kwa sababu haya ndiyo maendeleo taratibu ya nchi yetu, tumefika mahali ambapo sasa tunahitaji sheria hii ikamguse kila mtu kijijini ambaye anahitaji hilo. Nimalizie tu kwa kuwashukuru wote kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.
**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, nitawahoji baadaye. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2016 *[The Legal Aid Bill, 2016]*

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 4

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nili- *move* hiyo hoja na ku-*add member* wa *Tanganyika Law Society* ambayo imekubaliwa na vilevile nilitoa mapendekezo ya kuwatoa mapolisi na makamishna katika bodi na yote yamezingatiwa. Nashukuru.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 14

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki nilipendekeza tuongeze *clause* namba 4 ambayo Mheshimiwa Waziri alizungumzia.

Nilipendekeza kwamba kuwe na *clause* namba 4 inayosema; *"the institution which is aggrieved by the decision of the Minister may within 30 days from the date of receiving such decision, appeal to the High Court.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alizungumzia kwamba anaona sio muhimu sana kuiweka, lakini mimi kwa maoni yangu naona ni vizuri kuiweka kwa sababu, kama alivyosema mwenyewe, sisi Watanzania wengi bado hatujui haya mambo ya sheria na ingependeza zaidi kama hii *clause* ingekuwepo kwa watu wengine waweze kuelewa kwamba wanaweza ku-*appeal* pamoja na maamuzi ya Waziri, na sidhani kama inapunguza maudhui yoyote katika *clause* hii.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Ruth Mollel, isipokuwa badala ya kuwa rufaa ni *application* kwa sababu ile *Law Reform fatal accidents and Miscellaneous Provisions Act Cap. 360* ni *application,* zile *judicial review* huendi mahakamani kwa ku-*appeal.* Kwa hiyo fursa ya *appeal* imewekwa hapa, sasa kule una-*apply.* Kwa hiyo sasa kile kifungu kisomeke hivi:-

*"The institution which is aggrieved by the decision of the Minister may, within 30 days from the date of receiving such decision apply to the High Court for legal redress or for redress."*

**MWENYEKITI:** Kabla sijamkaribisha Mheshimiwa Ruth Mollel, kwa ajili ya uelewa, ile sheria uliyoitaja ya *Cap. 360 or something like that,* yenyewe inataja muda gani? Kwa sababu sasa ukisema *application* ya hapa unataka uiwekee muda mahsusi, ni afadhali hapa labda pakae hivi uache ile sheria akatumia huyo mtu kuliko ukambana hapa na siku 30 wakati kule kunatoa muda zaidi. Kwa hiyo, itabidi ajikute anatumia hizi siku 30 badala ya ule muda mrefu zaidi unaotolewa na hiyo *Cap. 360,* kwa hiyo hebu mtusaidie upande huu kabla hajasimama Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tungemuuliza Mheshimiwa kwa sababu hapo umemsaidia, yeye mwenyewe anaonaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lengo langu lilikuwa ni ninyi mtusaidie ili Waheshimiwa Wabunge tuelewe hata tutakapokuwa tunaamua hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollel, kwa sababu ninyi mkisema mmekubaliana kuweka siku 30 huku, huyu ambaye tunamtetea kwamba hajua sheria hizo siku 30 atazijua vipi ikiwa sheria nyingine ile inatoa mwanya mkubwa zaidi kuliko hapa mnapotaka kumbana; hicho ndicho ninachotaka mtusaidie ninyi hapo ambao ndiyo wataalam wa sheria. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata yeye mwenyewe Mheshimiwa Ruth Mollel alishanisikia nikieleza kwamba haukuwepo umuhimu sana kuweka yale aliyopendekeza, lakini anasisitiza tu kwamba Watanzania wengi hawajui. Tunamfahamisha tu kwamba katika miaka yote hii tumekuwa tunatumia sheria ambayo mtu ana haki, ni haki ya kufanya *application* kwenda *High Court* kupinga hayo, yeye ana-*insist* lakini sasa tunasema anacho-*insisit* sisi hatuwezi kupinga, hili ni Bunge linatengeneza sheria, lakini muda unaouweka hapa utawafanya wengi washindwe, warudie kule kule kwenye sheria ambayo sisi tunaitumia mara kwa mara ambayo tunajua kabisa maamuzi ya Waziri hayawezi kuwa *final and conclusive,* lazima mtu anakuwa na *access* kwenda *High Court*.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi si mwanasheria, lakini *AG* na yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri anaweza kuona ni jinsi gani ata-*craft* hiyo *paragraph* ninayoizungumzia kusudi yule mtu ambaye anakuwa *aggrieved* aweze kwenda ku-*appeal,* ajue kwamba anayo *venue* nyingine ya ku-*appeal* baada ya kushindwa kwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel hajatoa hoja, lakini sasa kwa sababu amesema yeye sio mwanasheria, Mheshimiwa Ruth Mollel, ukiweka humu muda maana yake huu ndiyo utakaotumika na kwa sababu kifungu hiki hakuna mahali kinasema maamuzi ya *Minister* ni ya mwisho ni vizuri kikakaa hivi kwa yule ambaye hajui, kwa sababu atakapopata muda ndipo ataweza kuomba kwa sababu ukimuwekea muda hapa italeta taabu, japo kuwa Serikali naona inakubaliana na hilo wazo lako la kuweka muda ila litamsumbua yule ambaye tunamtetea kwa sababu muda wake utakuwa mfupi zaidi kuliko ule uliopo kwenye sheria ile nyingine ambayo angeweza kuitumia.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaondoa hiyo ya muda na badala yake sasa kifungu kisomeke kwamba; *"The institution which is aggrieved by the decision of the Minister may apply to the High Court for legal regress."*

Kwa hiyo inakuwa *general,* sasa itakuwa itaongozwa na ile sheria ilivyo kule, japokuwa wataalam wangu wameniambia hata kwenye ile sheria ni zile siku 30 ambazo zimewekwa hapo, lakini tukiweka hivi inakuwa nzuri zaidi kwa sababu haitamfunga kama kule kwenye utaratibu wa ile sheria nyingine imekaa vingine.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo yako Mheshimiwa *AG* nadhani tutakuwa salama zaidi basi tukichukua kule kuliko tukaacha wazi unavyosema kwa sababu maana yake ile sheria kule imebana hii huku haina muda, sasa tutakuwa tunajiweka mazingira ambayo hatuhitaji, kama kuna haja ya kuongeza kifungu basi kiongezwe namna anavyosema kuliko kukiacha wazi.

Nadhani tufikie huo mwafaka ili tuweze kuendelea, tukichukue namna kilivyo kifungu ambacho maana yake ni kwamba ni sawa na kile kingine kwa hiyo hakuna tofauti, kwa hiyo, tuchukue cha kwake kama mnakubaliana upande wa Serikali tuendelee mbele.

Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukituruhusu basi ngoja tutafanya *cross reference* ya kile kifungu kingine, tutaifanyia hivyo.

**MWENYEKITI:** Vizuri. Mheshimiwa Ruth Mollel, hukuwa umetoa hoja na nadhani kwa namna walivyosema wamesema watakiweka hapa kwa namna ambayo kitakuwa kinaoana na ile sheria nyingine lakini kitaonesha kwamba mtu akienda kwa Waziri, Waziri akitoa maamuzi anaweza akaenda hatua nyingine, nadhani tutakuwa salama.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba muitikie ili tuweze kupata kumbukumbu sahihi za Bunge.

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa! Ahsante…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, sina jedwali lako la marekebisho.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia juu ya utaratibu kwa sababu kifungu hiki pamoja na 35 na 36 kinaonekana kama kimekuwa *wrongly placed* hakileti *clarity* na *consistency*. Kwa mfano ukisoma *sub headline* ya *page 16* inasema *legal aid and criminal matters,* lakini baadaye ndani huku kuna *expenses incurred by advocates*. Sasa nilikuwa nasema kwa ajili ya *clarity* kwa sababu vilevile hata 35 na 36 nili-*suggest* katika kamati kwamba kwa ajili ya *clarity* zi-*move* kabla mbele na si kuja mwisho ili ipatikane *sequence* kuliko kuleta suala hili la *legal aid* kwa watoto hapa wakati *sub heading* hapa ni *legal and criminal matters,* ije sehemu ya kwanza kuliko kuja sehemu ya mwisho, *that was my point*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tunaweza tukafanya namna yoyote tunayoona bora ya utungaji wa sheria, mapendekezo ya Mheshimiwa Ally Saleh kwenye Kamati hii ya Bunge Zima hatutaweza kuyachukua isipokuwa upande wa Serikali uchukue hayo maelezo yaliyopo, tutakapomaliza huu mchakato muangalie namna ya kuleta mabadiliko ya sheria, kwa sababu katika nafasi hii hakuna namna ya kuleta jambo jipya; lakini ameuliza swali kuhusu *clarity* na nadhani ukiisoma vifungu vya 34, 35 na hiyo 36 Mheshimiwa Ally Saleh, utakuta yana uhusiano na watu ambao wanaitwa hapo *accused person, convict* wote hao wanahusika kwenye *criminal matters* kama ulivyosema.

waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Mheshimiwa Ally Saleh umeishauri Serikali na imekusikia ikafanyie kazi hayo mawazo yako, lakini kwenye Kamati hii ya Bunge Zima hatuwezi kuchukua mabadiliko ambayo hatuna Jedwali la Marekebisho. Waheshimiwa tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42
Ibara Mpya ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizoyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2016 (*The Legal Aid Act, 2016)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Huduma Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2016 *(The Legal Aid Act, 2016)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wengi wameshinda waliosema ndiyo kwa hivyo tutaendelea na utaratibu unaofuata, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuratibu Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa watu wasiokuwa na uwezo, kuwatambua Wasaidizi

wa Kisheria, kufuta Sheria ya Msaada wa Kisheria katika mashauri ya kijinai na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo *(A bill for an act to regulate and coordinate the provision of legal aid services to indigeneous personel, paralegals, to repeal the legal aid criminal proceedings act and to provide for other related matters).*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2016 utaratibu wetu wa Kibunge umemalizika. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali na mtoa hoja kwa muswada huu muhimu ambao sasa Bunge hili limeshaupitisha na utasubiri taratibu zingine za kupelekewa Mheshimiwa Rais ili aweze kumalizia kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 97.

Tunaamini kwamba michango iliyotolewa na Kamati lakini pia na Wabunge waliopata fursa ya kuchangia, kwa kuwa yote mmeitilia maanani tunaamini sheria hii itaenda kufanya kazi ile iliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wale ambao hawawezi kulipia huduma za Mawakili. Kwa hiyo, hongereni sana Serikali lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha muswada huu ambao ni muhimu sana kwa jamii yetu kwa kadri mlivyochangia kwa pamoja. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka wakati akitaka kuchangia Mheshimiwa Anatropia Lwehikila, aliuliza kuhusu muda wa kupeleka marekebisho ama maboresho ya sheria kwa sababu wakati mwingine yanapopelekwa, Wabunge wanaambiwa kwamba wamechelewa kwa hiyo hayawezi kupokelewa tena. Kwa hiyo, nitoe ufafanuzi ambao ulikwishakutolewa katika Bunge lililopita yaani Mkutano wetu wa Tano mwezi Novemba, 2016.

Ukifuatilia hizi Taarifa Rasmi za Bunge utagundua siku ambayo Mwenyekiti Mheshimiwa Andrew Chenge alikuwa amekaa hapa, tarehe 4 Novemba, alikuwa ametoa muelekeo wa namna bora ya utungaji wa sheria na namna ya kuchukua marekebisho ya sheria ama Jedwali la Marekebisho kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kusaidia pia Serikali kuangalia namna ya kuweza kuyachukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge mapema. Wote mtaangalia namna tulivyoenda leo imekuwa rahisi sana kwasababu mambo mengi ambayo Kamati ilipendekeza upande wa Serikali umeyachukua, lakini hata yale ambayo Mheshimiwa Ruth Mollel alikuwa amependekeza pia kwa sababu alienda mapema upande wa Serikali umeweza kuchukua. Sasa nieleze, muongozo uliokuwa umetolewa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya tano kwa

sabaabu lazima tuongozwe na pia maamuzi yaliyopita ya Spika ama ya kiti. Si maelezo marefu sana, nitawasomea.

Tarehe 4 Mheshimiwa Chenge alitoa maelekezo na alisema hivi; tarehe nne mwezi Novemba, 2016 na aliendelea tarehe tano pia na yote nitayasoma si marefu sana, alisema hivi; "Waheshimiwa Wabunge ombi langu ni kwamba, kwa kuwa *schedule of amendments* za Serikali tunazo na ushauri ambao umeendelea kutolewa kwa upande wa Serikali wanajua yale ambayo wanadhani ni ya msingi lakini nawaomba Wabunge tukapitie hii *schedule of amendements* na wale ambao watataka kufanya *amendments* wakafanye usiku huu ili asubuhi ziweze kupatikana kwa wingi. Kwa sababu inakuwa ni kama fujo, tunapoingia kwenye Kamati ya Bunge Zima kunakuwa na lundo la marekebisho lakini ambayo yangeweza yakahakikiwa mapema na kuchujwa ili yakakae katika mtiririko mzuri. Sasa nendeni mkasome hizi *schedule of amendments* tuje vizuri na naamini tutaenda vizuri." Alikuwa anatoa maelekezo haya jioni ya tarehe nne mwezi Novemba, 2016 wakati tukiahirisha Bunge.

Tarehe tano asubuhi yakawepo malalamiko ya kuhusu *schedule of amendments* tena ama Jedwali la Marekebisho na akasema hivi; "Waheshimiwa Wabunge, *schedule of amendments* ambazo tumepokea ni ya Serikali na ya Mheshimiwa Waitara. Kwa sababau muswada huu tumekuwa nao, haitapendeza kuleta marekebisho kwa kuchelewa. Kama kuna Mheshimiwa Mbunge ana matamanio ya kufanya marekebisho, afanye hivyo mapema." Sasa anaendelea anasema; "ndiyo maana jana niliwaomba sana tujiandae ili asubuhi hii Katibu wa Bunge aweze kupokea mawazo ya kufanya marekebisho. Hatutaruhusu mtu kuleta marekebisho wakati wowote. Itakuwa ni vurugu tu maana Serikali na wenyewe lazima wapewe fursa ya kuyaona marekebisho hayo na kuyatafakari, lakini yakiletwa sasa hivi kule kwa Katibu maana yake hatuwezi kwenda zaidi ya kipindi hiki, itakuwa imesaidia sana shughuli za Bunge."

Waheshimiwa Wabunge kwa muongozo huu na kwa mujibu wa Kanuni yetu ya tano, ambayo inatutaka tutumie maamuzi ambayo yamekwishawahi kutolewa na kiti hapa, mapema iliyosemwa hapa ni asubuhi. Sasa pamoja na kwamba muda haukutajwa lakini asubuhi ya muda ambao utakuwa umempa fursa Waziri kuweza kuangalia ama upande wa Serikali kuweza kuyaangalia yale marekebisho yanayopendekezwa ili waone namna ya kuyachukua na wanapokuja hapa watueleze ni mangapi wamechukua ama ni yapi wameboresha kwenye yale wanayokuwa wanaleta wao, lakini yakipokelewa mpaka dakika za mwisho maana yake kwa muongozo huu ni kwamba kwanza yataleta fujo, lakini kimsingi ni kwamba hayataweza kupokelewa asubuhi.

Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Anatropia atapelekewa huo ujumbe lakini Bunge zima pia tupate huu muongozo utusaidie kwa sababu tutaendelea na miswada katika hizi siku mbili zijazo. Kwa hiyo, kwa mfano leo kwa sheria ya kesho maana yake mtu uwe umepeleka marekebisho yako, ama jedwali lako, ama upeleke kesho asubuhi siyo ukija humu ndani ukae kwanza halafu ndiyo upeleke. Kwa hiyo upeleke asubuhi na hayo ndiyo maelezo ama huo ndiyo muongozo kuhusu alichokuwa ameuliza Mheshimiwa Anatropia Theonest.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatano tarehe 1 Februari, 2017 saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.54 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 1 Februari, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*